ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Mhe. Pandu Ameir Kificho	-	SPIKA
1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi		- MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini		- MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary		-MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad		-MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban		-MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji		-MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed		-MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa

12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	-MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	-MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	-MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	-MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	-MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	-MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	-MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Omar Othman Makungu	- Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	-Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	- Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	-Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	-Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	-Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	- Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	- Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	- Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	- Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Salum Haji	- Jimbo la Kwahani
33.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	- Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asaa Othman Hamad	- Jimbo la Wete
35.Mhe. Asha Abdu Haji	- Nafasi za Wanawake
36.Mhe. Asha Bakari Makame	- Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Ashura Sharif Ali	- Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	- Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Farida Amour Mohammed	- Nafasi za Wanawake

40.Mhe. Fatma Mbarouk Said - Jimbo la Amani

41.Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Kwamtipura

42.Mhe. Hassan Hamad Omar - Jimbo la Kojani

43.Mhe. Hija Hassan Hija - Jimbo la Kiwani

44.Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Jimbo la Mji Mkongwe

45.Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Muyuni

46.Mhe. Kazija Khamis Kona - Nafasi za Wanawake

47.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa - Jimbo la Kikwajuni

48.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Jimbo la Kitope

49.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Jimbo la Mkwajuni

50.Mhe. Mgeni Hassan Juma - Nafasi za Wanawake

51.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma - Jimbo la Bumbwini

52.Mhe. Mohammed Haji Khalid - Jimbo la Mtambile

53.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi - Jimbo la Chambani

54.Mhe. Mohammed Said Mohammed - Jimbo la Mpendae

55. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak - Nafasi za Wanawake

56.Mhe. Mussa Ali Hassan - Jimbo la Koani

57. Mhe. Mussa Khamis Silima - Jimbo la Uzini

58.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

59.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Rahaleo

61.Mhe. Omar Ali Shehe - Jimbo la Chake-Chake

62.Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

63.Mhe. Rashid Seif Suleiman - Jimbo la Ziwani

64.Mhe. Raya Suleiman Hamad - Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Rufai Said Rufai - Jimbo la Tumbe

66.Mhe. Saleh Nassor Juma - Jimbo la Wawi

67.Mhe. Salim Abdalla Hamad - Jimbo la Mtambwe

68.Mhe. Salma Mohammed Ali - Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Salma Mussa Bilali - Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salmin Awadh Salmin - Jimbo la Magomeni

71.Mhe. Salum Amour Mtondoo - Jimbo la Bububu

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha - Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan - Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki - Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis - Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai - Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake

79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim - KATIBU

Kikao cha Sita – Tarehe 26 Januari, 2011

Kikao kilianza Saa 3.00 za asubuhi

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 50

Zanzibar Kunufaika na Jumuiya ya Afrika Mashariki

Mhe. Rashid Seif Suleiman - Aliuliza:-

Pamoja na ukweli kwamba Tanzania ndio yenye utambulisho katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, kuna haja ya kufahamu maeneo maalum ambayo Zanzibar ikiwa ni nchi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inaweza kufaidika moja kwa moja na kwa ukamilifu.

(a) Je, kuna hatua zipi zilizochukuliwa katika maeneo mbali mbali kwa Zanzibar kuwa na mchango (*Partner*) na kufaidika na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(b) Je, ni juhudi zipi zimechukuliwa na zimefikiwa wapi katika kuzifahamisha nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwamba Zanzibar ni nchi kati ya nchi mbili zinazounda Jamhuri ya Tanzania na hivyo, ingestah
ili kutambuliwa na kuheshimiwa kama ni nchi na sio mkoa ndani ya Tanzania.

Mhe.Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Zanzibar imetoa mchango mkubwa katika kuimarisha Jumuiya ya Afrika Mashariki miongoni mwa michango hiyo ni pamoja na wataalamu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wa sekta binafsi kushiriki kikamifu katika kuandaa na kupanga sera, sheria, mikakati na programu za Jumuiya wa Afrika Mashariki kupitia Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania. Kutokana na ushiriki huo Zanzibar ina fursa sawa kupitia Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama zilivyo Nchi nyengine wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika maeneo mbali mbali hususan katika matumizi wa soko la pamoja, ajira na kadhalika.

Pia mipango imepangwa kuhakikisha Zanzibar inafaidika kikamilifu katika mipango ya maendeleo ya Jumuiya ya AFrika mashariki. Mkakati wa Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kuimarisha huduma za usafiri 2010 -2020 *(EAC Transport Strategy)* umejumuisha pia miradi itakayotekelezwa Zanzibar. Miradi hiyo ni pamoja na mradi wa Ujenzi wa bandari Mpya ya Maruhubi, Mradi wa hudum za *Roll on Roll Off* na Mradi wa ujenzi wa *Upron* na *Tax way* katika Uwanja wa Ndege wa Zanzibar pia mradi wa kuimarisha Kiwanja cha Ndege cha Pemba.

b) Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni miongoni mwa Nchi Tano zinazounda Jumuiya ya Afrika Mashariki. Zanzibar inapewa umuhimu wa pekee katika Uwakilishi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye shughuli za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Katika kutekeleza hayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inahakikisha kuwa Ujumbe wake katika Vikao vya Jumuiya ya Afrika Mashariki unaishirikisha Zanzibar ipasavyo katika ngazi zote na ushiriki huo unaleta tija na faida kwa maendeleo ya Zanzibar na Watu wake. Aidha, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amepewa heshima ya pekee ya kualikwa katika vikao mbali mbali vya kilele (*summit*) vya Wakuu wa Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ahsante.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Kwa kuwa shughuli nyingi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zinashughulikiwa na Wizara ya Ushirikiano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo ni sehemu ya mambo ya Muungano.

(a) Je, yale mambo ambayo si ya Muungano kwa mfano kama ya afya, elimu na mengineyo yanaingizwa katika utaratibu gani ili Zanzibar iweze kufaidika moja kwa moja na hii jumuiya.

(b) Katika hali ya uzalishaji wa vitu au bidhaa kuingiza katika Jumuia ya Afrika Mashariki sisi tutapitia wapi ili zionekane bidhaa zetu kwamba ni Zanzibar tunaingia moja kwa moja au ni lazima ziwe *proved* na Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika,

(a) Hata kama mambo sio ya muungano kama nilivyosema kwenye jibu mama kwamba Zanzibar tumepewa nafasi yetu maalum ndani ya Jumuia, wataalamu wetu wanashiriki vikao vyote, vikao vya wataalamu, vikao vya makatibu Wakuu, vikao vya mawaziri hata Rais anaalikwa. Kwa hiyo ni fursa nzuri hiyo hata suala sio la muungano hulepeleka huko. Hilo tunashukuru sana, tunashiriki ipasavyo, wataalamu wetu wanakwenda, wanatetea hoja na mambo mengi sana tumeshafuzu na yameshakaa sawa kutokana na utaratibu huo.

(b) Kuhusu bidhaa nafikiri hili ni soko huria na soko la pamoja ni wajibu wetu kama Zanzibar kuzalisha bidhaa zenye viwango, tuzitie kwenye soko na sisi tufaidike kama wanavyofaidika wenzetu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa jawabu yake nzuri, lakini nataka niulize swali la nyongeza.

Mhe. Spika, kama tunavyofahamu kwamba jumuiya ya Afrikali Mashariki ni muunda mpya ambao tunakwenda kujiunga na tunapojiunga na Jumuia ya Afrika Mashariki tayari kuna baadhi ya sheria inabidi ziowanishwe ili zitekelezwe Kiafrika Mashariki. Lakini bado tuna tatizo katika ushiriki wa watendaji wetu hasa katika vikao vya mwanzo katika kuandaa baadhi ya sheria katika Jumuia ya Afrika Mashariki.

Je, Mhe. Spika, huoni kwamba fedha zilizotengwa kwa ajili ya ushiriki wa watendaji watu katika vikao vya Afrika Mashariki ni chache. Kama ni chache inapotokezea kwamba watendaji wetu hasa katika vikao vya mwanzo hawashiriki hatuoni kwamba yale maeneo ambayo Zanzibar pengine inaweza ikafaidika au inaweza ikapunjika tukaweza kuyakosa.

Mhe.Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba na nilisisitiza kwenye jibu langu la awali kwamba wataalamu wetu wanashiriki vikao vyote vya maandalizi ya kitaalamu. Kwa kweli tunapata heshma kubwa wataalamu wanaokwenda kule ni wazoefu, wanauchangamfu na wanajua hasa mada zinazozungumzwa. Na Hatupeleki kwa kuchagua.

Afisi yetu ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambayo ndiyo dhamana wa shughuli hizi za jumuia. Katibu Mkuu aliyeondoka ndugu Julian Rafael na sasa naibu katibu mkuu ambaye ni ndugu Natepe wanahakikisha wao

ni waratibu kwa wataalamu wa wizara nyengine. Kwa hiyo taarifa zikija tu tunazungumza na Makatibu wenzetu na fedha zipo za kutosha kwa sasa.

Hakuna tatizo la fedha kushiriki kwenye vikao hivyo. Hilo tunahakikisha kwamba bora vikao vya Mawaziri ambao zaidi tunakwenda kupitisha tu. Lakini vikao vya wataalamu ndio vikao vya kazi. Kwa hiyo hivyo tunahakikisha kwamba wanashiriki kikamilifu.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nakushukuru Mhe. Spika. Pamoja na majibu mazuri na ya kina ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, kwa kuwa katika makubaliano ya Muungano baina ya Jamhuri ya Watu wa Zanzibar na Jamhuri ya Tanganyika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepewa mamlaka kamili kwa mambo yote yasiyo ya Muungano na uendeshaji wake kwa upande wa Zanzibar. Kwa kuwa hilo linatambuliwa hata na Katiba ya Jamhuri ya Muungano inayotumika hiri sasa.

Kwa kuwa Mkataba wa Afrika Mashariki katika maeneo 17 yaliyotengwa kushughulikiwa na jumuia hiyo 13 katika hayo kwa upande wa Jamhuri ya Muungano ni maeneo ambayo sio ya Muungano.

Je, waziri haoni kama wakati umefika sasa serikali kuleta hoja katika Baraza la Wawakilishi ili Baraza lako lipitishe hoja ya kuitaka Zanzibar itambuliwe kama ni mwanachama kamili katika Jumuia ya Afrika Mashiriki kwa maeneo haya.

Mhe.Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, Mhe. Jusa katoa rai nzuri kwamba Zanzibar ishiriki kama nchi katika Jumuia ya Afrika Mashariki. Hilo ni wazo zuri lakini kwa sasa kwa utaratibu uliopo na hata katika Katiba yetu mpya kifungu cha (2) kinasema kwamba Zanzibar ni miongoni mwa nchi mbili zinazounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Sasa kama ni hivyo kwa sababu tupo chini ya mwamvuli wa Jamhuri ya Muuungano wa Tanzania. Kwa hivyo kwa sasa hatuna budi madhali tumeridhia muungano wetu twende na utaratibu huu. Hapo baadaye fikra yako nzuri tunaweza kuifanyia kazi.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais naomba niongeze jibu la nyongeza kutokana na majibu mazuri ya ambayo Mhe. Waziri ameyajibu.

Mhe. Spika, ni kweli nchi wanachama zinayo haki kupitia kifungu 150 za mkataba wa kuanzishwa Jumuia ya Afrika Mashariki kufanya mabadiliko katika mkataba huo kwa kuwaandikia rasmi Katibu Mkuu wa Jumuia na baadaye kushirikiana na nchi wanachama. Nchi wanachama zikubaliana mnaweza kufanya mabadiliko katiak kifungu chochote kile cha mkataba wa kuanzishwa Jumuia ya Afrika Mashariki.

Mhe. Spika, utaratibu tunaoendelea nao hivi sasa una nafuu kubwa kwa Zanzibar. Kwa sababu michango katika jumuia ya Afrika Mashariki ni zaidi ya dola Milioni tano kwa mwaka. Kwa maana hiyo Zanzibar inapata nafuu kubwa ya kutoa mchango huu kupitia Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Utaratibu huu unasaidia sana kutupunguzia gharama. Na kama alivyosema Mhe. Waziri kwamba utaratibu huu unatushirikisha kikamilifu kuanzia ngazi ya wataalamu, ngazi za makatibu wakuu, ngazi za mawaziri na hapa kuna gazeti linaonesha ushiriki wa Rais wa Zanzibar katika vikao vya kilele.

Kwa hivyo ni utaratibu mzuri tunaokwenda nao. Tukumbuke kwamba utaratibu huu baada ya maoni yaliyotolewa kwa Jamuhuri ya Muungano kwa pande zetu zote mbili za Zanzibar na upande wa Tanzania Bara. kwa hivyo naona kwa sasa utaratibu huu unatusaidia sana na ni vyema tukaendelea nao.

Nam. 52

Urejeshaji wa Ardhi kwa Wananchi

Mhe. Ussi Jecha Simai – Aliuliza:-

Makamo wa Pili wa Rais aliagiza kwamba wananchi wote waliony'ang'anywa ardhi kinyume na Sheria warejeshewe ardhi zao hizo.

(a) Je, Mhe. Waziri, Wizara yako imefikia wapi katika kutekeleza agizo la kiongozi huyo.

(b) Je, ni maeneo gani yaliyobainika kunyang'anywa ardhi wananchi kinyume na Sheria.

(c) Wahusika wa kosa hilo wamechukuliwa hatua gani za Kisheria.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 52 lenye vifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Kwanza ningependa nitoe maelezo ya utangulizi ili majibu ya swali hili yafahamike kwa kirahisi.

Mhe. Spika, kuanzia tarehe 8 Machi, 1964 kwa Sheria Nam. 13 ambayo ilitangazwa rasmi kwamba ardhi yote ni mali ya serikali. kuanzia tarehe hiyo hakuna mtu ambaye alikuwa na haki ya kumiliki ardhi isipokuwa kwa utaratibu wa kisheria ambao umeelezwa wazi wazi.

Wananchi wengi wa visiwa hivi waliendelea kutumia ardhi ambazo tayari zilikuwa ndani ya mikono ya serikali bila ya kupatiwa hati na haki ya matumizi waliyokuwa wakizitumia. Wananchi wengi waliimarisha kwa kupanda miti ya matunda ya kudumu katika ardhi hizo za ardhil halia na ardhi ya maweni na wengine katika miaka ya hivi karibuni wamekuwa wakipanda miti ya ujenzi na miti ya kuni kama mivinje na mikaratusi.

Wananchi wengi wamekuwa wakiendeleza vipando hivyo bila ya kuomba ridhaa ya serikali. Hata hivyo kwa mujibu wa sheria ya ardhi ya mwaka 1992 wananchi hao wanatambulika kumiliki miti na sio ardhi katika ardhi hizo za serikali. Inapotokea serikali kuzihitaji ardhi hizo kwa shughuli za kiserikali au ustawi wa jamii basi wananchi hao hudai wamenyang'anywa ardhi zao. Ikikumbukwa kwamba ardhi hizo waliachiwa wazitumie na sio wazimiliki.

Kwa mnasaba huo maelezo niliyoyatoa hapo juu ndipo chanzo cha matatizo ya ardhi yanapotokea.

Mhe. Spika, sasa napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi majibu yake yenye vifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Wizara yangu inasubiri hao walalamikaji ambao wanahisi kwamba Wizara yangu ndio iliyowanyang'anya basi walete maelezo yao na tutayashughulikia ipasavyo. Tokea Mheshimiwa atoe agizo hilo ni muda mfupi sana na inahitaji kupokea kwanza malalamiko kuyafanyia utafiti na hatimaye mwenye haki atapata haki yake.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, nataka kumuuliza Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi kama atakubaliana na mimi kifungu cha Nam. 56 cha mwaka 1992 cha ardhi. kinasema hivi:-

> "Serikali kabla ya kukifuta kiwanja kwa mwananchi aliyepewa kihalali lazima sababu za kufutwa kiwanja hicho ziridhishwe na mahakama."

(a) Je, Mhe. Waziri alifanya hivyo?

(b) Je, viwanja vilivyofutwa sababu zake zimeridhiwa na Mahakama?
(c) Fidia kiasi gani zilizolipwa viwanja hivyo vilivyofutwa
(d) Fidia ilipwe kiwanja kilichofutwa kutokana na *market* ya *value* ya kiwanja hicho kilipo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika mtu anapata hati ya kumiliki kiwanja baada ya kuleta ombi, wahusika wakakikagua kiwanja, na ikagundulikana kwamba kiwanja kile kipo na hakitumiki na wala serikali haina nia ya kukitumia mtu huyo hupewa hati miliki ya matumizi ya muda wa miaka 45, 66 au 99.

Mara tu serikali inapokuwa na haja ya kukitumia kiwanja kile kwa faida ya taifa au kwa faida ya jamii basi mtu yule *lease* yake hufutwa. Na kama hakufanya *development* zozote halipwi fidia. Na kama amefanya *development* basi atalipwa fidia inayostahiki kwa mujibu wa maamuzi ya wale wanaozingatia matumizi na thamani ya kile ambacho kitaondolewa.

Nadhani kwa jumla nimemjibu maswali yake.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwanza nimpongeze sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa kuona kwamba kuna baadhi ya wananchi wananyang'anywa ardhi zao kinyume na sheria basi warejeshewe.

Mhe. Spika, kwa kuwa kuna baadhi ya wananchi wamepewa heka na serikali. Na kwa kuwa siku za hivi karibuni kumejitokeza tatizo la serikali la kuwanyang'anya wananchi heka bila ya sababu ya msingi ni kwa ubinafsi tu.

(a) Je, Mhe. Spika, serikali haiyoni kufanya hivyo ni kwenda kinyume na mawazo ya muasisi wanchi hii Mzee Abeid Amani Karume.

(b) Je, Mhe. Waziri utanikubalia kuwa baada ya kikao hiki nikukutanishe na hao wananchi walionyang'anywa heka hizo ili upate ukweli wa jambo hili na uweze kulitatua.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, nakubaliana naye kwamba wapo wananchi waliopewa heka tatu, heka hizo wamenyang'anywa bila ya utaratibu sahihi. Nadhani hilo ndio kusudio la Mhe. Makamo wa Pili wa Rais la kwamba watu wa aina hiyo wakibainika kwamba wamenyang'anywa heka zao kwa dhulma basi warejeshewe eka hizo. Nakufanya hivyo ni kuheshimu matakwa ya Mhe. Rais wetu wa awamu ya kwanza Marehemu Shekh Abeid Amani Karume.

Nina kesi mbili tayari mikononi mwangu za Pemba, wahusika wamekuja kuniona nadhani baada ya tangazo la Mhe. Makamo wa Pili wa Rais. Tumezungumza kesi zao ziko wazi na wakubwa wamehusika katika kuzichukua ardhi hizo. Hao nimewaahidi nitakapokwenda Pemba nitayashughulikia mambo yao na Ishallah nitayamaliza kwa haraka sana. (*Makofi*)

Nam. 62

Wananchi wa Vijiji vya Mkwajuni Kunufaika na Huduma ya Umeme

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) - Aliuliza:-

Pamoja na juhudi zinazochukuliwa katika kusambaza umeme na maji safi katika maeneo mbali mbali Zanzibar, bado katika Jimbo la Mkwajuni, kuna baadhi ya Vijiji havijafaidika na huduma hizo.

(a) Je, Mhe. Waziri, kwa nini vijiji hivyo bado havina huduma hizo.

(b) Je, Wizara inajipanga kumaliza matatizo hayo lini.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 62 lenye vifungu (a), na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kama tunavyosema mara kwa mara kwamba nia ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuwasogezea huduma ya umeme kwa wananchi wa vijiji vyote vya Unguja na Pemba. Na kwa hilo kwa kiwango kikubwa tumelitekeleza na katika awamu mbili zilizopita za Mradi wa Usambazaji Umeme Vijijini, Jimbo la Mkwajuni lilibahatika kupata huduma hizo kwa kiwango kikubwa na naweza nikasema kwa asilimia 70 ya mahitaji ya umeme vijijini. Hata hivyo, kutokana na kuwa vijiji vingi miradi iliyokuja ya Norway awamu ya kwanza, pili, tatu na ya nne tulilazimika kugawa usambazaji wa umeme kwa Wilaya na kwa hali hiyo Wilaya ya Mkwajuni ilibahatika kupata huduma hizo.

(b) Namuomba Mhe. Mwakilishi kushirikiana na wizara yangu ili kuviingiza vijiji vilivyobaki katika Jimbo lake kwenye mpango wa usambazaji umeme ndani ya mwaka ujao wa fedha kama makisio tutakayoyapeleka yatakubaliwa vyenginevyo tutaendelea kugawa

umeme awamu kwa awamu, vijiji kwa vijiji na hatimae inshaallah tutakamilisha kazi hiyo.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii nimuulize swali moja la nyongeza Mhe. Waziri. Mhe. Waziri kuna baadhi ya vijiji katika Jimbo la Mkwajuni hasa vijiji vya Kibele Migombani na Muange viliwahi kupata huduma ya maji kama miaka mitano iliyopita nyuma. Mhe. Spika, maji hayo yalitoka kwa kipindi cha miezi mitatu mpaka minne lakini mpaka hii leo hakuna maji katika vijiji hivyo, mabomba yapo yamelala tu pale lakini maji hakuna.

Je, ni sababu zipi zinazochangia kuwa hakuna maji na wakati yalikuwa yanatoka na sasa hayatoki tena.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, suala la maji ni muhimu sana kwani linamgusa kila mwanadamu na kila kiumbe chenye uhai, Mhe. Spika, matatizo yake ni mengi sana na nimakubwa. Jibu sahihi ni kwamba tunajaribu kuangalia mtandao mzima wa maji kuyaangalia matatizo yale yaliyokuwa mazito na muhimu na sio ya Mkwajuni peke yake ni ya Unguja na Pemba. Mhe. Spika, tusipofanya hivyo tutakuwa tunafanyakazi nusu nusu hasa kwa tatizo la maji. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mwakilishi atupe muda kwani matatizo haya ni mengi na ya zamani sana, hivyo atupe muda ili tutakapokamilisha ufuatiliaji na utafiti na kujua matatizo yako wapi na ni makubwa kiasi gani basi nasema tutajaribu sina hakika kama tutafanikiwa bila ya kubadilisha *structure* yote ya maji.

Mhe. Spika, tutakapofanya hivyo basi si Mkwajuni tu lakini hata Donge tatizo hilo lipo, hata Makunduchi tatizo hilo lipo hivyo tutajaribu iwezekanavyo kulisawazisha.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, katika uongozi wa awamu ya sita wa Mhe. Rais Amani Abeid Karume serikali ilichukua nafasi ya kuwaagiza ndugu zetu wa *JAICA* kutatua tatizo la maji ndani ya miji ya Zanzibar.

Je, hawa wataalamu ambao walitoka nje kuja kutusaidia suala hili kazi yao ya utafiti pamoja na msaada ambao wameuotoa kutengenezea miundombinu pamoja na uwezekano wa kupatikana kwa maji haya. Je, kazi hii ilifanikiwa kiasi gani.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwa ghafla hii sitaweza kumpa jawabu sahihi kwamba kazi hii imegharimu kiasi gani

nitamletea kwa maandishi na kwa faida ya Baraza hili. Lakini nasema moja katika tatizo tulililoligundua kwamba kweli *JAICA* walikuja wakatusaidia sana, wakatuchimbia maeneo ya kupata maji na wakatupa baadhi ya mabomba ya kusambazia maji katika maeneo mbali mbali.

Mhe. Spika, kazi hiyo haikufanikiwa kwa kiwango tulichokitarajia kwa sababu kwa muda mrefu mabomba yaliopo hayakutumika mtandao wa maji mkubwa sana una matatizo yakujenga au kujaa *calcium* katika yale mabomba. Kwa hivyo, tuna mradi wa *ADB* na tuna mradi wa *UN*, miradi hii miwili mmoja kwa Pemba na mmoja kwa Unguja utandaza mabomba mapya ya plastik katika yale maeneo sugu yenye matatizo ili zile resources za maji tulizozitafuta na tukazipata tuweze kuzitumia vizuri na maji yaweze kuenea maeneo yanayotakiwa kwa kiwango kikubwa, sitaki niseme kwa asilimia mia moja lakini yataenea kwa kiwango kikubwa baada ya miradi hii miwili kumaliza kazi yake.

Nam. 83

Juhudi za Kuwakwamua Kiuchumi Wanawake Wajasiriamali wa Mkoa wa Kusini, Pemba

Mhe. Shadya Muhamed Suleiman - Aliuliza:-

Wanawake wengi wa Mkoa wa Kusini Pemba ni Wajasiriamali ambao wameunda vikundi mbali mbali vya Ushirika, ikiwa ni pamoja na kujishughulisha na ufugaji wa kuku na kutengeneza vitu vingi vyenye asili ya Mzanzibari. Hata hivyo, tatizo kubwa linalowakabili ni soko la uhakika la kuuzia biashara zao.

(a) Mhe. Waziri, wizara ina mpango gani wa kuwapatia wananchi hao soko la uhakika ili wauze bidhaa zao.

(b) Kwa kuzingatia umuhimu wa kuwakwamua wananchi hao kiuchumi. Je, wizara imechukua hatua zipi katika kulifikia lengo hili.

Mhe.Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo-:

a) Nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba upatikanaji wa soko la uhakika ni miongoni mwa changamoto zinazowakabili

wajasiriamali wetu. Lakini kama anavyofahamu, wizara yetu bado ni changa na tumo katika kujipanga kuandaa mikakati ambayo itasaidia katika kuwawezesha wananchi kuichumi. Tunafahamu kwamba moja ya tatizo linalowakwaza baadhi ya wajasiriamali ni upatikanaji wa soko la bidhaa zao.

Wizara yangu kwa kushirikiana na taasisi nyengine zinazohusika na masuala haya, italifanyia kazi suala hilo kupitia programu maalum ambazo zitaandaliwa ikiwemo zile zinazohusu utoaji wa mafunzo kwa wajasiamali waweze kuelewa mbinu za utafutaji soko pamoja na kuongeza ubora wa bidhaa zao ili zikidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya Zanzibar.

b) Kwa kuzingatia umuhimu wa kukwamua wananchi kiuchumi, Wizara yangu imeanza kuchukua hatua mbali mbali. Kwa kuanzia, imeweka idara maalumu ya kuratibu na kuendeleza programu za kuwawezesha wananchi kiuchumi. Idara hii, pamoja na mambo mengine itakuwa na jukumu la kubuni programu za kuwaendeleza wajasiriamali hususan wadogo wadogo katika maeneo mbali mbali ikiwemo mbinu za utafutaji soko na ujuzi wa kuimarisha ubora wa bidhaa zao ili ziweze kupata soko.

c) Soko. Idara hii pia itakuwa na jukumu la kufanya tafiti katika maeneo mbali mbali ya uwezeshaji, ikiwemo tathmini juu ya masoko na bidhaa ambazo zina uwezo wa kupata soko zaidi. Hii itasaidia wajasiriamali kupata ujuzi na ubunifu utakaowezesha bidhaa zao kuvutia soko zaidi na pia kupata taarifa zitakazowasaidia kuelewa ni aina gani ya biashara ambayo ina uwezo wa kupata soko.

Mhe. Muhammed Mbwana Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri kuna kauli kwamba wanawake ukiwawezesha wanaweza katika safari zangu za kuvitembelea vikundi vya wanawake jimboni kwangu kuna baadhi ya vikundi vimekusanya fedha karibu shilingi milioni saba hivi sasa wakiwa na nia ya kununua gari la mizigo kwa ajili ya kujikwamua kimaisha, lakini wamekwama kutokana na umasikini na mchango wao ni mdogo unaoendelea.

Je, Mhe. Waziri utawakwamua vipi wawanawake hawa ambao tayari wameshajiwekea rasilimali hiyo.

Mhe.Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, nakubaliana nae kwamba wanawake wakiwezeshwa wanaweza lakini hata wanaume nao wakiwezeshwa nao wanaweza kweli kweli.

Mhe. Spika, napenda nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba juzi nilipokuwa najibu swali Nam. 22 ambalo liliulizwa na Mhe. Salmin Awadh Salmin nilisema tayari tumeshajipanga kufanya ziara katika majimbo yote 50 kwenda kukutana na wananchi wa huko. Lakini kama kuna kikundi fulani au kuna wajasiriamali fulani katika maeneo ya majimbo yao ni kwamba fedha zipo za kukopesha na nakuomba Mhe. Mwakilishi tafuta ujumbe wako wa kikundi hicho mje wizarani kwangu basi mambo yatakuwa mazuri.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri kwa kuwa wanawake wengi bado hawajakutambua Je, Mhe. Waziri ni lini utawatembelea wanawake hao ili uweze kutambuana nao na kuweza kutatua matatizo yao.

Mhe.Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, nitafanya ziara za kuwatembelea na kuwakagua na kuona jinsi gani tunaweza kushirikiana nao na waweze kuniona huko kwa sababu sasahivi pengine wananiona kwenye televisheni au wanasikia habari zangu lakini nitakwenda *physical* wanione ili wajue uwezo wetu uko kiasi gani katika wizara hiyo.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, namuuliza Mhe. Waziri kuhusu matatizo ya mwani ni makubwa na yanautajiri mkubwa hapa Zanzibar lakini utaona wanaotajirika na wanunuzi wa mwani huo hivyo ana hatua gani ya kuwasaidia akina mama hao ili kupata bei nzuri ya mwani.

Mhe.Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, katika jibu mama nilieleza suala la msingi kwamba tutafanya mbinu ya kutafuta masoko kwa kuwasaidia wafanyabiashara na vikundi mbali mbali. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mwakilishi avute subra lakini pia nitashirikiana na wizara inayohusika na masuala hayo ya mwani ili tuweze kuona kwa kiasi gani tunaweza kusaidia.

Mhe. Spika, wizara hii kama nilivyosema juzi kwamba ni wizara ambayo ni MTAMBUKA itabidi kwa vyovyote vile ilivyo tushirikiane na Wizara ya Biashara, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Ardhi wizara zote katika njia moja au nyengine ili kuona kwa kiasi gani wananchi wetu tunawawezesha katika maeneo yao mbali mbali. Kwa hivyo, Mhe. Mwakilishi naomba ukae mkao wa kupata maendeleo katika jimbo lako.

Nam. 61

Utaratibu wa Huduma ya Ambulance

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) - Aliuliza:-

Tunapenda kuipongeza Wizara ya Afya kwa kutoa huduma ya gari ya kusafirishia wagonjwa (*Ambulance*), jambo ambalo linawasaidia sana wananchi wetu hususan wasio na uwezo.

(a) Mhe. Waziri kuna utaratibu gani unaotumika katika kutoa huduma hiyo, Mjini na maeneo ya Mashamba.

(b) Je, kuna gharama zozote ambazo mgonjwa anaepatiwa huduma hiyo analazimika kuilipia.

(c) Je, inaruhusiwa kwa gari hilo la wagonjwa kumfuata mgonjwa nyumbani kwake pale ambapo mgonjwa huyo amazidiwa na maradhi na kama hakuna ruhusa hiyo. Je, kuna sababu zipi zinazozuia kuwepo kwa utaratibu huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 61 lenye vifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifutavyo:-

Mhe. Spika, Wizara ya Afya inazo huduma za kusafirishia wagonjwa (*Ambulance*) katika Hospitali za Mnazi Mmoja, Mwembeladu, Cottage, Wete, Chake Chake na Mkoani.

Ambulance hizi hutumika kusafirishia wagonjwa kutoka hospitali moja kwenda nyengine kwa mgonjwa alieyepewa rufaa kutoka kwa daktari, na mara chache hutumika kuchukua wagonjwa kutoka nyumbani kupeleka hospitali.

Kawaida wagonjwa kutoka nyumbani kupelekwa hospitali na jamaa zao kwa usafiri binafsi hasa kwa kuzingatia kuwa vituo vyetu vya kutolea huduma ziko karibu na wananchi (chini ya Km 5). Hata hivyo, hakuna utaratibu wa kuzuwia *ambulance* kuwafata wagonjwa majumbani.

Hospitali ya Makunduchi kwa msaada wa wafadhili walionao wameanzisha utaratibu wa kuwafuata wajawazito wanaotaka kujifungua vijijini na kuwapeleka hospitalini. Mawasiliano hufanyika kwa kutumia simu za mikononi.

Huduma hizi hutolewa bure katika hospitali zote. Jamaa za wagonjwa katika baadhi ya hospitali kama vile Kivunge hutakiwa kuchangia kiasi kidogo cha fedha kwa ajili ya mafuta pale yanapomalizika, kwa vile mgao wa lita 200 kwa mwezi hautoshelezi.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nashukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Je, Mhe. Waziri ni kwa nini katika Hospitali ya Kivunge huduma hii ya *ambulance* inatolewa kwa malipo muda wote hata kwa wale wagonjwa wa rufaa na kama huna pesa mgonjwa wako wa rufaa anaweza kufariki kwenye hospitali ile kwa sababu tu ya pesa na hasa kina mama wale wajawazito wanapokuwa wamejifungua mara nyingi matatizo haya ndipo yanapotokezea.

Je, ni kwa nini tatizo hilo serikali halilitatui na wakati hospitali nyengine wanapata bila ya malipo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, tumesema kwamba huduma za ambulance ni bure na mgao wanaopata kila hospitali ni lita mia mbili na ndizo tunazopewa. Kwa hivyo, pale mafuta yanapokwisha ndio wananchi wanatakiwa kuchangia na nafikiri kuchangia huduma za afya ni moja ya sera zilizopitishwa na Baraza hili hili la Wawakilishi. Kwa hiyo, kama mafuta hayatoshi na hayapo dereva yupo na gari ipo kuna kosa gani wananchi wakiambiwa jamani tusaidie ili tumpeleke mgonjwa.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa katika jibu lake la msingi amejibu kwamba kazi ya *ambulance* hizi ni kuchukua wagonjwa kutoka hospitali moja kwenda hospitali nyengine, na mara chache sana kutoka majumbani hadi hospitali. Na kwa kuwa Vitongoji hospitali nayo imebahatika kupata *ambulance* hii, hivyo ambulance hii iliyoko Vitongoji Hospitali imepata ajali mbaya sana karibu miezi mitano iliyopita nyuma.

Je, Mhe. Waziri anajua kwamba sababu iliyosababisha ajali ya *ambulance* hii.

Wizara yake ni lini itafanya matengenezo ya *ambulance* hii kusudi kutoa huduma katika eneo lile la jimbo langu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, ni kwamba *ambulance* ya Vitongoji nimeiona kwa macho yangu kwamba imepata ajali na wakati nilipokwenda ilikuwa hata sio siku nyingi sijui sababu lakini kuiona kwa macho kwamba imepata ajali nimeiona. Kwa hivyo, mgao wa fedha na matumizi ya Wizara ya Afya ya Unguja na ya Pemba huwa unagaiwa sehemu

tofauti, Pemba wanapelekewa zao na Unguja wanabakiwa na zao hayo ndio makubaliano ya wizara. Kwa hivyo, ni jukumu la Wizara ya Afya Pemba kwa sababu kupanga ni kuchagua inategemea kiasi gani cha fedha wanazozipata kwa hiyo wakiamua kwamba safari hii tutakachokipata tutakipeleka Vitongoji kutengeneza ambulance hakuna utata wa hilo.

Mhe. Spika, kwa vile hilo ni jambo muhimu na wewe mwenzetu umeliona hebu fika kule Wizara ya Afya Pemba utakapokwenda uliulizie hilo na muone mtapanga vipi kuweza kusaidia hiyo *ambulance* ya Vitongoji iweze kufanya kazi.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, ni kweli *ambulance* imepata ajali na tulipofanya ziara tulilikuta na tulitoa maagizo kwamba litengenezwe lakini ndio matatizo ya utekelezaji kwa hiyo tukitoka hapa tutafuatilia tulimalize suala hili.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, madereva wa *ambulance* kazi yao kubwa ni kuwahisha wagonjwa kufika katika eneo jengine kwa mwendo wa haraka ili kunusuru maisha yao. Hivi hawa madereva wa *ambulance* wana bima za kinga za maisha yao katika kazi zao na kama hawana je, wizara ina mpango gani yakuwaekea bima kutokana na hali halisi ya kazi zao.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, mpango wa bima ya maisha Zanzibar haujaanza na tunategemea kwamba utaanza kwa hivyo mara nyingi inayokatiwa bima ni gari, hivyo hatujawa na utaratibu wa kukatia bima ya madereva kama mpango huo uanze utakuwa ni mpango wa serikali nzima na wizara yetu hivi sasa inaandaa waraka ili kufikisha serikalini wafanyakazi wote wa serikali tukiwemo sisi tukatiwe bima ya afya.

Nam. 36

Upatikanaji wa Madaktari Watakaoishi Kwenye Nyumba ya Madaktari Kojani

Mhe. Hassan Hamad Omar - Aliuliza:-

Ujenzi wa nyumba ya Madaktari katika kisiwa cha Kojani kupitia mradi wa *TASAF* umekamilika takriban kwa miaka mitatu sasa.

Je, wizara ina mpango gani wa kuwapatia wananchi hao wa kisiwa cha Kojani Madaktari watakaoishi katika nyumba hiyo na kutoa huduma za uhakika zaidi kwa wananchi wa kisiwa hicho.

Mhe. Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 36 kama ifutavyo:-

Mhe. Spika, Wizara ya Afya kila inapopokea wahitimu kutoka Chuo cha Afya Mbweni na nje ya Zanzibar huwapangia kazi katika sehemu zote za nchi hii. Hata hivyo kutokana na sababu mbali mbali wengi wao huwa hawako tayari kufanya kazi Kisiwani Pemba na vijijini.

Kati ya vituo vya afya tulivyonavyo tunavyowapangia wafanyakazi wetu wakiwemo daraja la kwanza, daraja la pili, cottage hospitali, hospitali za Wilaya na hospitali ya Rufaa.

Kituo cha Afya Kojani bado kinaendelea kujengwa kwa msaada wa *African Development Bank* (*ADB*) na hivyo nyumba ya daktari inatumika kutolea huduma za matibabu. Baada ya kumalizika ujenzi, nyumba hiyo itaendelea kuwa ni nyumba ya daktari kama wenyewe mlivyokuwa mmepanga iwe hivyo.

Kituo cha Kojani ni chenye hadhi ya daraja la pili (*PHCU+*) sasa nataka nitoe elimu kidogo kuhusu *PHCU+*. Tumesema kuna vituo vya aina 4 kituo cha daraja la kwanza ni *Primary Health Care Unit*, daraja la pili ni *PHU+* ina maana kwamba ni *Primary Health Care Unit* kama daraja la kwanza isipokuwa kuna nyongeza ya ziada pale. Sasa kituo cha Kojani kiko katika gurupu hilo na huduma zinazotolewa ni kama zifuatazo:

1. Huduma za msingi za magonjwa ya wanawake na uzazi.
2. Huduma za dharura za magonjwa ya wanawake na uzazi na kutayarisha rufaa ya mgonjwa kwenda hospitali ya wilaya, pale ambapo tatizo liko nje ya uwezo wao wa kitaalamu.
3. Huduma za mtoto aliyezaliwa.
4. Huduma kwa mzazi kabla ya kujifungua.
5. Huduma baada ya ujauzito kuharibika, kusafishwa mabaki ya ujauzito.
6. Huduma za vijijini kuhusu afya ya mama wajawazito.
7. Huduma za maabara.
8. Huduma za meno.
9. Huduma za ushauri nasaha kwa hiari.
10. Huduma za afya ya akili kwa mtu mmoja mmoja au kikundi.
11. Elimu ya afya ya akili, utambuzi na matibabu ya msingi ya maradhi ya akili.

Hizo ndizo huduma zinazotolewa katika *PHCU Plus* na ndizo zinazotakiwa zitolewe katika kituo cha Kojani.

Matarajio yetu ni kupeleka wafanyakazi zaidi kama daktari msaidizi, *clinic officer* kwa sababu ndio wanaotakiwa wawepo, muuguzi msaidizi, *PHNB* nurse wawili (*Public Health Nurse B*), mhudumu wa afya wa kinywa cha meno mmoja, mhudumu wa kituo, bwana au bibi afya, *health officer* mmoja, ufundi sanifu madawa. Kwa muda huu tayari mfanyakazi mmoja keshapelekwa kutoa huduma za kinga na tiba. Tunaamini hatua tulizopanga kuchukua kuboresha maslahi ya wafanyakazi zitasaidia kurahisisha upelekaji wafanyakazi sehemu zote za nchi yetu hasa Pemba.

Sasa hapa jamani Waheshimiwa Wawakilishi 'nnaangaliswa' (ninashangazwa). Mimi nilipomaliza kusoma *post* yangu ya kwanza ilikuwa Pemba na kama kuna mtu anatoka Kusini ya Pemba, Mkoani nafikiri ananikumbuka. Utaratibu wa serikali zamani ulikuwa hivyo, kwamba wanafunzi wanaomaliza miaka miwili aliyekuwa hatoki Pemba basi anafanya kazi Pemba halafu anarudi na hayo mambo yalikwenda kwa utaratibu mzuri tu na wanaotoka Pemba wanarudi Pemba. Baada ya kupata suala hili nimefanya utafiti nimekwenda Chuo cha Afya, wanafunzi walioko Chuo cha Afya asilimia 75 wanatoka Pemba, asilimia 25 wanatoka Unguja ukichukua ujumla wa wanafunzi walioko pale.

Mhe. Spika, tukimaliza tunawatawanya wale wanafunzi katika nafasi tofauti. Juzi tulikuwa Pemba jamani Pemba inasikitisha kwa ukosefu wa wafanyakazi na tatizo kubwa liliopo tukiwapanga wafanyakazi kwenda Pemba baada ya siku mbili tatu wakubwa kutoka humu humu na serikalini wanakwenda kuwaombea warudishwe Unguja. Wanatoka kule wanarudi Unguja, matokeo yake Pemba inabakia haina wafanyakazi, Unguja nao hawatoshi lakini wana afadhali ukilinganisha na Pemba.

Sasa Waheshimiwa Wawakilishi mimi nina ombi kwenu, tutafute njia muwafaka ambayo itaweza kuwafanya watu wetu watakaokwenda Pemba wabakie Pemba na suala la kuwatoa wanaotoka Unguja kwenda miaka miwili Pemba tutahakikisha linakuwepo.

Hivi sasa kuna wafanyakazi wanaotakiwa kuajiriwa kuna wanaotoka Pemba na Unguja, tutahakikisha wanaotoka Pemba tunawapeleka na wanaotoka Unguja watakaa Pemba miaka miwili ili ikisha warudi. Ikiwa tutafanya hiyo kazi kwa kipindi cha miaka mitano Wapemba watakwenda Pemba na wa Unguja watakwenda kwa mzunguko wa miaka miwili miwili kama ilivyopangwa zamani, Pemba hakutokuwa na tatizo. Kwa sababu kipindi hicho tulipokuwepo sisi Pemba hakukuwa na tatizo.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kupata nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuendeleza majibu ya Mhe. Naibu Waziri

katika Kituo changu cha Uondwe cha Afya kwa bahati mbaya kiasi miezi minane iliyopita daktari wake alikufa na mpaka leo hapana mwengine badala yake. Lakini pana kijana mmoja pale pale katika kijiji ambaye juzi tu kamaliza masomo yake katika Chuo cha Afya kilioko Mbweni, na mpaka nimeondoka kuja huku hajaajiriwa pamoja na kuwa nilipeleka ombi hilo la dharura ili aajiriwe.

Kwa sababu Mhe. Naibu Waziri kijana kama huyu yuypo na kuna pengo kama hilo la daktari. Sijui Mhe. Waziri atanisaidia vipi kwa hali ya dharura ili tumuajiri huyu kwa kuondoa lile tatizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, tunajua kwamba kuna upungufu wa wafanyakazi na hivi sasa kazi tunayoifanya ni kuhakikisha kujua kwamba kila kituo kina wafanyakazi wangapi waliopo na waliopungua ni wangapi na ni akina nani. Lakini tuna kazi moja ambayo tunatakiwa tuifanye, kuna huu mswada unaotaka kuletwa unaohusiana na masuala ya ajira, hatutopewa ruhusa kama huu mswada haukupitishwa ili kuweza kufanya kazi na wale waliotoka wakaajiriwa. Sisi kazi yetu tukimaliza na mswada huu ukipita wale waliotoka wataajiriwa na huyo wa kwenu atafika huko anakotakiwa kufika.

Nam. 45

Wanafunzi Kupatiwa Vikalio

Mhe. Rashid Seif Suleiman – Aliuliza:-

Pamoja na juhudi zinazochukuliwa na serikali kuhakikisha kwamba watoto wote wanaofikia muda wa kuanza masomo ya msingi wanapatiwa nafasi katika skuli mbali mbali za Serikali nchini, bado tunakabiliwa na tatizo la kukosekana kwa vikalio vya kutosha kwa wanafunzi wetu.

(a) Je, Mhe. Waziri, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba inalishughulikia tatizo hilo kwa haraka na bila ya kungoja misaada ya wafadhili.

(b) Je, wizara imeandaa mpango gani endelevu wa kumpatia kikalio kila mwanafunzi anayehudhuria skuli.

(c) Kwa kuwa hadi hii leo bado tunakabiliwa na tatizo hilo. Je, wizara inatuahidi mwaka gani itahakikisha kwamba imefikia lengo la kumpatia kila mwanafunzi kikalio chake.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.45 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba wananchi katika sehemu nyingi za nchi yetu wamejitokeza katika kuchangia ujenzi wa madarasa ya skuli katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu. Na kwa hili Mhe. Spika, nawapongeza wananchi wote.

(a) Idadi ya madarasa ambayo yamejengwa kwa nguvu za wananchi na yamefikiwa hatua ya kukamilishwa na serikali ni kama hivi ifuatavyo:-

Mkoa wa Mjini Magharibi kuna madarasa 72, Mkoa wa Kusini Unguja kuna madarasa 57, Mkoa wa Kaskazini Unguja kuna madarasa 105, Mkoa wa Kusini Pemba kuna madarasa 91 na Mkoa wa Kaskazini Pemba kuna madarasa 127 yote yanafanya jumla ya madarasa 452.

(b) Wizara inatarajia kuchukua kipindi cha muda wa miaka miwili kuweza kuyakamilisha madarasa hayo, hatua hiyo inatokana na uwezo wetu wa kifedha. Kwa mwaka 2010/2011 wizara inakusudia kukamilisha ujenzi wa jumla ya madarasa 120 Unguja na Pemba kama hivi ifuatavyo:

Mkoa wa Mjini Magharibi madarasa 19, Mkoa wa Kusini Unguja madarasa 22, Mkoa wa Kaskazini Unguja madarasa 26, Mkoa wa Kusini Pemba madarasa 24 na Mkoa wa Kaskazini Pemba madarasa 29 yatakuwa jumla 120.

Pamoja na mpango wetu huu wa ndani, wizara imeandaa andiko la mradi linaloelezea gharama za ukamilishaji kwa kila skuli na kuitafutia ufadhili kwa wahisani wetu wa maendeleo wa ndani na nje. Matokeo yanaonesha kwamba baadhi ya wahisani wameonesha nia ya kusaidia na wanaomba ufafanuzi zaidi juu ya mradi huu.

(c) Ingawa nia ya wizara ni kukamilisha majengo yote yanayoanzishwa kwa nguvu za wananchi, lakini bado skuli hizo haziwezi kukamilika katika kipindi hiki cha bajeti ya mwaka 2010/2011, kutokana na bajeti ya wizara kutoweza kukidhi ukamilishaji wa ujenzi wa skuli zote hizo.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika. Kwanza namshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri na ya kina. Mhe. Spika, wananchi

wetu ni masikini sana na wanajikamua sana katika kuendeleza ujenzi wa madarasa haya mpaka ile ahadi iliyochukuliwa na wizara kwamba ikifikia hatua ile watamaliza.

Kwa kuwa wizara inaonesha kushindwa sana katika kukamilisha madarasa yale, kwa nini haichukui dharura ya kuzuia kwanza ujenzi mpya mpaka haya yakamilike ili wananchi wasivunjike moyo na utaratibu huu.

Swali langu la pili ni kwamba, kwa nini hawaombi bajeti ya ziada kwa Mfuko Mkuu wa Serikali. Kwa sababu wananchi ndio wameshajitolea na mradi umeshafikia hapo. Kwa nini tena tuchukue muda mrefu sana na wakati mengine yatakuwa yanaendelea kuharibika bila ya kuezekwa na kushughulikiwa.

Lakini la tatu kwa sababu Sera ya Elimu ni kutoa elimu sawa kwa wanafunzi wote. Hatuoni kwamba wale tuliowaweka madarasa yao yakawa hayajakamilika tunawakatia ule utaratibu wa kutoa elimu sawa kwa wanafunzi wote.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwa mujibu wa idadi ya wanafunzi tulionao katika skuli, suala la kupata madarasa ya ziada ni suala la lazima. Pamoja na kuwa haya yaliyokwishajengwa hatujaezeka, lakini nia ya kuyaezeka na kuyamaliza ipo katika zile skuli ambazo bado zina matatizo kwa madarasa kuwa hayatoshi hatuwezi kuwaambia wasimamishe kujenga, waendelee na kujenga na wakijenga bila shaka tutayashughulikia kama tutakavyoyashughulikia haya mengine.

Mhe. Spika, ndio maana katika jibu langu mama nikasema kwamba, mbali na mpango wetu wa ndani lakini pia tunachukua juhudi ya kuwaomba wahisani watusaidie na kwa kweli wameanza kujichomoza wahisani wa nje ambao wako tayari kutusaidia katika kuyaezeka madarasa haya, isipokuwa wanataka ufafanuzi zaidi tu wa zile kazi zenyewe ambazo watazifanya wao. Kwa hivyo, tumuombe Mwenyezi Mungu wakubali ili tuweze kuyapata hayo na kupunguza msongamano wa wanafunzi katika madarasa yetu.

Mhe. Spika, bajeti ya ziada ya kuezeka madarasa haya sio jambo baya, lakini tatizo ni kwamba hiyo bajeti yenyewe ya Wizara ya Elimu ambayo inapitishwa katika Baraza hili tayari kipindi kilichopita tu, tumeomba kwa jumla ya shilingi bilioni arobaini na saba kwa Wizaraya Elimu. Katika matatizo, siiti matatizo naita changamoto kwa sababu ni mambo ambayo tumeamua kuyashughulikia. Katika mambo ambayo tumeamua kuyashughulikia hivi sasa mbali ya hizo ulizozitaja tunahitaji kwa madarasa tu 4.5 bilioni (milioni 4.5), tunahitaji bilioni nne kwa madawati angalau tupate madawati 20,000 ambapo jana Mhe. Ismail

Jussa Ladhu aliniuliza nilipoyafanyia kazi nikaona tukipata madawati 20,000 mambo yetu yanaweza yakawa mazuri.

Tunahitaji bilioni tano kwa ajili ya kuhudumia wanafunzi wanaosoma elimu ya juu, tuzipate hizo ni ziada ambazo ukizijumlisha utazikuta kwenye shilingi 13 bilioni ziwe za ziada. Njia zetu za kupata mapato tunazijua kwa hivyo, bila shaka itabidi twende katika utaratibu wa uhakika na ndivyo tunavyoendelea hivi sasa.

Kwa hivyo, nikijibu swali la tatu sio tunawakatisha, tunawaomba waendelee kwenda madarasani na jitihada tunaifanya na wote tutawashughulikia. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii. Naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja dogo tu la nyongeza. Rais Mstaafu Amani Abeid Karume katika ziara yake ya Pemba mwaka jana mwezi Machi alitembelea Skuli ya Kengeja. Hapo Mhe. Waziri alitoa ahadi ya kukamilisha mabanda ambayo tayari yamefikia hatua wizara kuyashughulikia. Lakini hadi hii leo hakuna chochote kilichofanywa. Kuna banda lenye madarasa saba ya *primary*, kuna na banda nyengine lenye madarasa manne ya sekondari na wizara iliahidi kwamba itayamaliza kabla ya kumalizika mwaka huu uliomalizika.

Je, wizara ina mpango gani wa kukamilisha majengo hayo ili watoto wapate kusoma.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, sio hakuna mpango wowote, mpango upo na ndio ule nilioupanga kwamba kwa mwaka huu tunakusudia kukamilisha madarasa 120. lakini nataka kulisema jambo ambalo Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi wanalijua, tusisahau kwamba tulipita kwenye Uchaguzi Mkuu, tulitumia fedha kwenye uchaguzi huo. Kwa hivyo, miradi mingi hatukuweza kuitekeleza mpaka sasa hivi ndio kwanza kipindi hiki tangu kumaliza uchaguzi mkuu tunaanza kuingiziwa pesa kwa ajili ya kushughulikia miradi mbali mbali. Kwa hivyo, namuomba Mheshimiwa aendelee kuwa na subira hiyo ahadi ya Mhe. Rais Mstaafu itatekelezwa bila shaka yoyote.

Nam. 84

Wanawake na Watoto Wanaotelekezwa

Mhe. Shadya Muhamed Suleiman – Aliuliza:-

Pamoja na juhudi zinazochukuliwa na wizara katika kuhakikisha kunapatikana maendeleo na ustawi wa Wanawake na Watoto katika jamii yetu, badi tatizo la kutelekezwa kwa wanawake na watoto linaendelea kutuathiri na kushamiri kila siku.

(a) Je, serikali imechukua hatua zipi za kulitokomeza tatizo hili.

(b) Je, sheria zilizopo hazitoshi kuondosha na kulitokomeza tatizo hili katiak jamii yetu.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Shadya Muhamed Suleiman Viti Maalum Mkoa wa Kusini Pemba swali lake nambari 84 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali kupitia Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto inaendelea na kuhamasisha jamii kuzielewa haki na sheria zinazomlinda mwanamke na mtoto, kupitia vyombo vya habari vya serikali na binafsi. Aidha inaendesha makongamano, warsha na semina katika ngazi za jamii kutambua wajibu wao katika malezi na makuzi ya watoto katika kamati za shehia za kuzuia unyanyasaji. Aidha, wizara inashirikisha na wazazi katika vikao vya kushajiisha kuhusu umuhimu wa kuzilinda haki za wanawake, watoto na haki za binadamu.

(b) Mhe. Spika, naomba kukubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba, sheria zilizopo hazitoshi kukabiliana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia kwa wanawake na watoto. Ndio maana wizara imo katika harakati za kutayarisha mswada wa sheria ya mtoto ambao utakapokamilika na kuwa sheria kamili utaharakisha upatikanaji wa haki kwa watoto wanaopatwa na madhila ya unyanyasaji na udhalilishaji. Aidha, wizara imeweza kuzikusanya na kuangalia ni

jinsi gani sheria ziliopo zinaweza zikakidhi haja katika kushughulikia kesi za udhalilishaji na unyanyasaji.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. kwa kuwa utelekezwaji wa wanawake na watoto uanathiri sana jamii yetu. Je, Mhe. Waziri kwa kipindi hiki cha miaka miwili hii suala hili la unyanyasaji wa watoto na wanawake limepungua kwa asilimia gani? Kama halijapungua limeongezeka kwa asilimia ngapi.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu mama kwamba sasa hivi sheria zilizopo hazikidhi haja katika kushughulikia mambo haya ya udhalilishaji wa kijinsia kwa wanawake na watoto. Kwa hivyo, sirahisi kwa sasa kutoa majibu kwamba tutalitekeleza kiasi gani suala hili ili liweze kuondoka kabisa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri namuomba nimuulize swali la nyongeza. Kwanza nataka nitoe pongezi maalum hasa kwa vyombo vya habari kwa namna wanavyofuatilia na kutoa taarifa mbali mbali hasa za udhalilishaji wa wanawake pamoja na watoto. Kwa kweli wanajitahidi sana na tunawapa pongezi hizo.

Mhe. Spika, swali langu lipo hapa. Pamoja na kwamba Mhe. Waziri amesema wako katika utaratibu wa kuandaa sera kwa ajili ya suala zima la wanawake na watoto, lakini tunajua kwamba tayari sheria zipo za kudhibiti masuala yote ya udhalilishaji wa kinamama na watoto.

Je, kutokana na udhalilishaji kuwa kila siku unaongezeka, hasa ubakaji wa watoto wadogo wengine chini ya miaka mitatu. Je, Mhe. Waziri haoni kwamba kuna haja sasa kuwa na Mahkama maalum ambayo itakuwa inashughulikia masuala ya udhalilishaji wa kesi za wanawake na watoto.

Lakini pili Mhe. Spika, Mhe. Waziri haoni sasa iko haja katika wizara yake kuwa na timu maalum ya kushughulikia hasa hizi kesi zinazohusu ubakaji na udhalilishaji wa wanawake na watoto kwa kuwa wananchi wetu wengi wanakuwa hawajui sheria. Wakati mwengine kutokana na uzunguushwaji wa hapa na pale hawajui au wanakata tamaa kuweza kufuatilia kesi za wanawake na watoto.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, ni kweli kwamba wapo baadhi ya wanawake ambao hawaelewi mambo ya sheria, lakini wako wengine wanaelewa sana mambo ya sheria. Kwa sababu kwa kufuata utaratibu jambo linapomfika kwenda

Mahkamani au Polisi, lakini maisha inakuwa ushahidi unapotea haupatikani na hivyo ile haki huwa haipatikani. Jengine naomba urudie kidogo.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, haoni Mhe. Waziri kutokana na udhalilishaji wa wanawake na watoto kuongezeka kila siku, haoni kwamba iko haja kuwa na Mahkama maalum ambayo itakuwa kazi yake kushughulikia kesi za wanawake na watoto.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwa sasa siwezi kutoa tamko kwamba kuwe na Mahkama maalum kwa ajili ya wanawake na watoto. Lakini nadhani hiyo itakuwa ni mipango ya baadae kwamba, ikiwa tutashindwa kabisa kuhusu udhalilishaji wa mama na mtoto unaendelea pamoja na sheria itakaporekebishwa na kuundwa upya, itakuwa tunashindwa kabisa hakuna maendeleo mazuri hata kidogo nadhani serikali pengine inaweza kuja kufikiria juu ya suala hilo.

Lakini sasa hivi Mhe. Spika, kuna mipango kabambe ambayo kwa vyovyote mtu atakavyojitahidi hawezi kupoteza ushahidi kama mtoto kweli amefanyiwa tendo baya. Jambo hili tumelipeleka kwa taasisi mbali mbali ili tukae pamoja na tatizo lolote likitokea basi lishughulikiwe haraka iwezekanavyo.

Mhe. Waziri wa Sheria na Katiba: Mhe. Spika, naomba niongezee kidogo kutokana na suala alilozungumza Mhe. Hamza Hassan na jibu ambalo ametoa Mhe. Waziri ni kwamba, kwa hivi sasa Mahkama za kitoto zipo zinaitwa *Juvenile Court*s. Kesi ya mtoto inapotokea Mahkama hizi ndizo zinazoshughulika kwa utaratibu maalum ambao uliwekwa kwa kuwahifadhi watoto hao.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe muda wa maswali unakaribia kumalizika na nimepewa taarifa na Katibu kwamba bado tuna maswali mengi yaliyobaji na muda wetu ni kesho na keshokutwa peke yake. Kwa hivyo, na leo tuongeze muda.

Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali: Mhe. Spika, kwa kuwa muda wa maswali umekaribia kumalizika na bado maswali yapo yaliyokuwa hayajajibiwa, naomba kutoa hoja kwamba tuangalie uwezekano wa kuongeza muda ili maswali haya tuweze kuyamaliza. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa anayekubali hoja anyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Nam. 37

Kunyanyua na Kuendeleza Michezo

Mhe. Nassor Salim Ali – Aliuliza:-

Kwa kuwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo ndio wizara inayohusika na michezo Zanzibar.

Je, Mhe. Waziri katika mfumo mpya wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa wizara yako ina mipango gani ya kuinua na kuendeleza masuala ya michezo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Rahaleo swali lake lenye nambari 37 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, katika mfumo mpya wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa imepanga mikakati kadhaa ya kuinua na kuendeleza michezo kama ifuatavyo:-

Wizara imekusudia kuinua michezo yote kufikia kiwango cha Kimataifa na kuweza kutoa ajira kwa wanamichezo wetu. Kuifanya michezo ni sehemu ya mipango ya maendeleo ya kupunguza umasikini MKUZA.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, mchezo wa mpira wa miguu ni mchezo ambao unapendwa Zanzibar na duniani kote kwa ujumla.

Mhe. Spika, serikali ya awamu ya sita katika kuona kwamba mchezo wa mpira wa miguu Zanzibar unapendwa iliweza kuleta kocha kutoka Misri kwa ushirikiano wa Ubalozi wa Misri. Kocha yule yuko hapa nchini lakini badala ya kuendeleza vipaji vya vijana wa *under* 17 pamoja na *under* 20 ambao ndio kazi aliyoletwa tumekuwa tukimuona akitoa mafunzo kwa timu za kawaida.

Je, wizara husika ina mpango gani wa kumpeleka kocha yule katika wilaya zote za Unguja na Pemba ili kutafuta vipaji kwa maendeleo ya vijana wetu kwa timu yetu ya Taifa ya hapo baadae.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, wizara yangu ina mipango na mikakati ya kuweza kumpeleka kila wilaya kocha yule kwa kuendeleza michezo na vipaji vya wanamichezo wetu.

Mhe. Salma Mussa Bilal: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, pamoja na mipango mizuri ya wizara yake ya kuendeleza michezo hapa Zanzibar. Je, wizara yake ina mipango gani ya kuendeleza mpira wa miguu wa wanawake hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, katika wizara yangu kwa sababu Naibu Waziri ni mwanamke na ataweza kuendeleza timu zote za mpira wa miguu wa wanawake Unguja na Pemba.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri amesema wizara yake kwa ajili ya kuipeleka Zanzibar katika hatua za kimataifa kimichezo wamedhamiria kufanya mipango mbali mbali. Kwa sababu Mhe. Waziri aliyepita Mhe. Ali Juma Shamuhuna alijitahidi na kuipeleka sasa Zanzibar kuweza kutajwa kwenye sifa. Je, Serikali mpya hii ya Umoja wa Kitaifa ina hatua gani za haraka kuifanya Zanzibar sasa kuwa mwanachama wa *FIFA* haraka iwezekanavyo.

Swali (b) amesema kocha huyu Mmisri wana mpango wa kumpeleka katika wilaya zote. Je, ni kwa mfumo gani watakaotumia ili aenee katika wilaya zote.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, ni kweli tayari Zanzibar inafikiriwa kuwa ni mmoja katika wanachama wa *FIFA* na hilo suala limeshakamilika na tunatarajia mwakani 2012 kikao cha mwisho kitakaliwa na FIFA ili kutoa idhini kwamba Zanzibar iwe nayo ni moja katika wanachama wa *FIFA*. Hata hivyo, pamoja na kwamba tunasubiri lakini bado tuna mawasiliano ya karibu ili kuona vipi masuala hayo yatafanyika.

Mhe. Spika, jibu (b) hilo ni suala la baadae wizara itakaa na kupanga tukishirikiana na Chama cha Mpira *ZFA* kuangalia uwezekano na mfumo gani wa kufanya suala hili. Nafikiri si suala zito kwa kweli.

Nam. 48

Serikali kuanzisha Ghala lake la Akiba

Mhe. Rashid Seif Suleiman - Aliuliza:-

Ili kupunguza mfumko wa bei nchini hususan katika chakula, Serikali imeshauriwa kuwa na ghala lake la akiba ya chakula *(strategic grain reserve)*, litakalosaidia upatikanaji wa chakula wakati wa upungufu ama kupanda kwa bei.

(a) Je, Serikali ina mikakati gani katika kufikia lengo hilo.

(b) Je, ni njia ipi nyengine inayofaa kuchukuliwa kudhibiti upandaji wa bei wa mara kwa mara wa chakula ambao unawaathiri wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 48 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Mhe. Spika, suala la kuwa na akiba ya chakula *(strategic grain reserve)* kwa ajili ya uhakika wa upatikanaji wa chakula wakati wa upungufu ama wakati wa ongezeko la bei ni jambo muhimu kwa nchi yoyote ile. Kwa kulifahamu hilo Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara yake ya Biashara, Viwanda na Masoko imekuwa ikifanyia kazi suala hili la kuwepo kwa akiba ya chakula. Kwa kuwa suala la uwepo wa takwimu za uhakika za mahitaji ya chakula *(food balance sheet)* ni moja ya masuala muhimu ya kuzingatiwa katika suala zima la uanzishwaji wa akiba ya chakula.

   Mhe. Spika, ninafuraha kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba pamoja na kuwa na kazi hii ya takwimu sio rahisi hata kidogo, lakini tayari takwimu halisi za mahitaji ya chakula nchini zimeshapatikana. Pia taratibu za kutafuta fedha kwa ajili ya kununulia bidhaa hiyo ya chakula zinaendelea kufanyika. Ni nia ya serikali hii kuwa na ghala ya chakula cha akiba cha angalau miezi mitatu ili iweze kukidhi haja endapo mahitaji yatatokea.

b) Mhe. Spika, katika kukabiliana na hali ya ongezeko la bei ya chakula pamoja na kuwa na akiba ya chakula, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili inawashajiisha wakulima kuongeza uzalishaji wa mazao hasa ya chakula kwa kuwapatia pembejeo na mbegu bora wakulima. Mhe. Spika, mpaka sasa Wizara ya Kilimo na Maliasili inatilia mkazo kilimo cha umwagiliaji maji ambapo inatarajia kulima karibu hekta 8000 za kilimo cha umwagiliaji. Juhudi hizi zitapelekea kuwa na akiba nzuri ya chakula na pia tunatarajia kwamba zitapunguza uagiziaji wa chakula na hasa mchele kwa asilimia 40.

   Mhe. Spika, hii inahakikishwa kwamba ndani ya nchi yetu tunao uwezo wa kuwa na chakula kwa kiwango cha asilimia 50.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, kwanza napenda nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri na kukubali uwezekano wa kuwa na ghala ya akiba katika visiwa vyetu. Lakini napenda nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

Kwa sababu ongezeko la bei za vyakula limekuwa likijirudia kwa miaka kama minne mfululizo sasa hivi. Je, Mhe. Waziri anatuhakikishia kwamba ghala hiyo ya akiba itakuwa tayari kwa kukabiliana na ongezeko hili la bei kwa kipindi cha mwaka unaokuja.

Lakini swali (b) alitueleza kwamba takwimu tayari imeshapatikana ya mahitaji ya chakula kwa Zanzibar. Je, kwa miezi hii mitatu tunahitaji tani ngapi za akiba.

Kwa sababu wakati Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anaukaribisha mwaka mpya alitoa hotuba yake na kueleza umuhimu wa kuwa na chakula cha akiba na alisema kwamba Tanzania sasa hivi tayari imeshajiwekea tani laki mbili za chakula na malengo yao ni kufikia tani laki nne. Mhe. Spika, napenda kujua kwa Zanzibar tumejiwekea malengo gani na tutaanza na kiasi gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, jibu (a) ni kwamba kwa hivi sasa wizara yangu imekuwa ikifanya mazungumzo ya karibu na wafanyabiashara ili kuongeza uagizishwaji wa zao la chakula hapa nchini. Halikadhalika imekuwa ikitoa wito kwamba wafanyabiashara wengi wajitokeze ili kujikita katika uagizishaji wa bidhaa hii ya chakula ili kupunguza umimi *(monopoly)* katika suala la biashara ya mazao ya chakula.

Mhe. Spika, vile vile Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko katika kulifanyia kazi suala hili la upungufu wa chakula au ongezeko la bei, basi imekuwa ikiweka utaratibu wa kuzipitia upya sheria zake zinazohusiana na masuala ya biashara.

Mhe. Spika, kuna sheria tatu ambazo zimepangiwa kufanyiwa mapitio, sheria ya kwanza ni ile Sheria ya Biashara ya mwaka 1989, lakini kuna Sheria ya Kumlinda Mtumiaji ya mwaka 1995, pamoja na Sheria ya Mizani na Vipimo ya mwaka 1983. Lengo kuu Mhe. Spika, ni kuleta ushindani halali katika soko hili la biashara.

Mhe. Spika, jibu (b) tani zinazohitajika ili kukidhi haja ya chakula hapa nchini ni kama ifuatavyo. Mhe. Spika, ili kuweza kukidhi haja ya mchele nchini ni tani 61,000 kwa mwaka zinahitajika na hapa nchini tunazalisha tani 8,000 na

wafanyabiashara wanaagizishia tani 53,000. Mhe. Spika, kwa bidhaa ya unga wa ngano tunahitaji tani 5,000 na kwa sukari ni tani 4,000. *(Makofi)*
Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe umeme umekatika na mawasiliano hayapo, tunaahirisha kikao kwa muda mpaka umeme utakaporudi.

(Saa 4:40 asubuhi Baraza liliahirishwa kutokana na kukatika kwa umeme)

(Saa 4:45 Baraza lilirudia)

Mhe. Spika: Kwanza niombe radhi Waheshimiwa Wajumbe umeme umekatika na hiyo ilikuwa ni sababu tosha ya kuweza kukatisha shughuli zetu kidogo. Hivi tunavyozungumza sasa tunatumia jenereta letu ambalo kwa kweli uwezo wake sio mzuri wa kutosha, mfumo wa hewa kidogo utakuwa matatizo humu ndani.

Tutajaribu kuangalia uwezekano wa kufungua milango baadae tuone kama itasaidia kuleta mfumo mzuri wa hewa. Kama itakuwa haiwezekani hivyo basi itabidi tuahirishe kikao baadae na tuone Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati atatusaidiaje. Kama ni jambo kubwa hiyo itakuwa ni dharura, kama ni jambo dogo la matengenezo basi waambiwe kwamba labda kuanzia kwenye saa saba na kuendelea kabla ya saa kumi na moja ndio wafanye matengenezo hayo, lakini tuweze kwenda na shughuli zetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe naomba radhi sana kwamba kwa sababu ya kukatika kule Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko na Naibu wake hivi sasa hawapo kwa hiyo tutaendelea na suala ninalofuata baada ya pale.

Nam. 65

Barabara kutopitika kwa sababu ya mvua

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Aliuliza:-

Kuna baadhi ya barabara za ndani katika Jimbo la Mkwajuni zimeharibiwa na mvua na pia hazipitiki, hivyo husababisha usumbufu kwa wananchi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuzifanyia ukarabati barabara hizo ili ziweze kupitika kwa muda wote wa mwaka.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 65 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kujibu swali husika naomba kurudia tena kutoa ufafanuzi nilioutoa nilipojibu swali Nam. 39 juu ya majukumu ya ujenzi na utunzaji wa barabara katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Barabara zetu zimegawika katika mafungu matatu makuu. Mafungu hayo ni 1. Barabara Kuu *(Main Roads),* 2. Barabara zinazounga Barabara Kuu *(Feeder /Secondary Roads)* na 3. Barabara za Ndani *(Town/Villages/Territory Roads).* Naomba pia kueleza kuwa sio kila barabara ama njia inayounga barabara kuu ni *feeder road* bali mgawanyo huo wa barabara na barabara hizo ni zile zilizoainishwa ndani ya Sheria ya Barabara, *Cap. 134.*

Kwa mujibu wa mgawanyo huo, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ina jukumu la kushughulikia makundi mawili ya kwanza, yaani *main roads* na *feeder roads* na barabara za ndani na zilizomo katika miji na vijiji ni jukumu la Mamlaka za Miji na Serikali za Mitaa.

Kwa kuzingatia hilo Mhe. Spika, swali la Mhe. Mwakilishi linahusisha moja kwa moja barabara zilizopo katika kundi la tatu ambalo ni zile hazipo moja kwa moja chini ya usimamizi wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Spika, pamoja na kuwa Wizara yangu haina jukumu la moja kwa moja kushughulikia barabara zilizomo katika kundi la 3; lakini kwa kuwa Serikali ina jukumu la kutoa huduma kwa wananchi wake, basi tumekuwa kila hali inaporuhusu tukishughulikia barabara hizo. Mara nyingi hushirikiana na mamlaka husika za maeneo na pia watu binafsi katika kuondoa matatizo yanayowakabili. Hivyo basi, namuomba Mhe. Mwakilishi awasiliane nasi ili tuweze kuona jinsi ya kutatua tatizo la barabara hizo za ndani za Jimbo la Mkwajuni kwa lengo la kuwapatia wananchi huduma nzuri.

Kama tulivyoahidi hapo awali wizara yangu iko tayari kutoa kila aina ya msaada katika kutimiza azma ya serikali ya kutoa huduma bora kwa wananchi wake. Napenda kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kuwa wizara yangu kwa ushirikiano wake na taasisi husika za Serikali za Mitaa na Halmashauri za Wilaya tutafanya ziara katika eneo hilo na kuona namna ya kulipatia ufumbuzi suala hilo la barabara katika Jimbo la Mkwajuni.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri amesema tuwasiliane ili tushirikiane na mamlaka nyengine kuweza kwenda kukagua hayo maeneo, mimi naomba aniambie tu ni lini tutakwenda kukagua hayo maeneo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, napenda kumhakikishia kwamba mara tu baada ya kumaliza kikao hichi cha Baraza wizara yangu iko tayari kufanya ziara. *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mji Mkongwe ni eneo linalotoa sura ya taswira ya nchi yetu nzima ya Zanzibar na barabara zake nyingi za ndani *(feeder roads)* zimekuwa katika hali mbaya sana na hazipitiki, kuanzia eneo la Mji Mkongwe wenyewe hadi katika maeneo ya Mwembetanga na Vikokotoni.

Kwa kuwa katika ufunguzi wa Jumba la Maendeleo la Michenzani Nam. 10 Rais Mstaafu Mhe. Dk. Amani Abeid Karume alitoa agizo wakati ule akiwa Rais, kuwa wizara sasa baada ya kushughulikia barabara kuu kuzishughulikia barabara hizi katika mji. Sijui Mhe. Waziri anaweza kutwambia wizara ina mpango gani kutekeleza agizo hili na lini wananchi wa Mji Mkongwe wategemee watafaidika na kuona barabara zao pia zinakuwa katika hali nzuri zilizokuwepo katika maeneo ya ndani.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, katika majibu mama tulieleza barabara ambazo wizara yetu inahusika lakini hapa kuna maagizo ya Mhe. Rais. Mhe. Spika, napenda nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba tutashirikiana na mamlaka husika kwa maana ya kwamba uendelezaji wa Mji Mkongwe kuona namna ya kulitekeleza agizo la Rais aliyestaafu.

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, Jimbo la Kikwajuni ni jimbo ambalo lina haiba nzuri na tuna utaratibu mzuri kule wa kutengeneza hili zao la asumini kwa kuwajaalia hawa wageni wanaokuja. Lakini katika jimbo hili Mhe. Spika, tuna jumba Nam. 10 ambalo limejengwa katika utawala wa serikali ya awamu ya sita. Jumba lile upande wa nyuma huku ukiangalia ile haiba na uzuri wa lile jumba inapotea kutokana na barabara ambayo iko katika mazingira magumu sana.

Je, Mhe. Waziri atatueleza nini juu ya suala la barabara zetu zile za ndani ambazo zinaunganika pamoja na barabara ile. Ni kwa muda gani atatutimizia ili na sisi tuweze kujisikia utamu zaidi katika Jimbo letu la Kikwajuni.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, napenda tena kurejea kauli yangu niliyoitoa nilipojibu swali Nam. 39 na niliyoitoa leo nilipojibu swali Nam. 65 juu ya namna ya barabara ambazo zinashughulikiwa na wizara yangu. Tumezieleza na ninaamini barabara anayoielezea Mhe. Mwakilishi ni barabara ambayo inastahiki kusimamiwa na

kuendelezwa na halmshauri na mamlaka husika ya mji wa Zanzibar. Lakini wizara yangu pale fursa na nguvu zitakapotokezea tuko tayari kusaidiana na wahusika katika kutatua kero za wananchi wetu. *(Makofi)*

Nam. 68

Uwezo wa Bandari ya Zanzibar

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa – Aliuliza:-

Tunaipongeza Serikali kwa kukamilisha ujenzi wa Bandari ya Malindi ambayo pamoja na kasoro ndogo ndogo ina nafasi kubwa ya kuinua uchumi wa nchi yetu.

(a) Je, bandari hiyo ina uwezo wa kuhudumia meli za aina gani na zenye ukubwa wa tani ngapi.

(b) Je, Shirika la Bandari lina vifaa vya kutosha kuweza kutoa huduma hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 68 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Bandari ya Malindi ina uwezo wa kuhudumia meli za aina mbali mbali zikiwemo meli za mizigo mchanganyiko, meli za makontena, meli za abiria, meli za mafuta na magari *(Ro-Ro)* pamoja na meli za kivita.

Meli zinazoweza kuhudumiwa ni zile tu zenye urefu wa hadi mita 200 *(LOA)* na ukubwa wa *GRT* 26,000 na uzito wa tani 13,000 *(DWT)* kulingana na vipimo vya ujenzi wa gati hiyo. Ingawaje baadhi ya wakati meli kubwa zaidi zimeweza kuhudumiwa kwenye gati hiyo.

(b) Shirika la Bandari lina vifaa vya msingi vya kuhudumia meli hizo ingawa si vya kutosha kukidhi matakwa ya utoaji wa huduma hizo. Kwa mfano, tagi zinazotumika hivi sasa kusaidia ufungaji wa meli uwezo wake ni mdogo kulinganisha na ukubwa wa meli zinazokuja hapa Zanzibar. Kadhalika kuna ukosefu wa krini za kushushia mzigo moja kwa moja kutoka melini hadi kwenye gati.

Mhe. Spika, Serikali kupitia Shirika la Bandari limeshachukua hatua za kununua krini mbili mpya ambazo zinategemewa kuwasili mwaka huu wa 2011 kukabiliana na upungufu huo. Tunaleta krini hizo ili kuweza kukabiliana na upungufu huo tulioueleza.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wafanyabiashara juu ya kukawia kutolewa kwa mizigo hapo bandarini yanayosababishwa na Shirika la Bandari. Kwa kuwa Mhe. Waziri ameeleza kwamba ana vifaa vya kutosha vya kufanyia kazi. Je, ni tatizo gani linalosababisha mizigo hii ikakawia.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, tumeeleza katika jibu mama upungufu wa vifaa vilivyopo katika bandari yetu. Mhe. Spika, suala la kuchelewa utoaji wa mizigo ni suala lenye sababu nyingi miongoni mwao ni upungufu wa nafasi uliopo bandarini, lakini pia uelewa mdogo au kutokukubali kufanya kazi kwa wafanyabiashara wetu kulingana na matakwa na maelekezo wanayopewa na mamlaka husika ya bandari. Ucheleweshwaji huu wa wafanyabiashara wetu nao unachangia kwa sehemu kubwa kuchelewa kutolewa kwa mizigo yao.

Mhe. Spika, naomba kutoa wito kwa wafanyabiashara wetu wawe wasikivu wenye kufuata maelekezo wanayopewa na taasisi husika katika namna ya utoaji mizigo bandarini ili kuondosha ucheleweshaji. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, huduma ya maji imekuwa ni huduma muhimu sana kwa binadamu na ndio kilio chetu kikubwa sana katika Baraza hili. Mhe. Spika, kumekuwa na usumbufu mkubwa sana kwa meli zinazokuja kufunga gati Zanzibar kutia maji. Ni sehemu moja tu inayopatikana pale kutia maji ukuta namba moja, lakini ukuta namba tatu iko *cork* imefungwa mpaka leo haijafunguliwa na maji yapo.

Je, Mhe. Waziri atachukua hatua gani za dharura kunusuru suala hili hasa kwa meli zetu zinazokwenda Pemba na ukiangalia abiria wanaopakia kuwa ni wengi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ni kweli katika Bandari yetu ya Malindi tumekuwa na upungufu wa maji, lakini upungufu huu unatokana na matatizo mengi, yakiwemo miundombinu ya maji yenyewe yaani upatikanaji wa maji yenyewe.

Mhe. Spika, kama ilivyoelezwa hapo awali suala la maji ni tatizo sugu katika nchi yetu. Kwa upande wa bandarini hali kadhalika suala hili lipo. Napenda nikuhakikishie kwamba baada tu ya kufanya uchunguzi na kuona namna ya kulipatia ufumbuzi, basi wizara yangu kwa kushirikiana na mamlaka husika Shirika la Bandari kutoa namna ya kufungua maeneo yote ili kuweza kuwapatia huduma hiyo muhimu kwa wananchi wetu.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali moja la nyongeza kwa Mhe. Naibu Waziri. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri. Mhe. Spika, hivi karibuni kulizama mali ya Fatihi, lakini kutokana na muda mwingi wa kuweza kuiokoa meli ile kwa kutokana na vifaa ambavyo sio vya kisasa, ndio ikabidi serikali iweze kukodi na watu wakaendelea kufa na vitu vikaendelea kuharibika.

Je, wizara yako ina mpango gani hivi sasa kuweza kutafuta vifaa ambavyo ni vya kisasa na kuweza kuokoa ajali kama ile isiweze kutokezea tena?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ni kweli hapo nyuma kulitokezea ajali ambayo sio malengo ya wizara wala watoa huduma wetu wa vyombo wanaowasaidia watu kusafiri. Mategemeo ya serikali ni kutafuta vifaa, sio tu kwa ajili ya kuzuia ajali, lakini kurahisisha huduma za wananchi wetu katika bandari yetu ya Zanzibar.

Mhe. Spika, nimuhakikishie Mhe. Mjumbe kama majibu yetu ya awali tulivyosema kuwa tumeanza kwa kutafuta *crane* kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa mizigo bandarini na vifaa vingine tunahakikisha kadiri hali itakavyoruhusu tutavitafuta, ili kufanikisha malengo na madhumuni ya huduma bora kwa wananchi wetu.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa ufafanuzi zaidi kwa suala ambalo Mhe. Naibu Waziri Miundombinu na Mawasiliano amekuwa akilijibu kama ifuatavyo. Mhe. Spika, ajali baharini ni kama ajali za mahali pengine popote. Lakini kwa kuzingatia hilo ni kweli kwamba bandari yetu na mamlaka yetu ya usalama wa baharini ilikuwa haijapata vifaa vya kutosha. Tumeandaa mradi maalum chini ya mamlaka mpya, *Zanzibar Maritime Authority*, ili kuhakikisha kwamba bandari yetu ina viwango vya kimataifa na kwa mujibu na kwa mujibu wa (IMO) *International Maritime Organization.* Miongoni mwa vifaa hivyo ni *rescue boat*, boti ya kuokolea ajali zinazotokea baharini.

Vile vile kuwa na *fire extinguish system* bandarini ni mahali ambapo kuna vifaa vingi vya hatari. Kwa hivyo, kama huna vitu vya kuzimia moto basi vile vile ni *risk* nyengine. Pia tunataka tuwe na uhusiano mzuri na wenzetu wa bandari

nyengine za kimataifa. Timu hiyo tunatarajia ifike hapa katika mwezi wa Mei mwaka huu, ili kukaa pamoja na kutuongoza vizuri, ili bandari hii pamoja na shughuli zake zote ijulikane duniani kote kuwa ni bandari ya kimataifa na vifaa vinavyotoka hapa kwenda mahali pengine popote visiwe na wasi wasi tena, kama ambavyo sasa hivi nchi nyengine wanao. Kwa hivyo, watuelekeze ni nini tufanye na watatusaidia vipi katika kufikia lengo hilo.

Mhe. Spika, ni kweli ajali ya Fatihi ilitokea kama ilivyotokea, hatukuwa kweli tumejipanga na hata kama tungekuwa tumejipanga, lakini hatukuwa na vitu vya kutosha vya kuokoa. Tuna utaratibu huo katika, "ukupigao ndio ukufunzao". Mhe. Spika, *Inshaallah* tutakuwa na mpango mzuri wa kuokoa ajali kama hizo.

Mhe. Spika: Nakushukuru Mhe. Naibu Waziri, pamoja na Mhe. Waziri kwa majibu hayo. Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujaendelea tulipokatikiwa na umeme, Mhe. Naibu Waziri wa Bishara, Viwanda na Masoko alikuwa anajaribu kujibu swali la nyongeza kuhusu chakula cha akiba na ilikuwa hakumaliza.

Sasa sikutaka arudi tena hapa, isipokuwa atowe majibu ya maandishi kwa wajumbe kuhusu chakula cha akiba, kwa anasuala muhimu. Kwa hivyo, naomba watowe majibu ya maandishi kuhusu ni kiasi gani ya chakula cha akiba kinahitajika Zanzibar. Nawashukuru, tunaendelea.

HOJA ZA SERIKALI

Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mswada wa Sheria ya Kuweka Miundo, Uendeshaji na Usimamizi wa Utumishi wa Umma Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na hayo

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha asubuhi ya leo kuja mbele ya Baraza lako tukufu na kuwasilisha hoja ilioko mbele yetu.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba sasa Baraza lako tukufu likae kama kamati ili kujadili Mswada wa Sheria ya Kuweka Miundo, Uendeshaji na Usimamizi wa Utumishi wa Umma Zanzibar na Mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kuwasilisha mswada huu muhimu kwa maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Spika, naomba vile vile kuwapongeza na kuwashukuru sana wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi, chini ya Mwenyekiti wao Mhe. Ali Abdalla Ali, Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini kwa mchango wao na msaada mkubwa wa mashirikiano katika kuupitia kwenye hatua ya awali kwenye Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, mchango wa marekebisho yaliyofanywa na kamati kwa niaba ya Baraza la Wawakilishi. Wizara yangu imeyapokea na itayathamini sana katika kuhakikisha kuwa sheria hii baada ya kupitishwa rasmi na Baraza, inatekelezeka bila mgongano na sheria nyengine.

Madhumuni ya mswada huu ni kupendekeza kutungwa kwa sheria ya utumishi wa umma ya mwaka 2011, kwa lengo la kuweka utaratibu bora wa usimamizi wa utumishi wa umma ili kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Mhe. Spika, mswada pia umelenga kutekeleza ahadi za Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wa Awamu ya Saba Dk. Ali Mohammed Shein, katika mikutano yake mbali mbali ya kampengi ambayo aliahidi kuweka mazingira bora ya utumishi wa umma na kunyanyua maslahi ya wafanyakazi.

Mhe. Spika, katika utafiti uliofanyika juu ya mfumo na hali ya utumishi wa umma hapa Zanzibar, matokeo yalionesha mapungufu mengi na zikahitajika hatua za haraka za kufanya mageuzi makubwa ya utumishi wa umma, ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa mradi maalum kwa ajili ya kuratibu mageuzi hayo.

Hatua za awali za mageuzi ilikuwa kuandaa sera ya utumishi wa umma, ambayo imeshakamilika na kuidhiniswa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hatua iliyofuatia ni kuandaa mswada wa sheria ili kuweka msukumo wa kisheria katika kusimamia matakwa na maelekezo ya sera hiyo ya utumishi wa umma.

Mhe. Spika, mswada huu umeshapitiwa na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza lako tukufu na kufanywa marekebisho mbali mbali kwa mujibu wa taratibu za miswada kabla ya kujadiliwa na Baraza zima.

Aidha, tuliandaa semina kwa ajili ya Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Maoni na michango mbali mbali imezingatiwa katika chapisho jipya.

Mhe. Spika, tuliona ni vyema kuuchapa upya mswada ili uwe rahisi kwa wajumbe ili wauone unavyosomeka baada ya marekebisho ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

Madhumuni ya mswada

Mhe. Spika, madhumuni ya mswada ni kuweka sheria itakayosimamia utumishi wa umma Zanzibar, pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo ambayo ni ya msingi. Hatua hii pia itaondoa migongano ya majukumu kati ya kada moja na nyengine. Kuweka uwiano kati ya watumishi wanaolingana katika sifa za elimu na kusaidia kupanga maendeleo ya watumishi wa umma.

Mhe. Spika, kuna mabadiliko kadhaa ya msingi ambayo yanapendekezwa katika rasimu hii, kwamba rasimu ya sheria imeweka mipaka ya maamuzi kwenye tume za utumishi serikalini, idara maalum, mahakama na Baraza la Wawakilishi. Aidha, imebainisha majukumu ya Kamisheni ya Utumishi wa Umma na kuweka uhusiano wake na tume nyengine za Utumishi wa Umma.

Mhe. Spika, kamisheni itakuwa ni chombo cha juu cha maamuzi juu ya watumishi wa umma na tume zitakuwa na jukumu la kupeleka mapendekezo ya muundo ya watumishi, ajira, maslahi au mishahara. Kupandishwa madaraja na malalamiko yaani *appeal*, ya wafanyakazi walio chini ya tume zao. Uteuzi wa wenyeviti wa Tume ya Utumishi Serikalini na ile ya idara maalum, sasa utafanywa na mawaziri husika wakati uteuzi wa Mwenyekiti wa Tume ya Mahakama na ile ya Baraza la Wawakilishi utafanywa na Mhe. Jaji Mkuu na Mhe. Spika wa Baraza la Wawakilishi, kama viongozi wakuu wa vyombo hivyo.

Mswada umempa nguvu Katibu Mkuu Kiongozi ambaye pia ni Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Kiongozi wa Utumishi wa Umma. Aidha, umetambua rasmi Kamati ya Makatibu Wakuu kuwa chombo cha kitaalamu cha kulishauri Baraza la Mapinduzi na Mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Muundo wa Mswada wa Sheria ya Utumishi wa Umma

Mhe. Spika, mswada huu umegawika katika sehemu 11 na una vifungu 105 na majadweli 4.

Sehemu ya kwanza inaeleza kuhusu jina fupi la sheria, kuanza kutumika na tafsiri ya maneno muhimu kama yalivyotumika ndani ya sheria hii.

Sehemu ya pili inafafanua kuhusu misingi mikuu ya maadili ya utumishi wa umma na misingi mikuu inayoongoza utumishi wa umma na jinsi ya usimamizi

wa utekelezaji utakavyofanyika. Katika sehemu hii pia inaeleza uhusiano kati ya utumishi wa umma na uongozi wa kisiasa.

Sehemu ya tatu inachambua kuhusu upana wa utumishi wa umma yaani *scope*, katika eneo hili linazungumza.

1. Majukumu ya uwezo wa Rais, majukumu ya waziri, uteuzi wa Katibu wa Baraza la Mapinduzi na majukumu yake, Kamisheni ya Utumishi, Kamati ya Makatibu Wakuu kama chombo kikuu cha ushauri wa kitaalamu.

2. Uwezo na wajibu wa mawaziri katika wizara, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Idara, mashirika na wakala mbali mbali wa serikali.

Sehemu ya Nne inafafanua uundwaji wa taasisi mbali mbali za serikali, ikiwa ni pamoja na wizara, idara, wakala wa utumishi wa umma.

Sehemu ya tano imeweka utaratibu wa usimamizi wa rasilimali watu, ikiwemo miundo ya utumishi pamoja na mipango ya rasilimali watu. Masharti ya kujiunga na Utumishi wa Umma, utaratibu wa kupandisha vyeo.

Sehemu ya sita inaweka viwango vya ajira, yaani *label standard* na uhusiano kazini.

Sehemu ya saba imeweka utaratibu wa muundo, taratibu na mamlaka ya usimamizi ya nidhamu kwa watumishi wa umma. Katika sehemu hii mswada umetoa uwezo kwa mamlaka mbali mbali kusimamia nidhamu kazini.

Sehemu ya nane inazungumzia taratibu za malipo katika utumishi wa umma.

Sehemu ya tisa inatoa muongozo kuhusu usimamizi wa mfumo wa hahari na uwekaji wa kumbukumbu.

Sehemu ya kumi inazungumzia uwajibikaji na inatoa uwezo kwa Katibu Mkuu Kiongozi kusimamia uwajibikaji na kutoa miongozo mbali mbali.

Sehemu ya kumi na moja inahusu mambo mengineyo, ikiwa ni pamoja na utaratibu wa kushughulikia watu wenye ulemavu, uwiano wa kijinsia katika utumishi wa umma, walioathirika na ugonjwa wa Ukimwi. Pia kutoa fursa kwa waziri kutunga kanuni, kufutwa kwa baadhi ya vifungu vya sheria ikiwa ni pamoja na sheria ya Tume ya Utumishi wa Mahakama na Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi, ili viendane na sheria hii.

Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe, nategemea kwamba mswada huu mmepata muda wa kuupitia na viambatanisho vyake, nategemea kwamba mtaujadili na kuuchangia ipasavyo.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja *(Makofi).*

HOTUBA YA MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA KUHUSU MSWADA WA SHERIA YA KUWEKA MIUNDO, UENDESHAJI NA USIMAMIZI WA UTUMISHI WA UMMA ZANZIBAR

UTANGULIZI

Mhe. Ali Abdalla Ali: (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hotuba ya maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuweka Miundo, Uendeshaji na Usimamizi wa Utumishi wa Umma Zanzibar.

Awali ya yote naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Azza wa Jala kwa kunipa taufiki ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu nikiwa na afya njema ili niwasilishe rasmi mchango wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na pia kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mfenesini kuhusu, Mswada wa Sheria ya Kuweka Miundo, Uendeshaji na Usimamizi wa Utumishi wa Umma Zanzibar

Mhe. Spika, nitakuwa mtovu wa shukuruni ikiwa sitakushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya mwanzo kabisa baada ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Spika, wakati wa kupitia na kuchambua Mswada huo katika Kamati, nathubutu kusema kuwa Kamati yetu ilipata mashirikiano ya kutosha kukamilisha majukumu kutoka kwa Watendaji wa Wizara hii. Hivyo, Kamati yetu inawashukuru wote hao kwa pamoja kwa mashirikiano mazuri waliyotupa wakati wote wa kujadili.

Mhe. Spika, itakuwa ni jambo lisilokubalika kama sitatoa pongezi maalum kwa Katibu wa Baraza la Wawakilishi Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim pamoja na Mshauri wa Sheria - Baraza la Wawakilishi Ndugu Yahya Khamis Hamad kwa michango yao madhubuti waliyoitoa wakati kamati yetu ilipopitia na kuuchambua Mswada huu.

Mhe. Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ina Wajumbe 10 ambao walihusika kikamilifu katika kuupitia Mswada ulio mbele yetu, naomba niwatambue Wajumbe hao ni kama wafuatao.

1.	Mimi mwenyewe, Mhe. Ali Abdalla Ali	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Panya Ali Abdalla	-	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Ismail Jussa Ladhu	-	Mjumbe
4.	Mhe. Mussa Ali Hassan	-	Mjumbe
5.	Mhe. Mussa Khamis Silima	-	Mjumbe
6.	Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	-	Mjumbe
7.	Mhe. Suleiman Hemed Khamis	-	Mjumbe
8.	Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Mjumbe
9.	Ndg. Nasra Awadh Salmin	-	Katibu
10.	Ndg. Abubakar Mahmoud Iddi	-	Katibu

Mhe. Spika, kabla ya kutoa maoni ya Kamati naomba niishauri serikali kwamba, endapo itaandaa mswada wowote, ambao hatimae itakuwa ni sheria ya nchi ni vyema kushirikisha wadau mbali mbali ili kuepusha malalamiko yasiyokuwa ya lazima.

Mhe. Spika, baada ya pongezi na ushauri huo napenda sasa niende moja kwa moja kwenye mswada. Mhe. Spika, Mswada wa Sheria ya Kuweka Miundo, Uendeshaji na Usimamizi wa Utumishi wa Umma Zanzibar umetungwa kwa lengo la kuwa na sheria itakayosimamia Utumishi wa Umma – Zanzibar. Kama tunavyofahamu kwamba suala la Utumishi wa Umma ni suala muhimu sana na halina budi kuratibiwa na kuwekewa Sheria madhubuti yenye kuwajenga Watumishi wa Umma katika kutekeleza wajibu wao kwa moyo na uadilifu mkubwa. Ni matarajio ya Watumishi wa Umma kuwa Sheria hii itakuwa ni chachu ya maendeleo na ustawi wa Watumishi wa Umma ikiwa itatekezwa ipasavyo.

Mhe. Spika, pamoja na mambo mengine, Kamati yetu inaipongeza Serikali kwa kuweka ndani ya Mswada huu adhabu mbali mbali za kinidhamu kwa Watumishi wa Umma zinazolingana na uzito wa makosa yenyewe. Hatua hii inaonesha ni jinsi gani nchi yetu inafuata misingi ya Utawala Bora, kwani hakuna kosa linaloonesha adhabu ya moja kwa moja ya kumuachisha kazi Mtumishi wa Umma bila ya uchunguzi au onyo kutolewa.

Mhe. Spika, mswada huu pia, katika Sehemu ya Sita umeweka “Viwango vya Kazi na Mahusiano Kazini”. Tunaunga mkono Sehemu hii, kwani imeonesha yale mambo ambayo Mtumishi wa Umma anahitajika kuyapata kama Shirika la Kazi Duniani “*International Labour Organisation - ILO”* linavyoagiza.

Mhe. Spika**,** tulipendekeza kufanyiwa marekebisho baadhi ya maneno yaliyotokana na makosa ya kiuchapaji. Baadhi ya maneno hayo ni; katika ukurasa wa 125 kifungu cha 26(3)(b) mstari wa pili kutoka juu neno "kipinci" Kamati ilipendekeza lisomeke "kipindi", aidha, kifungu cha 29 mstari wa kwanza kutoka chini neno la kwanza "itavyoone" ilipendekezwa lisomeke "itakavyoona". Pia, katika ukurasa wa 126, kifungu cha 31(1) mstari wa tatu kutoka juu neno la nne kutoka mwisho "yaliyguswa" Kamati ilipendekeza lisomeke "yaliyoguswa". Mhe. Spika, marekebisho mengine ya maneno kama haya yanapatikana kwenye waraka wetu wa mapendekezo ya marekebisho.

Mhe. Spika, Kamati yetu ilibaini kuwa baadhi ya maelezo ya Vifungu vya Mswada wa Kiswahili hayaendani na maelezo ya Mswada wa Kiingereza. Baadhi ya maneno hayo ni; katika ukurasa wa 111 wa Mswada wa Kiswahili maneno "kinyume na taratibu" Kamati ilipendekeza yasomeke "tabia mbaya". Hii ni kutokana na kuwa neno lililotumiwa kwenye Mswada wa Kiingereza "*misconduct*". Aidha, neno "biashara" Kamati ilipendekeza lisomeke "fani", kwa kuwa neno "*trade*" lililotumika kwenye Mswada wa Kiingereza halikukusudiwa hivyo. Mhe. Spika, marekebisho mengine ya maneno kama haya yanapatikana kwenye waraka wetu wa mapendekezo ya marekebisho.

Mhe. Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala pia, imegundua kuwa baadhi ya Vifungu kwenye Mswada husika vinakwenda kinyume na Katiba ya Zanzibar ya 1984, jambo ambalo halikubaliki kisheria. Kwani kama tujuavyo kuwa Katiba ya Nchi ndio Sheria Mama, hivyo Sheria au kifungu chochote cha Sheria kinachotungwa kinyume na matakwa ya Katiba kinakuwa ni batili *"null and void"*. Mhe. Spika, baadhi ya vifungu hivyo ni; Kifungu cha 32 kinachoelezea "Bodi za Utumishi". Mhe. Spika, kifungu hiki kipo kinyume na Katiba ya Zanzibar. Hii ni kutokana kuwa Kifungu cha 77(2) cha Katiba kinaitambua Tume ya Utumishi wa Baraza la Wawakilishi, Kifungu cha 102 cha Katiba kinaitambua Tume ya Utumishi ya Mahkama, Kifungu cha 122 kinatambua uanzishwaji wa Tume ya Utumishi ya Idara Maalum na Kifungu cha 117 kinaanzisha Tume ya Utumishi ya Serikali. Hivyo, Mswada huu kwa kuzingatia Tume hizo kuwa Bodi ni kinyume na Katiba yetu. Kwa mnasaba huo, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ilipendekeza zijulikane kwa jina la "Tume" na sio "Bodi" kama ilivyoelezwa kwenye Mswada husika.

Mhe. Spika, Kamati yetu ilipendekeza baadhi ya Vifungu viandikwe upya ili viendane na matakwa ya Katiba ya Zanzibar. Kwa mfano; Kifungu cha 4 kinachozungumzia "Misingi Mikuu ya Utumishi wa Umma Zanzibar", ambapo Kijifungu cha (1)(vi) kinawawajibisha Watumishi wa Umma kutumikia Serikali iliyopo madarakani, jambo ambalo ni kinyume na Katiba. Hapa tunamaanisha kuwa kwa mujibu wa Kifungu cha 5A cha Katiba ambacho

kimeweka mfumo wa mgawanyo wa madaraka kati mamlaka tatu na kuzuia mamlaka mojakuingilia mamlaka nyengine. Hivyo, Mtumishi wa Baraza la Wawakilishi ambae Taasisi aliyopo katika mamlaka ya Kutunga Sheria na Kusimamia Utekelezaji hawajibiki kwa serikali na wala kwa Mahkama, na Mtumishi wa Mahkama hawajibiki kwa Serikali na wala Baraza la Wawakilishi. Hivyo, Kamati ilipendekeza Kijifungu hicho kisomeke "wajibu wa kuitumikia Mamlaka ya Nchi" badala ya "wajibu wa kuitumikia Serikali iliopo madarakani".

Mhe. Spika, Kifungu cha 6 kinachohusiana na "Uhusiano na Utumishi wa Kisiasa" tulipendekeza pia, kiandikwe upya kutokana na Mswada wa Sheria uliopo mbele yetu unahusiana na Masuala ya Utumishi wa Umma. Hivyo, haitokuwa busara kuzungumzia masuala ya kisiasa ndani yake kwa kuwa masuala haya ya kisiasa si sehemu ya Utumishi wa Umma. Mhe. Spika, kauli yangu hii inathibitishwa na Kifungu cha 134 cha Katiba ya Zanzibar chenye tafsiri ya neno "Utumishi wa Umma" ambacho kimeelezea wazi kuwa Utumishi wa Umma unajumuisha Utumishi wa Kisiasa.

Mhe. Spika, sambamba na hayo kamati yetu imependekeza kufutwa baadhi ya vifungu kutokana na sababu mbali mbali. Kwa mfano, kifungu cha 11 (6) kinachozungumzia kuondoshwa Madarakani Jaji wa Mahakama Kuu na endapo ataondoshwa madarakani, basi atachukuliwa kuwa amestaafu.

Kamati imependekeza kifungu hiki kifutwe, kwa sababu kinatoa mwanya kwa majaji kuitumia fursa hiyo kufanya lolote walitakalo, kwani watathibitishwa kuwa kosa au makosa hayana *style* yoyote watakayopoteza.

Aidha kamati imependekeza hilo kutokana kwa kuwa kifungu cha 37 (8) cha Katiba kinasitisha stahili za rais iliwa atathibitika kufanya kosa. Hivyo, kwa busara na watendaji hawa watasitishwa stahili hizo pindi watakapoondoshewa katika madaraka ya ujaji.

Vile vile napendekeza pia kufutwa kwa baadhi ya vifungu kutokana kuwa maelezo yake yanareje. Kwa mfano, kifungu cha 37 (2) kamati imependekeza kifutwe kwa kuwa maelezo yake hayatofautiani na maelezo ya kifungu cha 39 (3).

Mhe. Spika, kwa kuwa serikali imeanzisha Wizara inayohusika na Utumishi wa Umma, kamati yetu imehisi ni busara Katibu Mkuu Kiongozi kupunguziwa madaraka ambayo yanaweza kutekelezwa moja kwa moja na waziri.

Kwa hivyo, baadhi ya vifungu hivyo ni kifungu cha 11 (2) ambapo kamati yetu imependekezwa kuwekwa Waziri badala ya Katibu Mkuu Kiongozi. Pia

kifungu cha 17 kamati imependekeza waziri kuwa miongoni mwa Wajumbe wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma badala ya Katibu Mkuu Kiongozi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa muhtasari hayo ndio maoni ya Kamati yetu ya Katiba, Sheria na Utawala. Pamoja na hayo, nawaomba Wajumbe wa Kamati hii kutoa maoni yao katika maeneo muhimu ambayo mimi sikuyataja.

Sasa napenda niwashukuru tena Wajumbe wa Baraza lako tukufu Mhe. Spika, kwa kunisikiliza kwa makini, pia nikushukuru wewe mwenyewe kwa kuniruhusu kuwasilisha maoni ya kamati pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Mfenesini.

Mwisho kabisa Mhe. Spika, napenda kutamka bayana kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala pamoja na wananchi wa Jimbo la Mfenesini kwamba tunaunga mkono hoja ya Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Spika, wanaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu wauchangie na hatimaye kupitisha mswada huu muhimu kwa maslahi ya wananchi wetu pamoja na nchi yetu kwa jumla.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Ali Abdalla Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala) tunakushukuru kwa kazi kubwa ya kamati ambayo mmeifanya na yote ilikuwa na madhumuni ya kufanya mswada huu uwe bora na tuweze kuujadili vizuri hapa Barazani. Sasa nadhani tuendelee na uchangiaji wa jumla nataka nianze na kumkaribisha Mhe. Salmin Awadh Salmin na baadaye Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza katika wachangiaji wa jumla. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana hapa leo kwa ajili ya kuchangia mswada huu muhimu sana ambao unahusu Watumishi wa Umma.

Pili nimpongeze Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kuanzisha Wizara mpya ya Utumishi na Utawala Bora kama alivyoahidi kwenye Mikutano yake ya Kampeni, kwamba katika serikali yake mwaka huu anategemea kuanzisha wizara itakayoshughulikia masuala ya utumishi na utawala bora.

Vile vile nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kuandaa mswada huu na leo upo katika Baraza letu tukufu.

Pia nitumie nafasi hii kuwapongeza sana Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kuweza kuupitia mswada kifungu kwa kifungu na hatimaye kufanya marekebisho makubwa. Mhe. Spika, kama unavyoona kwamba mswada wa awali ni tofauti kabisa na mswada huu ambao umetoka juzi. Kwa hivyo, wameweza kufanya marekebisho makubwa na kugundua zile kasoro ambazo zilikuwemo kwenye mswada ule uliotangulia. *(Makofi)*

Mhe. Spika, lengo la Mhe. Rais la kuanzisha wizara hii ni kuona kwamba Watumishi wa Umma wanakuwa na chombo chao ambacho kitaweza kusimamia masuala yao moja kwa moja na sio kama ilivyokuwa pale awali.

Lakini bado mswada huu wa sheria unaonekana umempa mamlaka makubwa Katibu Mkuu Kiongozi ambaye kwa mujibu wa taratibu sio mtumishi au kiongozi aliyekuwepo kwenye wizara hii. Kwa kweli hali hii inaonesha kwamba bado mswada huu unahitaji kuangaliwa upya kwani una mapungufu, yaani bado umempa mamlaka makubwa Katibu Mkuu Kiongozi kama ilivyokuwa pale mwanzo.

Mhe. Spika, unaposema Utumishi wa Umma, maana yake ni utumishi wa watu na watu kwa maana ni wananchi. Sasa tunapojadili Watumishi wa Umma, maana yake tunajadili masuala yanayohusu wananchi wetu, wananchi ambao kwa mujibu wa Katiba mamlaka ya kuendesha nchi yako mikononi mwao, ambapo nguvu na uwezo wote wa serikali kufuatana na Katiba yetu utatokana na wananchi wenyewe. Kwa misingi hiyo Mhe. Spika, tunatakiwa tuwe makini sana katika kujadili mambo haya yanayohusu mswada huu.

Vile vile mswada huu wa sheria unaonekana una mapungufu wakati nilipoupitia nimeyaona. Kwanza inavyoonekana hakujawa na Sera ya Moja kwa Moja ya Utumishi na kama sera ipo, basi sera hiyo bado haijawasilishwa hapa Barazani.

Kwa maana hiyo, pengine sheria iliyotungwa imetofautiana na sera, pamoja na kwamba kwa mujibu wa Katiba maamuzi ya sera yatapitishwa na serikali, lakini nadhani ni vyema Mhe. Waziri kabla ya kutunga sheria ilikuwa ni vyema iwasilishwe sera katika chombo hiki, ili kuona kwamba sheria inayotungwa inaoana na matakwa ya sera yenyewe. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mapungufu mengine yanayoonekana ni baadhi ya vifungu vya mswada huu wa sheria vimegongana na Sheria ya Kazi. Kwa mfano, kifungu cha 79 cha mswada kinazungumzia viwango vya kazi, ambapo kifungu cha 79 (3) kinazungumzia juu ya Kanuni za Utumishi wa Umma katika utekelezaji wa viwango vya kazi. Lakini katika Sheria ya Kazi viwango kama hivyo vimo

katika Sheria ya Ajira kifungu Nam. 7. Mfano mwengine kifungu cha 84 cha mswada kinagongana na kifungu cha 109 cha Sheria ya Ajira kuhusu kusimamishwa kazi.

Kulingana na hali hiyo, inaonekana bado kuna migongano ya vifungu vile vilivyopitishwa katika Sheria ya Utumishi wa Umma na ile Sheria ya Kazi. Pamoja na kwamba mswada kifungu cha 7 kimezungumzia waziri anayehusika na utumishi anaweza kuwasiliana na waziri anayeshughulikia masuala ya kazi katika utungaji wa kanuni.

Mhe. Spika, nadhani ni vyema tunapoanzisha sheria basi tusianzishe migongano katika hatua za awali. Kwa hivyo, ni vyema Mhe. Waziri akviangalia vifungu vya Sheria ya Ajira na vile vinavyohusiana na masuala ya utumishi, ili visijevikaleta migongano hapo baadaye.

Kasoro nyengine inaonekana kwamba katika mswada huu wa sheria kumekosekana baadhi ya tafsiri muhimu. Kwa mfano, unapozungumzia Wawakilishi wa Watumishi, neno hili linahitaji tafsiri katika mswada huu, unapozungumza Wawakilishi wa Watumishi unakusudia nini. Kwa hivyo, neno hili linahitaji ufafanuzi au tafsiri katika mswada wa sheria.

Vile vile suala la maslahi ya umma limekosa tafsiri katika mswada huu, unapozungumzia maslahi ya umma unakusudia nini. Pia unapozungumzia majadiliano yapamoja nalo linahitaji tafsiri katika mswada huu. Mhe. Spika, unapozungumzia Vyama vya Wafanyakazi pia napo panahitaji tafsiri.

Kutokana na hali hiyo, nafikiri kuna kasoro ya tafsiri kwa baadhi ya maneno muhimu ambayo yangehitaji kupata tafsiri kwenye mswada wa sheria huu.

Sehemu ya nne Mhe. Spika ambayo tunahisi inamapungufu katika mswada huu wa sheria ni namna walivyoshirikishwa wadau kwa maana ya Vyama vya Wafanyakazi. Kwa kweli inaonekana kwamba wakati wa uandaaji wa mswada huu hakuna mashirikiano ya moja kwa moja yaliyotolewa, pamoja na kwamba wenzetu katika hatua za awali walitueleza kuwa wamewashirikisha wadau.

Lakini inavyoonekana, uchunguzi wetu na kwa mujibu wa semina ambayo imefanywa na Wizara ya Nchi (AR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora, inaonekana wadau wakubwa watumizi wa sheria hii hawakushirikishwa moja kwa moja. Hayo ni mapungufu makubwa ambayo yanaweza kuleta matatizo katika utekelezaji wa sheria hii.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 6 cha mswada ambacho kinazungumzia uhusiano wa utumishi wa kisiasa, kifungu cha 6 (2) (a) katika sheria hii

inalazimisha kutungwa kwa sheria nyengine. Sasa ikiwa serikali inaona ipo haja ya kutunga sheria nyengine badala ya ile, nadhani sio vyema sheria hii iilazimishe kutunga sheria nyengine.

Kwa hivyo, ni pale serikali inapoona kuna haja ya kutunga sheria, basi itatunga sheria, kwa sababu kinacholazimisha sheria kutungwa ni Katiba ya nchi. Kwa mfano, pale itakaposema kwamba Katiba hii katika utekelezaji wake ni lazima ipitishwe sheria katika utekelezaji wa jambo hili. Nafikiri kifungu hiki cha 6 kinaonekana kinamapungufu.

Mhe. Spika, kifungu hiki cha 6 kinazungumzia kuhusu uhusiano na utumishi wa kisiasa. Kwa kweli kifungu hiki ninapendekeza kifutwe kwa sababu hakuna uhusiano kati ya Utumishi wa Umma na Utumishi wa Kisiasa na hata ukiangalia Katiba yetu kifungu cha 134 ambacho kimetoa tafsiri juu ya Utumushi wa Umma. Kwa maana hiyo, kifungu hiki kiondoshwe kabisa kisiwemo katika mswada huu wa sheria, kwa sababu hakuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya Utumishi wa Umma na Utumishi wa Kisiasa. *(Makofi)*

Vile vile kifungu cha 21 kinazungumzia kuhusu ripoti ya mwaka. Mhe. Spika, kwa nini Kamishna awasilishe Ripoti ya Fedha kwa Katibu Mkuu Kiongozi, wakati kifungu cha 31 (2) kinazungumzia kazi ya Waziri wa Utumishi wa Umma, ambapo kifungu cha 31 (2) (f) kinasema waziri atasimamia utendaji wa kazi za Kamisheni. Hali hii inadhihirisha katika maelezo yangu ya awali kwamba bado anaonekana Katibu Mkuu Kiongozi amepewa nafasi kubwa juu ya Watumishi wa Umma, ambapo waziri anayehusika na wizara hii, yaani kuna muingiliano katika usimamizi wa wizara hii.

Kwa hivyo, naomba Mhe. Spika vifungu kama hivi ambavyo vinaleta kutokuonesha utekelezaji mzuri katika mswada huu wa sheria, basi vifanywe marekebisho. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho atueleze namna alivyofanya marekebisho hayo.

Mhe. Spika, kifungu cha 68 kinazungumzia kuhusu suala la Mkataba wa Ajira. Kifungu hiki ambacho ni kifungu cha 68 (1) (c) (iii) kinazungumzia kustaafishwa kwa maslahi ya umma juu ya watumishi wa umma. Nataka kuuliza Mhe. Waziri nini maana ya kustaafishwa kwa maslahi ya umma, sasa unapozungumzia mtumishi amestaafishwa kwa maslahi ya umma nini maana yake.

Lakini mtumishi wa umma anapostaafishwa kwa maslahi ya umma inapotokea jambo gani. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika atakapokuja kufanya majumuisho atupe ufafanuzi. Vile vile mtumishi anapostaafishwa kwa maslahi ya umma anapata haki zipi kisheria.

Kifungu cha 62 cha mswada kinazungumzia kuhusu muundo wa utumishi na mpangilio wa kutangulia kazini. Mhe. Spika, kifungu cha 62 (2) nane viongozi wa kisiasa liondoshwe katika mswada huu wa sheria, kwa sababu viongozi wa kisiasa sio viongozi wa umma.

Mhe. Spika, kifungu cha 79 kinazungumzia viwango vya kazi, ambapo kifungu cha 79 (3) (H mpaka L) kinahusu likizo mbali mbali. Kwa kweli wapo watumishi wa umma ambao wengine zaidi ya miaka kumi hawajenda likizo na wala watumishi hawa hawajawahi kuomba na kukataliwa. Kwa hivyo, Mhe. Spika nadhani ni vyema Mhe. Waziri kueleza juu ya watumishi wa aina hiyo. Kutokana na hali hiyo, inaonekana kuna watumishi ambao wanafanyakazi na wala hawataki kwenda likizo tena hawaombi.

Sasa kwenye mswada huu wa sheria haujawazungumza, labda anakusudia kuweka kwenye kanuni, lakini kifungu cha 79 (3) (H mpaka L) kimezungumzia masuala kama haya na kuacha maeneo ambayo kuna watumishi ambao hawataki kwenda likizo na sijui kwa sababu gani. Kwa maana hiyo, kuna haja ya kuwa na maelekezo juu ya watumishi wa aina hii ambao wanaonekana wapo na wala hawataki kwenda likizo kutokana na ubinafsi wao.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo nisichukue muda wako mwingi. Kwa hiyo, mimi pamoja na wananchi wa Jimbo la Magomeni tunaunga mkono mswada huu wa sheria pale ambapo Mhe. Waziri atafanya marekebisho juu ya vifungu mbali mbali ambavyo tumevizungumza na hatimaye mswada huu utakuwa una manufaa kwa watumishi pamoja na wananchi wetu kwa jumla. *(Makofi)*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa hii kuwa mtu wa pili na aghalabu huwa mtu wa kwanza, lakini ndio mageuzi yalivyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwanza namshukuru sana Mhe. Waziri kwa kuona mapungufu ambapo tumeletewa karibu kitabu kizima chenye asilimia 90 kutokana na marekebisho yaliyofanywa na kamati.

Vile vile nimshukuru Mhe. Ali Abdalla Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala) mwenyewe, wajumbe wa kamati pamoja na wanasheria kwa kuangalia kwa upeo wa macho na kuona kuna mambo ambayo yanaweza kuingiliana na kuleta athari katika nchi yetu na kuweza kurekebishwa na Mhe. Waziri kuridhia. *(Makofi)*

Mhe. Spika, faraja kubwa juzi tulipokuwa kwenye semina, kwa sababu ilinijia hamu katika hii ile *paper* ya Dhana ya Utawala Bora, ambapo tuliambiwa kuna

misingi ya utawala bora minane, katika kifungu cha 8 kwenye ukurasa wa 3 katika *document* hiyo tuliyopewa, inasema kuwa ushirikishwaji ni suala muhimu sana.

Kwa maana hiyo, ilikuwa kuna ulazima wa kushirikishwa wadau kwa ajili ya kuleta mafanikio mazuri katika mswada huu wa sheria ambao tunataka kuupitisha pengine kesho au kesho kutwa kwa mujibu wa utaratibu Mhe. Spika utaangalia jinsi ya wachangiaji watakavyokuwa wengi.

Mhe. Spika, kwa huzuni zaidi niseme kutokushirikishwa Vyama vya Wafanyakazi ni moja katika ishara ambayo imeonesha mapungufu makubwa na kuna hatari mbele. Kwa mfano, wenzangu walisema hapa kama vile Mhe. Ali Abdalla Ali ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala pamoja na Mhe. Salmin Awadh Salmin, lakini mimi nataka kuonesha jinsi gani hatari inaweza kutufika kutokuwashirikisha Vyama vya Wafanyakazi.

Kwa kweli hivi sasa kuna Azimio Maalum 144 *International Labour Organization (ILO)*. Kwa hivyo, hii ni tatizo kwa sababu tumejikubalisha kuwa mswada wa aina yoyote utakaohusiana na watumishi ni lazima hawa washirikishwe, lakini azimio hilo tumelipuuza. Kwa maana hiyo, tumeonesha jinsi ule udhaifu wetu na hii ni hatari kubwa sana.

Mhe. Spika, nadhani si vibaya Mhe. Waziri akaa na watu wa Vyama vya Wafanyakazi kwa ajili ya kuzungumza nao kwa lugha nzuri kwa ajili ya kujiridhisha nafasi zao. Kwa kweli hawa wakisema waandike barua na kupeleka huko duniani Mhe. Spika, nafikiri itakuwa ni hatari kubwa, yaani hata sisi pengine tusishirikishwe vizuri kwa wenzetu.

Hatari zaidi Mhe Waziri wetu wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika pamoja na Katibu wake, kwa mfano kuna utaratibu kule ukionekana kama tayari umekiuka azimio lao basi kuna hatari ya kuzomewa. Sasa nafikiri tuione hii hatari ambayo inayoweza kutufika.

Mhe. Spika, ndio maana mara nyingi sana tunapoamua masaula haya ya marekebisho basi tuangalie na athari za wale wafadhili wetu, kwa sababu tusipoangalia ndio athari hii inaweza kutufika kuhusiana na Azimio la 144.

Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika kukaa na hawa watu wa Vyama vya Wafanyakazi, kwamba binadamu kukosea ni nafasi yake ipo, lakini tukubali kwa sababu binadamu hakuna mkamilifu, ili kuweza kuridhia.

Vile vile niwashukuru sana watu wa Vyama vya Wafanyakazi kwa kweli hawakuwa na jazba, kwa sababu walikuwa na uwezo wa kufanya maandamano kama nchi nyengine na ingekuwa hatari kubwa, lakini hawa ni watu ambao tayari wamelelewa katika misingi ya kiujamaa, basi wameweza kuwa watulivu, yaani wametumia diplomasia katika kuleta masuala yao. Kwa kweli hata kamati kuweza kuridhia na Mhe. Ali Abdalla Ali Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala anatueleza vifungu mbali mbali walivyokubaliana kuweza kuvipitisha. Mhe. Spika, hawa watu wa Vyama vya Wafanyakazi wameshiriki kwa asilimia mia moja.

Nikiendelea na mchango wangu Mhe. Salmin Awadh Salmin alisema kweli kuna baadhi ya vifungu vinataja tafsiri, yaani pengine vinaweza kugongana na mambo ya sheria.

Lakini mtazamo wangu ukurasa wa 8 kwenye kifungu cha 3 neno maslahi ya umma naomba nipewe tafsiri yake kisheria. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika atakapokuja kufanya majumuisho anisaidie tafsiri ya neno maslahi ya umma kwa mujibu wa sheria.

Vile vile ukurasa wa 15 kifungu kinachozungumzia masuala ya kumshauri Rais juu ya mishahara ya umma. Mhe. Spika, kifungu hiki naomba kiondoshwe kabisa na kuwe na Bodi ya Mishahara ambayo ndio itayaoweza kumshauri Mhe. Rais.

Kwa mtazamo huo kwa kuwa bodi tayari imo kwenye sheria basi namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, atakapokuja kufanya majumuisho anisaidie zaidi, ili kuona ufanisi huo wa kuona bodi ndio ipewe mamlaka ya kumuona Mhe. Rais, ili kuweza kupanga na kumshauri kuhusu masuala ya maslahi.

Katika ukurasa wa 33 kifungu cha 3 pia kifungu hiki kinanipa utata kidogo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, akiangalie kifungu hiki kwa mujibu wa utaratibu wa sheria, ili Waheshimiwa pamoja na wadau waweze kukifahamu kifungu hiki na hasa maslahi yake kutokana na hiyo sheria. Kwa kweli kimeeleza pamoja na mikataba ya ajira na masharti, ajira ya ziada inaweza ikaingizwa katika utumishi wa umma kama hatua yoyote au wakati wa ajira na masharti hayo yatakuwa bila ya kujali sheria.

Nadhani hapa kidogo angetufahamisha Mhe. Waziri, kwani tayari kuna sheria ambazo zimeshatungwa, lakini yeye Mhe. Waziri amekusudia vipi kutaka kutuletea hapa, ili tuweze kukipitisha na kukiunga mkono. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, atusaidie nini hasa dhamira yake juu ya kifungu hiki kwenye mswada huu.

Nikiendelea katika ukurasa wa 21 pia kifungu cha 93. Mhe. Spika, katika kifungu hiki namuomba Mhe. Waziri akiangalie vizuri naona kama kinanipa mashaka kidogo. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho, basi kifungu hiki atafafanulie vizuri kwa mujibu wa utaratibu wa sheria lengo la kifungu hiki kwa ajili ya kukiweka sawa, ili kisipingane kama tunavyosema hapa Katiba pamoja na masuala ya mswada kuingiliana na kuleta mgongano wa hapa na pale.

Mhe. Spika, kwa kumalizia kama nilivyosema leo sitokuwa na mchango mkubwa, kwa sababu mambo mengi sana ambayo yalikuwa yamenigusa ndani ya moyo tayari yamepatiwa ufumbuzi kwa kumalizia ukurasa wa 60 kwenye kifungu cha 54.

Nadhani kwanza nianze kwenye kushiriki kwenye migomo au kukataa. Mhe. Spika, mgomo wenyewe tuseme, nafikiri ni vyema akaongeza neno mgomo ambao sio halali, badala ya hili neno ambalo lipo hapa namuomba Mhe. Waziri aweke wazi kabisa mgomo ambao sio halali. *(Makofi)*

Tukiangalia kifungu cha 54 kinachozungumzia kuhusu uwezo wa hali ya juu, sasa hapa hii hali ya juu ni ipi. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, hili neno hali ya juu liondoshwe kabisa, yaani hiki kifungu kibakie, isipokuwa hili neno la hali ya juu huu msisitizo, basi ninamuomba Mhe. Waziri aitizame hii tafsiri yake iko vipi na kuweza kuiondoa.

Mhe. Spika, nampongeza sana Mhe. Waziri pamoja na Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala kwa kubaliana yale ambayo dhana yetu ilikuwa ni mapungufu ya mswada huu na kuweza kukubali kurekebisha na kutuletea kitabu hiki kizito sana mpaka mkono wote unaniuma.

Kwa hayo machache kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kitope ninaunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza angalau kuchangia chochote katika mswada huu muhimu. Kwa kweli mimi sitokuwa na mchango mkubwa.

Kwanza naomba nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuleta mswada huu muhimu katika kipindi hiki, kwa sababu nchi yetu kwa kipindi kirefu sana inakabiliwa na tatizo kubwa la watumishi wa umma. *(Makofi)*

Pili naomba niishukuru kwa dhati kabisa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Kwa kweli nikiri kwamba kamati hii imefanyakazi kubwa sana, kazi ambayo

kwa kiasi kikubwa imeturahisishia sisi wajumbe katika kuuchangia mswada huu. *(Makofi)*

Sasa baada ya shukurani naomba nitangulie kwa kusema, kwamba Mhe. Spika tunatakiwa katika kutunga sheria zetu tuzingatie sana Katiba ya nchi yetu, kwa sababu Katiba yetu ndio Sheria Mama. Kwa hivyo, chochote ambacho tutapaswa kukiandaa iwe ni sera, mipango ya serikali pamoja na sheria, basi tunapaswa kwanza tu-*revise* Katiba yetu, ili tuone mwelekeo wa mambo ambayo tunataka tufanye, lakini vile vile sheria zetu hizi zizingatie sera tunazozipitisha katika Baraza hili, lakini vile vile sheria zetu zizingatie zaidi mipango yetu ya maendeleo ikiwa ni pamoja na dira yetu ya maendeleo, mpango wetu wa kuondosha umasikini pamoja na mipango mingine.

Lakini zaidi nataka niseme kwamba sheria zetu zizingatie sana juu ya uimarishaji wa demokrasia na utawala boda katika nchi yetu, diama Zanzibar iwe ni yenye kwenda mbele sio yenye kurudi nyuma na ndivyo serikali zote zinavyofanya hakuna taifa linalorudi nyuma, mataifa yote hutaka kusonga mbele katika kuimarisha suala zima la demokrasia pamoja na suala la utawala bora.

Mhe. Spika, mimi naiomba serikali katika kutunga sera zetu tuzingatie mambo hayo ya msingi, sasa mchango wangu moja kwa moja uende kwenye tafsiri ya kifungu cha tatu neno mtumishi wa umma, kwa mujibu wa umma imeainishwa kwamba mtumishi wa umma kwa madhumuni ya sheria hii maana yake ni mtu anayeshika nafasi au kukaimu katika Afisi ya Utumishi wa umma, ni mtu anayeshika nafasi au kukaimu katika Afisi ya utumishi wa umma. Mimi nadhani neno hili halitoi tafsiri sahihi ya mtumishi wa umma, kwa sababu kama tutazingatia kwamba ni mtu tu anayeshika nafasi au kukaimu hawa wengine ambao wao hawana nafasi yoyote au hawakaimu wao tutawaita vipi.

Kwa hivyo mimi nadhani neno mtumishi wa umma litafsirike kwamba kwa madhumuni ya sheria hii maana yake ni mtu aliyeajiriwa katika Afisi ya Utumishi wa umma, tukifanya hivyo nafikiria litaleta tafsiri kwa mujibu wa sheria hii ilivyo.

Mhe. Spika, sasa naomba niende kwanye kifungu cha sita moja kinasema kwamba utumishi wa umma utakuwa na uhusiano na utumishi wa kisiasa katika kanuni na maadili na sera za malipo, sasa mimi nadhani hili sio sahihi kuunganisha utumishi wa umma pamoja na utumishi wa kisiasa, si sahihi kwa sababu ile ile niliyoitaja kwamba katiba yetu imeeleza kwa ufasaha katika kifungu cha 5(a) 1,2,3 kwamba nchi yetu itakuwa ni nchi yenye kufuata mgawanyiko wa mamlaka tatu. Na katika kifungu cha tatu kama sikosei

kimesema kwamba hakuna muhimili mmoja unaoweza kuingilia mhimili mwengine.

Sasa leo tutakapofika pahala sheria ikata kuunganisha vitu hivi baina ya watumishi wa uma na watumishi wa siasa tarsiri yake Mhe. Spika, ni kusema sasa tunajaribu kuleta mapinduzi katika kifungu hichi, hiyo ndio tafsiri. Kitu ambacho ni kinyume kabisa kabisa na katiba yetu, katika kifungu cha 118 kimesema wazi kwamba kutakuwa na tume ya utumishi, kutakuwa na Tume za zitakazokuwa na mamlaka ya kuajiri, kuthibtisha ajira, kusitisha au kuachisha ajira na kupendekeza serikalini mishahara pamoja na marupurupu.

Mhe. Spika, hivyo ndivyo katiba ilivyoelekeza kwamba kutakuwa na Tume za Utumishi ambazo zitakuwa na majukumu hayo, katika kifungu cha 77 katika katiba yetu kimeeleza wazi wazi kwamba kutakuwa na tume ya utumishi ya Baraza la Wawakilishi.

Kifungu cha 102 kimeeleza wazi wazi kwamba kutakuwa na Tume ya Utumishi ya Mahakama, kifungu cha 102 kimeeleza kwamba kutakuwa na tume ya utumishi ya Idara maalim kadhalika kifungu cha 117 kimeeleza kwamba kutakuwa na tume ya utumishi katika serikali.

Mhe. Spika, juzi ulivyotueleza kwenye semina kwamba umewatuma wataalam wako wa mambo ya sheria nilitaraji kwamba hili katika mswada huu uliyoyaandika upya hili hatutolikuta, lakini bahati mbaya kwamba hili linakuja tena katika mbele yetu. Mimi napendeleza Mhe. Spika, katika dhana ile ya utawala bora ni pamoja na kuheshimu katiba ambayo tunaapa kuilinda kwa hivyo nadhani ni vyema turudi katika viapo vyetu vya kuilipa katiba yetu.

Kwa msingi huo naomba kifungu nambari 6 katika kutekeleza dhana hiyo kuondoshwe ili tuiacha katiba iendelee kama ilivyo, kwa hivyo hilo napendekeza kwamba tuiache katiba iendelee kama ilivyo.

Kadhalika katika kifungu cha 7 kwa sababu katika kifungu hichi cha 6 tumeambiwa kwamba utumishi wa kiasa katika kanuni za maadili na sera za malipo tafsiri inayoelezea kanuni na maadili zimeelezewa katika kifungu cha saba, kwa hivyo pamoja na kwamba kifungu hichi kitakuwa kikivunja katiba lakini vilevile ni sawa na kusema kwamba hata sisi watumishi wa kisiasa tunatakiwa tufuate maadili yaliyomo kwenye kifungu cha 7. Ndio hii tukasema kwamba hii sheria wakati mwengine inakuwa na matatizo katika tafsiri yake maana yake tafsiri za maadili zinaonekana katika kifungu cha 7.

Mhe. Spika, kifungu cha 10 vile vile utumishi wa umma Zanzibar utaundwa na tumishi zifuatazo kifungu cha kumi vile vile kitakuwa hakina maana yoyote

kutokana na hii hoja niliyoisema kwanza, kwamba utumishi wa umma kwa mujibu wa katiba yetu utaendelea kuwa ni utumishi wa na tumishi nyengine zitaendelea kubakia kuwa tumishi nyengine. Sasa kusema kwamba utumishi wa umme Zanzibar utaundwa na tumishi zifuatazo hiyo inapingana na katiba yetu. Kwa hivyo kifungu cha 10 vile vile kitakuwa hakina maana yoyote.

Mhe. Spika, kifungu cha 13 (d) kutekeleza majukumu na kifungu cha 13(1) kinasema Rais anaweza kutangaza kwa tangazao rasmi litakalochapishwa katika agizo rasmi la serikali kuagizwa kutekeleza yote kati ya majukumu yafuatayo kwa Katibu Mkuu Kiongozi kamisheni, tumya ya utumishi, bodi ya wakurugenzi, Baraza la uongozi au na mawaziri kama atakavyofikiria inafaa. Na katika kifungu (d) imeelezwa kwamba kupitia katibu mkuu kiongozi Rais anaweza kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya wateule wa Rais walioteuliwa moja kwa moja na Rais au chini ya mamlaka iliyokasimiwa.

Mhe. Spika, mimi nadhani jukumu hili asipewe Katibu Mkuu Kiongozi, kuwa wateuliwa wa kisiasa hasa mawaziri kwa sababu naweza kujiuliza mimi kati ya Waziri na Katibu Mkuu Kiongozi nani mkubwa kati ya hawa wawili, kwa tafsiri hii inawezekana kwamba Rais haiwezekani kumtuma Katibu Mkuu Kiongozi kumchukulia hatua za kinidhamu Mhe, Haji Omar Kheir. Mimi nadhani kwa sababu Mhe. Haji ni muwakilishi tena ni Waziri aliyeteuliwa na Rais kama kuna hatua yoyote ya kinidhamu kama anataka kuchukuliwa basi nadhani Mhe. Rais amchukulie moja kwa moja kulikoni kupitia kwa Katibu Mkuu Kiongozi.

Mhe. Spika, kama nilivyosema awali kwamba mchango wangu hautokuwa mkubwa naomba niishie kwa kuunga mkono hoja, lakini naunga mkono hoja baada ya Mhe. Waziri atakapokiondosha kifungu cha sita. Ahsante sana *(Makofi)*

Mhe. Asaa Othman Hamad: Nakushukuru sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia nafasi hii kuweza kuchangia machache juu ya mswada huu muhimu sana kwa Zanzibar ya leo. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima wa afya na kuendelea na majukumu yatu tuliyopangiwa na wananchi.

Mhe. Spika, nitumie nafasi hii kwanza kwa kuunga mkono hoja. Mswada wa sheria ulioko mbele yetu madhumuni yake binafsi nimeridhika sana na nadhani sasa tunaelekea pahali ambapo tunastahiki kuelekea, kutokana na matatizo mengi ya utumishi kwenye taasisi zetu mbali mbali hapa Zanzibar, lakini sasa kwa sababu tunakwenda kuanza na misingi na tunapoweka msingi tunajenga uimara. Lakini la pili ni jinsi ya sisi wenyewe tulivyojitayarisha kuendeleza na kuona kwamba ile dhana iliyokusudiwa kwa wananchi wetu inapatikana.

Mhe. Spika, misingi mikuu iliyotajwa kifungu cha 4(1) kuansia A mpaka F ina umuhimu mkubwa, lakini nimepata na wasi wasi kwamba bado na sijui Mhe. Waziri atatuelezaje utekelezwaji wa haya.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nivitaje vichache tu pale kifungu cha 4(1) kujielekeza katika matokeo ya kazi, hizi tafsiri nitamuomba Mhe. Waziri atakapokuja atusaidie zinatukanganya kwa kiasi fulani. Lakini jengine kujielekeza kwa mpewa huduma, sasa hivi kuna matatizo tunayokabiliana nayo makubwa hasa kwenye taasisi ya Afya na hizi taasisi zinazotoa huduma, zaidi leo nitaelekea hapa kwenye afya.

Mhe. Spika, uwajibikaji umeshuka kwa kiasi kukubwa sana misingi hii kama itatekelezwa kama ilivyokusudiwa ni imani yangu kwamba hali inayowakuta wananchi wetu sasa hivi huenda sasa hivi tukapata ahuweni. Labda niseme kwenye namba mbili uvunjaji wa makusudi kuna neno la nidhamu hapa, na uvunjaji wowote kwa sababu ya dharau, matendo haya ndiyo yaliyoenea au yaliyozoeleka katika utendaji tulionao sasa, endapo sasa hali hii kwa wale watakaoyatenda watachukuliwa hatua za nidhamu huenda tukaanza mwendo mpya wa utumishi ndani ya nchi yetu hii.

Mhe. Spika, Mheshimiwa Waziri pia kwanye sheria ameyataja maadili makuu, utumishi wa umma utakaoongozwa na maadili hata yale yaliyorithiwa nakumbuka kwamba na kama tunavyokumbuka wote tumerithi maadili kutoka kwa wakoloni ambayo siyo yote kwamba ni mabaya, kwa upande wa utumishi kulikuwa na nidhamu ya hali ya juu, wale waliobahatika kusoma shule zile za wakati wa ukoloni tuliojaariliwa kuona angalau kwa muda mfupi sana ni vipe mgonjwa ama daktari hata nesi ama muuguzi alivyokuwa anamuhudumia mgonjwa aliyelazwa pale hospitali. Tukiyakumbuka yale au wazee wetu wanapokumbuka ya zamani na wanayoyakuta hivi sasa ndipo hiyo tofauti kubwa tunayoisema kwamba ipo na sheria hii ishaalla baada ya kupitishwa na wajumbe wako, ikapata baraka za Mhe. Rais huenda sasa tukabadilika.

Mhe. Spika, ni lazima tubadilike kwa kujenga heshima na kurudisha heshima ya nchi yetu, tubadilike kwamba sasa na sisi Zanzibar inaingia moja kwa moja na mkondo huu wa utandawazi ambao hatuna namna ya kukwepa kadiri tutakavyoweza na mazingira tuliyokuwa nayo ni lazima tubadilike

Mhe. Spika, kifungu cha 5(2) zaidi ya mabadiliko hayo utumishi utapaswa kufuata maadili ya kawaida ya utumishi wa umma yafuatayo yameandikwa humu.

Kwamba sasa hakutokuwa na ajira za kumwambia tu basi mwambie aje afisini, lakini anayestahiki apate ajira ile hapewi kwa sababu kuna upendeleo wa aina fulani , ama ananyimwa kwa donda ndugu lililotusibu muda mrefu tofauti za kisiasa. Nashikuru kwamba leo Mhe. Waziri ameona umuhimu wa kuileta hapa kwani hapa tumepoteza wataalam wengi wazuri kwa sababu tu wananyimwa ajira kwa tofauti hizi. Ishaalla Mwenyezi Mungu atujaalie tuondokane na hayo tena na sisi tungine pale ambapo ulimwengu uinatushangaa kwa nini Wazanzibari muda mfupi huu wamefika walipofika. Waheshimiwa wajumbe nawaomba kwa pamoja tuidumishe heshima hii ambayo viongozi wetu wametupatia.

Mhe. Spika, kuna uteuzi na upandishwaji vyeo anaingizwa mtu leo anamkuta afisa yupo pale ana uzoefu miaka kumi na tano na kuendelea lakini anaambiwa huyu ndiye bosi wake, haidhuru kamaliza chuo lakini katika masuala ya maofisi uzoefu una heshima maalum, kisingizio kisiwe kwa vyeti alivyokuwa navyo lakini pia tutizame na ufanisi ambao watakuwa nao katika ufanisi huo kwa muda huu aliofika haya tulikuwa tumeyakosa kwa muda mrefu sana.

Lakini Mhe. Spika, suala la upendeleo sasa hivi linageuka kwa namna nyengine watu waliokuwa watumishi wamemaliza muda wao wanarejeshwa tena, wameshapewa viinua mgongo lakini unamkuta yupo ofisini pale huku kuna msururu wa vijana wenye uwezo ambao labda nao wangepata nafasi ile wakaendelezwa bado umri wao ni mdogo tunatarajia kwamba watakuwa na muda mrefu wao kazini, lakini hawa wananyimwa kwa sababu tu fulani ameondoka kule na huyu ni mwenzetu tusimuache akaathirika. Lakini hayo tuna viongozi wetu maalum ambao wametajwa kwa mujibu wa sheria kwamba hawa wapate huduma maalum kwa kuyakimbia hayo, lakini sasa yanakuja mpaka kwenye ngazi ambazo zinatizama huu upendeleo ama mfumo wa kisiasa.

Mhe. Spika, Sheria hii tukijaaliwa itatusaidia sana katika kulinda na kudumisha heshma ya Zanzibar, Zanzibar ambayo kwa leo duniani inatajwa vyengine kuliko hivyo tulivyokuwa zamani, muundo wa utumishi kwa kadri itakavyowezekana nasema kwamba watakuwa ni watu wa Zanzibar. Hili nalo lina umuhimu kilio kikubwa sasa hivi kipo kwa sababu vijana wetu wanakoseshwa ajira au wanazikosa ajira na badala yake zinavamiwa na wageni, kuna sababu za hapa na pale lakini kuna Mhe. Mjumbe hapa alisema hivyo ni kweli hata kutandika kitanda Mzanzibari hajui, sio kweli kuna mengine labda kwa taaluma mimi hilo sibishani nalo lakini kwa sababu tunajikita sasa kujenga misingi na maadili ya utumishi hayo nayo ni imani yangu kwamba Mhe. Waziri atayazingaria ya kutoa taaluma kwa watumishi, wetu ili yale mambo ambayo hatuna uwezo nayo tunalazimika kupata wenzetu

watusaidie ndio hao wageni kwa hapo hatutokuwa na hoja, lakini tunaweza kuwajenga vijana wetu na nafasi tuweze kuzimudu wenyewe.

Mhe. Spika, nadhani pia ule utamaduni wa kuwazawadia watumishi bora nadhani tuendelee nao, ile inamjenga mtumishi kumpa morari ya kufanya kazi kwa bidii anapomuona mwenzake anapata heshima ile ya kuzawadiwa kwa kile alichokifanya, bidii ya kazi itajengeka tu endapo na sisi mtumishi huyo tutamjenga.

Nidhamu ni suala nyeti Mhe. Spika, katika utumishi bila ya nidhamu na maadili mazuri tunayakosa na sasa hivi nidhamu hii sio tu kwamba mtumishi awe nayo lakini nafikiri na muajiri nae hatuna budi sasa tuwatizame watumishi wetu kwa kuwajenga kwa maslahi yao na mafao, tunapoteza vijana wengi wataalam wazuri kwa sababu mafao tunayowapatia hawa hayalingani hata kidogo na uhalisia. Kijana anarudi masomoni na wenzake akirudi hapo mrima anaambiwa hiyari yako uzalendo huo rudi matokeo wanaondoka watano na wawili wanarudi.

Mhe. Spika, suala la mafao pamoja na kilio chetu pamoja na hali yetu ya uchumi lakini sasa nadhani tujipange, mimi suala la uchumi napigana nalo sana kwa sababu imani yangu inanambia bado tuna nyanja nzuri sana za uchumi wetu ubadilike kutoka hapa tulipo ni suala la kujipanga tu. Zanzibar kuondokana na umasikini inawezekana kabisa wala hiyo haitaki longo longo, tukijipanga tutaweza kama walivyoweza haiwezekani kama Mauritius kuondoka walipokuwa kwa nini tusiweze sisi mazingira yetu yanafanana sana. Tuna nafasi kubwa ya vianzio vya uchumi.

Mhe. Spika: Mheshimiwa umebakiwa na dakika tano.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Spika, nashukuru nimekusikia lakini ilikuwa namalizia. Mhe. Omar Ali Shehe kaliogolea lakini Mhe. Spika, kwa unyeti wake naomba niseme kwamba *scheme of service* ambayo kwa muda mrefu imeonekana ni suala la kelele za watumishi lakini ina maana yake, sasa ndio hilo ninalolisemea linazaa matatizo mengine.

Lakini sasa huu uliotajwa kwenye sheria kwamba uwepo utumishi chini ya mapitio ya kawaida kwa ajili ya kuhakikisha malipo, mafao na maslahi na mfumo huu kwamba uhusiano wa utumishi na kisiasa. Waheshimiwa wajumbe wa Baraza lako tumezoea kwamba kwa mujibu wa katiba yetu anayejua kusoma na kuandika tayari yeye inampa nafasi ya kuchaguliwa kuwa mjumbe wa baraza lako tukufu, lakini sasa kuna mchujo hapa kwa mujibu wa maelezo haya. Lakini hapa sasa Mhe. Waziri itabidi atufafanulie tujijue mapema tokea asubuhi.

Mhe. Spika, la mwisho kwa leo ieleweke kwamba wanasiasa wa Zanzibar tunfaya kazi ya ziada kuisaidia serikali yetu, izingatiwe sana sheria hii mfumo wetu kuchanganywa na ule wa utumishi wa umma nadhani kama mwenzangu alivyosemea haitokuwa sahihi sana.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo machache nakushukuru ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mtumwa Kheri Mbarak: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa na afya na uzima na kuweza kufika leo kutekeleza majukumu yetu, mimi kama nilivyokuwa mjumbe wa kamati nimesimama hapa kumuwekea sasa kwenye Hansard Mwenyekiti wangu.

Mhe. Spika, sehemu ya sita ya mswada katika sehemu ya uhusiano wa utumishi, wakati alipokuwa anatoa hotuba yake kidogo matamshi yalikosea kifungu kifungu cha 13 cha katiba ya Zanzibar kwenye tafsiri ya neno Utumishi wa Umma ambacho kinaeleza wazi kuwa utumishi wa umma haujumuishi, nadhani hii ndio ilikuwa kauli sahihi ambayo alikosea kidogo pale kwa hivyo naweka hansard sawa kuwa haujumuishi utumishi wa kisiasa.

Kwa hivyo ningeliomba hansard kidogo ikakaa sawa. Baada ya hapo niingie kwenye ukurasa wa 59, vile vile hapa naomba tufanye marekebisho kidogo. Ukurasa 59 kwenye *table* hiyo katika sehemu ya 41, kuna sehemu imeandikwa unyangaji naomba tufanye masahihisho, nadhani hapo imekusudiwa unyanyasaji au kufanya aina yoyote ya unyanyapaa ikiwemo ubaguzi wa ukabila.

Jengine Mhe. Spika, tunakuja ukurasa wa chini napo tungefanya marekebisho katika sehemu ya 48 kuna neno limeandika ukimya nadhani kilichokusudiwa ni kushindwa kuweka vitendea kazi au sehemu ya kazi vizuri.

Mhe. Spika, jengine nije katika ukurasa 63 hapa kidogo ningeomba nipate ufafanuzi. Mhe. Waziri hapa nimeshtuka kutokana na hii adhabu iliyokuwepo hapa naomba unipatie ufafanuzi pengine sikufahamu kutokana ama na huruma au sijui kitu gani.

Kutofika kazini bila ya sababu ya msingi na kudanganya muda wa kufika kazini. Hapa nimeona kwamba huyu mtu hakufika kazini bila ya sababu ya msingi lakini kapewa onyo la mdomo, onyo la maandishi, onyo la mwisho la maandishi na kadhalika na kuendelea. Lakini huyu kaja kazini kosa lake kadanganya tu muda wa kufika kazini.

Mhe. Spika, tutakuwa na wafanyakazi hapa. Adhabu yake kupunguzwa mshahara au kuteremshwa cheo au kusimamishwa kazi na kusubiri uchunguzi.

Mimi ningeliomba Mhe. Waziri kidogo anisaidie kwa hali hii, naona huyu ambaye hakufika kazini kapewa onyo, huyu kafika kazini na pengine amefika kazini mtu aliyefika mwanzo kafika saa 1:29 alivyomuona mwenziwe ndivyo alivyoandika pale na alipokuja yeye akaongeza moja ikawa saa 1:30. lakini pale pale ikaja ikamuangukia bahati mbaya. Mimi naona tuwatizame na wafanyakazi wetu tukitunga sheria, adhabu hii tuitizameni kidogo tuone kwamba hizi sheria hatuwatungii wao tu lakini zitatugusa na sisi hizi sheria.

Mhe. Spika, mimi nashukuru sana Mhe. Waziri kukaa viongozi wetu kutuletea Mswada huu. Ninaimani Mswada huu utatusaidia sana katika kupata maadili mazuri ya utendaji wa kazi katika utumishi wa umma. Namshukuru sana na nawaomba wajumbe muuchangie na tuupitishe ili tuweze kuweka mazingira mazuri katika utumishi wetu.

Mhe. Spika, kama mimi nilivyokuwa Mjumbe wa Kamati kwa hivyo sikuwa na maelezo mengi zaidi katika Mswada huu. Moja ni kuweka Hansard uzuri na kufanya marekebisho haya mafupi. Nakushukuru Mhe. Spika, ahsante.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi hii kutoa mchango wangu mfupi sana katika Mswada huu wa Utumishi wa Umma ambao Mhe. Waziri ameuwakilisha asubuhi hii.

Mhe. Spika, kwanza kabisa nitumie nafasi hii kuipongeza Kamati ya Katiba na Sheria kwa kazi kubwa waliyoifanya. Kwa kweli katika historia ya Baraza hili, miaka mitano iliyopita niliyokuwemo sijaona marekebisho makubwa kama ambavyo walivyoyafanya haya ambayo yametokezea.

Mhe. Spika, Kamati yako ya Biashara ina watu wazuri na bila shaka hizi ni busara zako ambazo zenye mamlaka ya kuchagua watu waingie kwenye Kamati zipi. Kazi hii ambayo Kamati ya Katiba na Sheria wanayoifanya ni kazi ambayo haihitaji kupuuzwa. Ni kazi ambayo ni muhimu na kama si busara ya Baraza lako basi nadhani Mswada huu hata tungesema urejeshwe kwa sababu haukukidhi matakwa ya Kanuni katika siku 21. Lakini busara za Kamati na Waziri wetu ndio tumeamua kuujadili ili kusogeza mambo yetu mbele.

Mhe. Spika, kanuni imetukataza kwamba tusirejee rejee mambo, lakini kutokana na umuhimu wa jambo lenyewe inabidi tuchangia kwa upeo mwengine. Kwa misingi hiyo na mimi naomba nichangie moja kwa moja kwenye kifungu cha 6 cha Mswada huu.

Mhe. Spika, nataka niwakumbushe wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba kabla hatujaanza kwa Baraza hili tumeapa kwa kutumia misahafu kwamba Wawakilishi tutalinda Katiba ya Zanzibar na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa msingi huo naomba hasa waandishi wa habari watuelewe kwamba hatukatai kifungu cha 6 kwa sababu sisi ni Wawakilishi, tunakataa kifungu cha 6 kwa sababu sisi ni walinzi wa Katiba ya Zanzibar na Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, kifungu cha 6 kinapingana na katiba ya Zanzibar kifungu cha 134 moja kwa moja, kwa hivyo kifungu hicho kifutwe. Naomba Mhe. Waziri kuhusiana na mjadala, kifungu hichi atukubalie kwamba kimekiuka Katiba ya Zanzibar, kifutwe moja kwa moja.

Mhe. Spika, kifungu cha Sheria ambacho kinapingana na Katiba kifungu hicho kinakuwa na batil na Katiba ndiyo inakuwa imechukua nafasi. Kwa hiyo kwa utafsiri wowote hata wale *bush lawyers* kama mimi Mhe. Salmin basi tukiona kifungu hichi kimepingana na Katiba ya kifungu cha 134 na kwa hivyo kifutwe tusikiunge mkono Wawakilishi wote.

Mhe. Spika, nikichangia Mswada huu niungane na wenzangu hasa Mhe. Mshimba kwamba Mamlaka ya Katibu Mkuu Kiongozi ni makubwa mno, ni lazima Mhe. Waziri akubaliane nasi kwamba mamlaka haya yapunguze. Huyu ni binaadamu si malaika, leo yupo Katibu Mkuu Kiongozi Mzuri, keso atakuwa Hija. Huwezi kumtafsiri mtu kwa rangi au sura.

Mhe. Spika, Mamlaka ya Katibu Mkuu Kiongozi anayewekwa ni lazima yazingatiwe kwa upeo wa maendeleo ya nchi hii. Si tu kumuangalia mtu aliyekuwepo leo. Unaweza leo ukawa na mtu mzuri sana kesho, akaja mtu mwengine mwenye nia nyengine mbaya, akaathiri wafanyakazi wetu na akaathiri uchumi wa nchi yetu. Bila ya wafanyakazi, bila ya watumishi wa umma hakuna uchumi katika nchi.

Mhe. Spika, mimi nasema kwamba Mamlaka ya Katibu Mkuu Kiongozi yaangaliwe upya na yapunguzwe. Vifungu vingi humu vinaeleza kwamba ataweka maamuzi na matakwa kwa vile anavyoona inafaa.

Mhe. Spika, mtu anavyoona inafaa mtu huona mengi ambayo yanafaa na kumbe si sahihi. Nadhani matakwa na mamlaka ya Katibu Mkuu Kiongozi wataalamu wa Wizara hiyo waangalie na wakubaliane nasi kwamba wapunguzwe kwa ustawi wa wafanyakazi wetu na utumishi wa umma Zanzibar.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningependa nilichangie haraka haraka ni ushirikishwaji wa wadau hasa vyama vya wafanyakazi, kama ambavyo Mhe. Mshimba amesema, kwa kweli hatujawafanyia haki wafanyakazi wetu na wadau wengine katika Mswada huu. Bila shaka mara nyengine ni vyema tutazingatia umuhimu wa kuwashirikisha wadau ili tupate ufanisi wa jambo hili na mambo mengine kwa ustawi wa Zanzibar.

Kuwadharau wafanyakazi wetu au wadau wa Mswada huu ni kutokuwafanyia haki Wazanzibari. Kwa hivyo hili tunalijadili na bila shaka Mhe. Waziri ametusikia, ningemuomba kwa mara nyengine na Waziri mwengine yeyote yule azingatie umuhimu sana wa kuwashirikisha wadau katika upangaji wa masuala yote na ustawi na maisha ya nchi.

Mhe. Spika, mwisho kabisa kifungu cha 15 kinaeleza kwamba Katibu Mkuu Kiongozi atapokea ripoti kutoka kwa Makatibu Wakuu wa Wizara na ripoti hizo hatimaye atazipeleka kwa Mhe. Rais kwa hatua zaidi. Mimi nasema kwamba kwa sababu Baraza la Wawakilishi ndio wasimamizi wa serikali, ripoti hizi zisimalizie kwa Rais, zije na Baraza la Wawakilishi zijadiliwe. Kwa sababu ripoti kutoka kwa Makatibu Wakuu wa Wizara hadi kufika kwa Katibu Mkuu Kiongozi bado ni muhimu na Makatibu Wakuu wa Serikali.

Mhe. Spika, ushauri wangu kama ilivyo ripoti ya PAC, Tume ya Raisi baadaye ije kwenye Baraza la Wawakiishi na ripoti za Katibu Mkuu Kiongozi zote zimalizie Baraza la Wawakilishi kwa hatua za mwisho za utekelezaji.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo Mhe. Waziri akiongeza kifungu cha 6 nitaunga mkono mia kwa mia kwa niaba ya wananchi wangu wa jimbo la Kiwani.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, nashukuru na mimi kwa kupata nafasi hii ya kuchangia Mswada huu. Namshukuru Mhe. Waziri kwa kuleta Mswada ambao unaweza kusaidia kaifa letu katika masuala mazima ya utendaji wa kazi za kila siku.

Mhe. Spika, mimi ninamichango kama mine, mchango wa kwanza upo katika kifungu cha 11 ambacho kinaelezea “Rais atakuwa ni msimamizi Mkuu wa Utumishi wa Umma na mtu yeyote anashikilia Afisi ya Utumishi wa Umma isipokuwa kwa utumishi katika Mahakama au pale ambapo Katiba imeweka utaratibu ya uwajibikaji wa afisi hiyo ya utumishi wa umma.

Mhe. Spika, ningeona kwa maoni yangu hekma na husara basi baada ya kuweka Mahakama peke yake basi pakaongezwa na neno Baraza la

Wawakilishi. Kwa sababu kuweka Mahakama peke yake naona kutainyima haki Baraza la Wawakilishi kuwepo katika kifungu hiki.

Mhe. Spika, ningeomba nichangie katika kifungu cha 74 (1)

Kifungu cha 74(1) "Hakuna mamlaka inayoweza kumuachisha kazi mfanyakazi ambaye ni Afisa wa Cheo cha Juu isipokuwa Katibu Mkuu Kiongozi ametoa cheti kinachoeleza kwamba:"

Mhe. Spika, kwa maoni yangu naona yale mamlaka aliyopewa Katibu Mkuu Kiongozi ni makubwa sana. Ni vyema basi pawe na kitu cha nyongeza Rais awe na Mamlaka ya peke yake. Pawepo na kifungu cha kumuwajibisha Katibu Mkuu Kiongozi pindipo na yeye kutatokezea namna moja au nyengine katika masuala ya utendaji wake wa kazi. Yeye ni binaadamu anaweza akawa na matatizo, tukimwachilia tu kama hakuna kifungu ambacho kitakachoainisha yeye uwajibikaji wake utakuwa wapi hili ni tatizo. Ni vyema tukaangalia nini cha kuongeza.

Kwa mfano tunaweza tukaweka Baraza la Mapinduzi linaweza likakaa na kumjadili Katibu Mkuu Kiongozi pale ambapo ataonekana na yeye ametenda kosa moja au jengine ili apate kudhibitiwa kwa namna moja au nyengine.

Mhe. Spika, jengine ambalo nilikuwa napenda kuchangia ni katika kifungu cha 76.

Kifungu cha 76(1) "Mkuu wa taasisi ya utumishi wa umma, baada ya kuthibitishwa na Bodi ya Utumishi, …"

Mhe. Spika, baada ya kusoma kote Mswada huu kitu bodi kidogo kilikuwa kinanipa matatizo nilikuwa sijapata kukiona. Hapa kidogo naona pananitanza katika uwekaji sawa wa kifungu hiki. Ni vyema kama itakuwa inawezekana baada ya kusomeka neno bodi ya Utumishi ni vyema basi ikasomeka Tume ya Utumishi.

Mhe. Spika, baada ya mchango huo naomba kukaa. Ahsante.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii pengine itakuwa ya mwisho kwa saa hizi ili kutia baraka zangu mbili tatu katika Mswada huu muhimu sana.

Mhe. Spika, mimi kwanza nataka niipongeze serikali kwa kuchukua hatua hii ya kuleta Mswada huu wa Utumishi wa Umma katika Baraza hili. Utumishi wa

umma ni muhimu na nathubutu kusema ndiyo roho ya nchi. Maendeleo yote katika nchi yanapatikana kupitia sekta hii ya utumishi wa umma. Kwani ndiyo inayotoa huduma na ndiyo inayoleta uzalishaji katika nchi.

Ni sekta muhimu kwa nchi na kwa wale watumishi wa umma wenyewe. Kwa sababu na wao hawawezi kuendelea bila ya kuwa katika ajira au katika utumishi wa mambo kama hayo ndimo wanamojipatia riziki yao, kwa hivyo ni jambo muhimu.

Mswada huu ni muhimu sana kuletwa kwa sababu tulikuwa tupo hewani, utumishi wa umma ulikuwa hauna mashiko. Mswada huu nadhani unaweza ukaweka mkakati wa mashiko katika utumishi wa umma. Nasema tulikuwa tupo hewani kwa sababu kulikuwa kuna mambo mengi yana kasoro.

Kwanza kabisa hata maslahi ya wafanyakazi yalikuwa yanalalamikiwa sana. Watumishi wa serikali wengi wao hali zao ni mbaya. Matarajio yangu ndani ya Mswada huu kuna kifungu ambacho kinamuelekeza waziri kutunga kanuni ya mambo kama hayo. Changamoto hii nayo inaweza ikaondoka baada ya kuwekewa utaratibu mzuri zaidi.

Mhe. Spika, pia kuna kasoro kubwa ya utendaji wa kazi. Sijui kama nitakuwa sahihi nikisema hivi lakini kwa kweli watendaji wetu ama ni wazembe au ni wavivu. Wazanzibari hatuna utamaduni wa kujituma katika kazi. Mimi mara nyengine husema kwa nini sisi hatufiki kwenye malengo ya kimaendeleo wakati watu tunao, sekta za kazi zipo, lakini bado siku zote Wazanzibari tunakuwa tupo nyuma kimaendeleo, nchi yetu haiendelei. Lakini nikagundua utendaji wetu wa kazi ni wa kubahatisha au wa kuripua ripua.

Mhe. Spika, unaweza kushangaa kazi ambayo sisi waswahili twenye ngozi nyeusi huwa tunasema wenzetu wazungu ni watu legelege, tepetepe hawana uwezi wa kufanya kazi vizuri, yaani hawawezi kujituma sana. Lakini unaweza ukashangaa kazi ambayo anaifanya mzungu akija hapa kama *contractor* ni kubwa zaidi kuliko tunazozifanya sisi.

Mhe. Spika, wanaweza wakagaiwa watu kazi kwa hali ya kawaida binaadamu wa kawaida anaweza kuifanya ndani ya siku tatu ikamalizika. Lakini mfanyakazi yule atakwenda akikaa chini ya kivuli weee, masaa yakimaliza atakwenda zake na siku ya pili, wiki mbili kazi ya siku tatu hajaimaliza. Mimi nadhani hilo ni moja katika changamoto yetu kubwa. Ndani ya Mswada huu mambo hayo yatazingatiwa.

Nafikiri ndipo serikali ilipoona kuna haja ya kuleta huu Mswada kwa kurekebisha kasoro kama hizo. Tunataka maendeleo ni lazima tujitume, tukiwa

hatuwezi kujituma nina hakika mimi hatutofikia maendeleo hata siku moja, tubakia kuomba omba na kusaidiwa.

Mhe. Spika, nimevutiwa sana na maelezo yaliyokuwemo katika kifungu cha 4 na naomba nikinukuu kidogo.

Kifungu cha 4 (1) "Utumishi wa Umma Zanzibar utafuata misingi ya lazima na kila afisa anayehusika na usimamizi wa afisi yoyote ya umma atahakikisha anatekeleza ipasavyo misingi ifuatayo:

(i) Kujielekeza katika matokeo ya kazi;…"

Yaani kujielekeza katika malengo ya kazi, kazi hii lengo lake tufikie wapi. Lazima awajibike ahakikishe kwamba lile lengo linafikiwa, ni jambo muhimu sana. Kujielekeza kwa mtoa huduma, wewe umeambiwa utoe huduma fulani lakini huduma hii apewe fulani. Lazima uhakikishe kwamba yule mlengo ile huduma anaipata.

Hiki kifungu ni muhimu sana lakini kina kasoro moja, kasoro yake kimemtaja Afisi tu. Nilipokuwa naangalia tafsiri ya Afisa wa Utumishi wa Umma imo katika ukurasa wa tatu anasema:

Kifungu cha 3(c) "afisa utumishi wa umma" maana yake ni mwajiriwa katika utumishi wa umma anayeshikilia wadhifa au daraja (cheo) kinachotambuliwa chini ya muundo wa utumishi unaohusika,…"

Inaonekana hiki kifungu kinamuhusu yule afisa tu mwenye cheo. Je, mtumishi wa kawaida hawajibiki yeye kujielekeza katika matokeo ya kazi. Je, hawajibiki kujielekeza katika kutoa huduma. Nilikuwa nahisi hapa pana kasoro kidogo. ilikuwa hiki kifungu kimtaje afisa anayehusika na usimamizi wa utumishi, lakini pia na mfanya kazi wa kawaida ndio kinamuhusu. Mhe. Waziri hili angelilizingatia akaongeza japo sentensi moja itakayomuhusisha na yule mfanyakazi wa kawaida sio awe ni afisa tu kwa mujibu wa tafsiri hii ya afisa alivyotajwa, labda niwe sijui Kiswahili vizuri. Lakini kama najua Kiswahili vizuri afisa huyu aliyekusudiwa ni msimamizi wa ile sekta anayosimamia. Lakini yeye anasimamia watu, sasa hawa watu nilikuwa nadhani na wao wanamajukumu kama haya lakini sheria hii haijawaelekeza huko, haiwabani.

Mhe. Spika, kifungu cha 5(2) (a) naomba nikinukuu:-

Kifungu cha 5(2)(a) “maamuzi ya uajiri katika utumishi wa umma wa Zanzibar yatafanywa bila ya kujuana, upendelea au utashi wa kisiasa;”

Mhe. Spika, hapa natoa wasia kwa Mhe. Waziri na taasisi zake za utumishi wa umma, huku tunakotoka hakukuwa kwema katika hili. Na nilikuwa mara nyengine nilikuwa nayashuhudia kwa mamcho yangu. Kule katika jimbo langu kuna sheha mmoja yeye ni CCM lakini mwanawe aliyemzaa mwenyewe ni CUF. Kulikuwa kuna utaratibu wa kutoa ajira kupitia kwa masheha. Sheha yule alimuapia yamini mwanawe akamwambia ulivyokuwa ni CUF nafasi ya ajira ninayo lakini sikupi, na hakumpa kweli.

Sasa nilikuwa naomba sana na natambua sana busara aliyokuwa nayo Mhe. Waziri, lazima apewe wasia mara kwa mara, apewe nasaha mara kwa mara kwa watu wanaohusika na ajira wasije wakarudia huku tunakotoka. Hapa tulipo tupo pazuri sana, nafikiri twende mbele tusirudi nyuma.

Mhe. Spika, kifungu cha 11 hichi kinampa uwezo Rais wa kuamua ukubwa na ubora wa utumishi wa umma. Kifungu hiki kinaowana kidogo na kifungu cha 79 ambacho kinataja viwango vya kazi. Kuna mambo mengi yameelezwa pale katika kifungu cha 79. Lakini pamoja na yale yote yaliyoelezwa nilikuwa nadhani na haya yafuatayo yangejumuishwa.

Uwezo wa kitaaluma. Katika kuangalia viwango vya ajira basi iangaliwe na ukubwa wa ile ajira yenyewe lakini na ubora wake. Ubora huu utatokana na uwezo wa yule mtu anaepewa ile nafasi husuka.

Nilipokuwa nayaangalia haya mambo katika kifungu cha 79, sikuona hiki kifungu cha uwezo wa kitaaluma, nafikiri ni vizuri Waziri angelizingatia sana. Tukiwa na uwezo wa kitaaluma halafu tukaangalia na masaa ya kazi ambayo yameelezwa. Masaa ya kazi yanaendana na maslahi ya wafanyakazi.

Sasa hivi ni masaa manane (8), tukisema kama tunazingatia masaa ya kazi yaongezwe na ndivyo ilivyoelezwa katika Mswada huu. Ni vyema yule mtu akishakuwa na taaluma inayohusika halafu ukamuongezea na masaa ya kazi basi na maslahi yake nayo uyaangalie vizuri.

Mhe. Spika, tuna vijana wetu hapa mara nyengine hutoroka hapa nchini jambo ambalo mimi nalilani kwa nguvu zangu zote, wanakimbilia Ulaya. Akifika kule anapewa kazi mbovu ambayo angekuwa katika mazingira ya hapa Zanzibar asingeifanya angeona aibu yeye kufanya kazii kama ile. Anaifanya kazi hiyo pengine kwa masaa 20 usiku halali. Lakini malipo anayoyapata akifanya kazi hiyo miaka miwili inamsaidia yeye kupata msingi wa kuishi hapa Zanzibar.

Kwa hivyo, si uzuri kufanya kazi ile lakini maslahi yanayopatikana yanakwenda sambamba na ile kazi anayoifanya na anachokifanya kinajulikana.

Kwa hivyo nilikuwa naomba sana tuongeze masaa ya kazi lakini pia tuwalipe wafanyakazi wetu vizuri inavyostahili kwa kazi wanazozifanya.

Ilivyokuwa wakati unakimbia sana naomba nimalizie kwa kifungu cha 50.

Mhe. Spika, kifungu cha 50(1) kuna uanzishwaji wa taasisi pale, naomba nikinukuu kidogo.

Kifungu cha 50(1) "Kamisheni itakuwa na wajibu wa kumshauri Rais kuhusiana na hadhi ya taasisi ya umma na muundo unaofaa na kuzipanga taasisi na utekelezaji wake."

Kifungu cha 50(2) "Katika kutekeleza kazi ya ushauri chini ya kijifungu cha (1) cha kifungu hiki, Kamisheni itazingatia:

(a) faida za kiuchumi na kijamii;"

Mhe. Spika, hili ni jambo muhimu sana Raisi anauwezo wa kuunda taasisi na kuzivunja, leo akaiunda halafu akiiona haina faida akaivunja, kesha akaona kuna haja ya kuunda taasisi nyengine akaiunda. Hii sheria inampa uwezo huo Rais.

Mimi nilikuwa natoa angalizo katika kutekeleza hilo basi serikali kupitia waziri na Mhe. Rais, waangalie faida inayopatikana katika vikosi viwili, Kikosi cha JKU na kikosi cha KVZ, sina tatizo na kikosi cha KMKM, wala sina tatizo na kikosi cha Zima Moto wala magereza kutokana na kazi zao muhimu na nyeti sana.

Mhe. Spika, kikosi cha JKU kina wastani wa chini bilioni 5 kwa mwaka. Sasa tujiulize je, kile kinachozalishwa kinakidhi hapa au angalau kinalingana na hapa. Naomba Mhe. Waziri hilo aliangalie. Kikosi cha KVZ kina wastani wa kutumia bilioni 3 kwa mwaka. Vikosi viwili hivi viangaliwe, ikionekana havizalishi kuliko matumizi basi Mhe. Rais ana mambo mawili yakufanya ama kuvifuta au kuviboresha zaidi vikawa vinazalisha, lakini isiwe vinakwenda kwa hasara.

Mhe. Spika, jambo la mwisho kabisa nilikuwa naangalia sana katika huu Mswada sijaona mageuzi ya serikali za mitaa humu. Sijui hayahusiki yale na Mswada huu au vipi. Nilikuwa nahisi serikali za mitaa ni jambo muhimu sana

na ni sekta muhimu ya uzalishaji au ya ukusanyaji mapato katika nchi yetu. Ilikuwa ni vyema yazingatiwe vizuri katika huu Mswada, lakini hayakugusiwa katika mahali popote. Naomba sana waziri alizingatie hilo.
Mhe. Spika, baada ya kusema hayo kwa sababu muda wako umemalizika naomba na mimi niunge mkono hoja kwa asilimia 100. Ahsante.

Mhe. Spika: Kabla ya kuahirisha kikao kuna matangazo mawili.
Kwanza waheshimiwa wajumbe wanawake watakuwa na mkutano wa uchaguzi wao katika ukumbi wa juu pale ukumbi mkubwa wa mikutano mara baada ya kuahirisha kikao hichi. Kwa hiyo ukitoka tu hapa wanaelekea juu kwenda kufanya uchaguzi wa jumuia yao ya Uwawaza.

Pili waheshimiwa wajumbe mnaarifiwa kwamba kesho baada yakuahirisha Kikao mnamo saa 7:00 kutakuwa na uchaguzi wa viongozi wa Klabu yetu ya Michezo ya Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo nayo hiyo inawahusu wajumbe wote, tunatakiwa tuhudhurie kwenye Kikao hicho cha uchaguzi wa viongozi wa Club ya Baraza la Wawakilishi kuhusumichezo.

Baada ya hayo waheshimiwa wajumbe nakushukuruni na sasa naahirisha kikao hiki hadi saa 11:00 jioni.

(*Saa 7:00 Baraza liliahirishwa hadi Saa 11:00 jioni)*

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii. Mhe. Spika, mimi nataka nichangie kifungu Nam. 6 cha mswada huu, lakini kwa mtazamo wangu katika kifungu hiki kuna mambo mawili ya msingi ambayo yanajadiliwa. Mhe. Spika, kubwa ambalo nimelibaini hapa ni sera ndizo ambazo zinazungumzwa zaidi katika kifungu hiki. Kuna sera ya utumishi na kuna sera ya malipo.

Mhe. Spika, kwa sababu wawakilishi baada ya kwishakuingia katika eneo hili wao wanakuwa ni watumishi wa wanaishi. Kwa hivyo, sera ya kimaadili katika masuala ya utumishi wao inawagusa moja kwa moja. Pia sera ya malipo kwa sababu wawakilishi wanalipwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar nayo pia itakuwa wanakitumia kipengele hiki kusababisha hayo malipo.

Mhe. Spika, kwa msingi huo kwa mtazamo wangu mimi naona bado kifungu Nam. 6 kiendelee kubakia.
Mhe. Spika, baada ya hayo mimi naunga mkono hoja hii.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia katika mswada huu. Kabla sijaingia katika mswada Mhe. Spika, napenda niseme kwamba naunga mkono hoja ya kuwepo kwa sheria hii kwa sababu mbili kubwa. Sababu ya kwanza ni ile ambayo tulielekezwa na wanasheria wetu akiwemo Mkurugenzi wa Uendeshaji Mashtaka kwamba hiki kitu hakipo na kingehitajika kuwepo. Kwa hivyo, kwa sababu hakipo na kingehitajika kuwepo hili ni moja lililonishawishi kwamba tuendelee na kujadili mswada huu na tuupitishe.

Mhe. Spika, jambo la pili ni kwa sababu kuna malalamiko mengi ya watumishi wa umma katika taratibu za uendeshaji za ofisi zetu. Na kwa sababu tumelemaa katika kuendesha kienyeji ni bora tuanze pale padogo kwanza na mambo yatakwenda kidogo kidogo, lakini ningemuomba sana Mhe. Waziri akakubaliana na mimi kwamba baada ya miaka miwili ya kupitishwa sheria hii iletwe tena katika Baraza hili kwa kuikamilisha. Mhe. Spika, kwa sababu ni hakika sasa hivi kutokana na mazingira yalivyo na hali ilivyo, basi sheria hii haitokuwa na usahihi wa kutosha au ufanisi wa kutosha katika kupitishwa kwake.

Mhe. Spika, kwa nini nikachukua kipindi cha miaka miwili. Mhe. Spika, kwa sababu ndani ya miaka miwili tunaweza tukasoma mambo mengi na kwa sababu tumejipangia hasa kwamba ndani ya miaka miwili tufanye tathmini ya pale tulipofikia na kuu-*renew* mswada wetu ili kuweza kumaliza vizuri katika kipindi hiki cha miaka mitano ya awamu hii tutakuwa na kazi tuliyokwishajipangia. Lakini tukiuchukulia kwa mnasaba huu kwamba ndio *fainal* tuendelee tu, basi itakuwa ni vigumu kuweza kukubaliana na hoja hiyo kwani bado kuna mambo mengi ambayo yataonekana kwamba yana kasoro za pale na pale.

Mhe. Spika, kwa mfano suala hilo linalobishaniwa sasa hivi, ni dhahiri katika dunia kwamba sehemu ya utumishi wa kisiasa inatenganishwa na utumishi wa umma. Kwa sababu pamoja na katiba ilivyotaja lakini katika ulimwengu huu utumishi wa kisiasa unabadilika, kila kiongozi anayeingia madarakani ana vipaumbele vyake katika mambo ambayo anatekeleza. Lakini utumishi wa umma unabaki pale pale kutekeleza vile vipaumbele vitakavyowekwa.

Kwa hivyo, sio sahihi kuoanisha baina ya utumishi wa kisiasa na utumishi wa umma, na sio sahihi katika njia zote ambazo utazipelekea Mhe. Spika. Kwa sababu watumishi wa umma huwa wanazingatia mambo mengi ambayo yanamgusa kila mtu katika jamii, aliyekuwa katika siasa, mwenye chama na aliyekuwa hana chama na kila mmoja anaingia. Mhe. Spika, lakini kada mbili ukizilinganisha unaweza ukatokezea utata huenda moja ikamshawishi mwenzake na hapo ndio patakapokuwa na matatizo.

Mhe. Spika, kwa rekodi ya *hansard* mimi napenda kusisitiza tena mambo mawili ambayo niliyatoa wakati tulipokuwa tunafanya semina. Mhe. Spika, mara nyingi tunakuwa na sheria nzuri au sera nzuri, lakini utekelezaji wake unasuasua kwa sababu nyingi. Kwa mfano, katika matatizo haya ya utumishi wa umma kunakuwa na ubinafsi unatawala, muda utakaotawala ubinafsi tusifikirie kabisa kwamba sheria hii itatekelezeka. Jamii ambayo maslahi ya binafsi yanawekwa mbele kunakuwa na kasoro nyingi zinaweza zikajitokeza na yale matatizo halisi yakawa hayakuonekana. Kwa hivyo, mimi ningependa sana kumtaka Mhe. Waziri kwa kupitia ngazi mbali mbali za utendaji ahakikishe kwamba mambo matatu yanapatikana.

Mhe. Spika, kwanza ni elimu ya kutosha ya sheria kwa maafisa wote wa serikali wale watendaji wakuu. Mhe. Spika, ni dhahiri kwani sisi tunatokea utumishi wa serikali maafisa wengi wanatumia amri kutoka kwa wakubwa kuliko kufuata mtandao wa sheria ulivyo. Hata kama angependa kufuata sheria basi asingeruhusika kufanya hivyo kwa sababu amri ndio za wakubwa zinazotawala. Mhe. Spika, kwa sababu tunaingia katika mfumo mwengine basi tusikubaliane kabisa na suala la amri kutawala.

Mhe. Spika, hapa hapa Zanzibar kuna taasisi sasa hivi huwezi kuamini zinavyokwenda mbio kwa sababu ya kujipangia utaratibu wa utawala ambao sheria waliyoipanga pale wanaifuata. Taasisi hizi tumezitembelea katika nyakati mbali mbali wakati wa kamati zetu zilizokuwa zikifanya kazi. Kwa hivyo, inaonesha hapa Zanzibar tunaweza tukapiga hatua nzuri itakapokuwa sheria itatumika na kanuni zitatumika badala ya kutumia amri za wakubwa kwamba fanya hivi fanya hivi kuiweka kando sheria. Mhe. Spika, tunaweza kuwa na sheria nzuri lakini huko juu haitumiki.

Mhe. Spika, la pili kuwe na mikataba inayoeleweka baada ya sheria hii kupita waajiriwa wote wawe na mikataba inayoeleweka kufafanuliwa kazi zao, maslahi yao na fursa zao badala ya kupata uajiri ambao unasema tu umeajiriwa. Kwa njia hiyo wizara hii itoe fursa kwa wale waajiriwa waweze kuelezea zile kero zao. Kwa hivyo, suala la utawala bora ambalo bahati nzuri sana bila ya shaka Mhe. Rais alipaona hapo kwamba hii Wizara ya Utumishi ilichanganywa na utawala bora kwa sababu mambo mawili haya lazima yawe pamoja. Mhe. Spika, hatuwezi kupata ufanisi katika utumishi wa umma kama hatujafuatana sambamba na utawala bora, na utawala bora utaja kuhusu uwazi na uajibikaji katika mambo.

Mhe. Spika, kwa hiyo inapotokezea hayo na wananchi waliokuwa wameajiriwa wakajua kwamba kuna uwazi na kuna uajibikaji katika nchi. Hivyo kila mmoja

atafuata mkondo wake. Lakini pale inapobainika kwamba ubinafsi unatawala sheria hii itakuwa ni ndoto ya kutekelezeka.

Mhe. Spika, jengine ni kwamba lilitaja siku ile kwa njia ya lugha ya Kiingereza wataalamu wenyewe wanaita *appraisal* ya wafanyakazi. Mhe. Spika, hii namuomba Mhe. Waziri ikiwa sheria haikusema hivyo moja kwa moja basi atakapotunga kanuni ahakikishe inapatikana *appraisal* ya wafanyakazi tena kila mwaka. Kwa nini Mheshimiwa nasema hivyo? Kwa sababu mfanyakazi yeyote atakayeandikiwa ripoti yake kila mwaka na ikawekwa rekodi basi inazuia wakati wa kupandishwa cheo mtu mwengine kutumia madaraka yake ama kwa kumpandisha ambaye asingestahiki au kwa kumnyima yule ambaye anastahiki. Kwa sababu rekodi zake zitakuwa zipo na yeye mwenyewe amepewa kopi, lakini kwa kukaa tu ndio maana Mhe. Spika, mimi nikalipigia kelele sana suala la uteuzi wa Urais kwa sababu unakaa wee katika ngazi mpaka upate nafasi Rais akuteua ndio ujulikane kwamba wewe umepata *promotion*.

Hii imewezekana wakati ule wa uteuzi wa Rais ndio wakati ule watu wanatumia fursa ya kuwapeleka wale ambao wangewahitaji, lakini kama upo utaratibu wa kuhakikisha kuwa kila mwaka mfanyakazi anaekewa rekodi zake basi hakuna haja yakusema niletee fulani na fulani kwa sababu yale majina yapo. Kwa hivyo, huu utaratibu wa utumishi wa umma kama hakuna *job appraisal* ya kila mwaka tutaendelea kusema kwamba huyu kachaguliwa huyu hafai, huyu hivi…

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe naomba radhi tena kikao tuahirishe kwa muda mpaka umeme utakaporudi.

(Saa 11:15 jioni Baraza liliahirishwa)

(Saa 11:31 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe hali inatufundisha jambo tena jambo lenyewe anaambiwa Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais pamoja na Mhe. Waziri wa Fedha kwamba ingefaa sasa kutafuta *generator* ambalo litakuwa na uwezo mkubwa wa kukidhi haja ya hapo na shughuli zetu. Kwa hivyo, hali halisi ndio hiyo nadhani tujipange ili tuwatafutie vijana wetu hilo *generator*.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, ahsante sana naomba dua usizimwe tena. Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu napenda niseme kwamba kifungu Nam. 6 na kifungu Nam. 10 zinapingana. Kwa hivyo, ni dhahiri

kwamba kifungu Nam. 6 hakiwezi ku-*prevail* kwa sababu kifungu Nam. 10 kinaeleza utumishi wa umma Zanzibar utaundwa na tumishi zifuatazo:-

Kutakuwa na utumishi serikalini utasimamiwa na Tume ya Utumishi Serikalini Utumishi wa Mahakama utakaosimamiwa na Tume ya Utumishi ya Mahakama Utumishi wa Baraza utakaosimamiwa na Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, tukisema kwamba katika kifungu Nam. 6 utumishi wa umma utakuwa na uhusiano na utumishi wa kisiasa katika kanuni za maadili na sera za malipo zinapingana kwa sababu huku Baraza la Wawakilishi lishaekewa Tume ya Utumishi, huku Tume ya Serikali ishaekewa tume yao kwa hiyo zina uhusiano vipi na hayo ni *autonomous boardies*. Kwa hivyo, hivi vifungu vinapingana kile ambacho kina-*privail* ni kile ambacho kiko sahihi kwamba ilivyokuwa hii ni *autonomous* kifungu Nam. 6 moja kwa moja kinakuwa mbali ya yale maelezo niliyoyaeleza ya jumla ya ulimwengu lakini hata katika hii sheria wenyewe inasema hivyo.

Mhe. Spika, mimi nasema haya si kwa sababu yakupendelea kwamba hii nafasi niliyonayo kama mwakilishi, nasema haya kwa sababu tumekubali kwamba kuna mihimili mitatu ya dola. Wakati wote tuangalie kwamba muhimili mmoja hauelemei muhimili mwengine na ukaufuta, kwa sababu yote mitatu inatakiwa iende sambamba.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu naomba nimtanabahishe Mhe. Waziri matatizo matatu makubwa yanayotukweza katika utumishi wa umma katika kipindi kilichopita. Mhe. Spika, naomba ikiwa sheria haikuzungumza hivyo basi kanuni zitakapotengenezwa ziyaone mambo haya.

Mhe. Spika, kwanza nafasi ya kukaimu katika sheria zilizopita au kanuni zilizopita nafasi ya kukaimu ilitarajiwa isizidi miezi sita, lakini nafasi hiyo imekuwa ikiburuzwa na yule aliyekaimu kwa zaidi ya mwaka mmoja inapokuja nafasi kamili hapewi tena yule anapewa mtu mwengine kabisa. Hii nafasi ya kukaimu imekuwa ikitumika vibaya katika suala la utumishi wa umma.

Mhe. Spika, tunazo taasisi za umma au mashirika muda mwingi Bodi ya Wakurugenzi huwa haiko kwa wakati wake au unapomaliza muda inakuwa muda mrefu unapita bila ya kuwa na Bodi ya Wakurugenzi jambo ambalo inakuwa ni kinyume na utaratibu wa uendeshaji wa taasisi zile. Kwa hivyo, nafikiri kwamba sheria sasa ingechukua mkondo wake kuhakikisha kwamba kabla ya bodi haijamaliza muda wake utaratibu wa kutayarisha bodi nyengine unapatikana ili mara tu bodi ikimaliza muda wake Bodi ya Wakurugenzi mpya inapatikana.

Mhe. Spika, suala la tatu ambalo lilijitokeza katika utumishi wa umma ni suala la uzoefu katika kazi. Mhe. Spika, hapa mimi napenda nisisitize mambo mawili katika kada ya ualimu na kada ya hospitali kuwe na utaratibu wa *grade*. Mhe. Spika, kwa sababu mwalimu anaweza kuwa ni yule yule wa diploma au degree ya kwanza, lakini huyu ni mzoefu basi anaitwa mwalimu tu hakuna *grade* I, II na III kutokana na uzoefu wake alionao katika kazi. Ndio maana wakati ya kutayarisha *scheme of service* wizara inatayarisha hata ikishatayarisha kuna kesi zinafika 100 zinakwenda au 1000 kwa sababu hakukuwa na *grade* ya wale walimu. Mhe. Spika, katika uratibu ujao basi tubadilishe tuanze kabisa kutizama kwamba miaka mingapi anapanda *grade* inakuwa hakuna tena matatizo hayo. Nasema kada mbili hizi kwa sababu ndio zinazowaajiri watu wengi zaidi kuliko wizara yoyote katika Zanzibar.

Mhe. Spika, la mwisho nizungumzie kuhusu suala la uzoefu wa kazi. Mhe. Spika, katika baadhi ya mawizara ya wenzetu hata kama kuna maongezeko ya taaluma ya kiasi gani, lakini mkuu wa kitengo mara nyingi anakuwa ni mtu mwenye umri zaidi kuliko wale watu wengine. Kwa hivyo, hii inaonesha kwamba ule uzoefu katika kazi una dhamana kamili. Kwa hivyo, hata kama huyu ana uzoefu wa juu kuliko mwengine lakini utaratibu upangwe kiasi cha kwamba wale wakuu wa vitengo katika mawizara au maidara wanachukuliwa kwa ile *seniority* yao ndio ule utaratibu wa kuheshimu kazi utakapokuja. Lakini inapokuwa mtu kafanya kazi miaka 20, 30 ana uzoefu kuna watu wakenda tu pale mtu keshajua huyu anakwendea nini katika ofisi, akifika tu huyu anamjua lakini unamuweka yule ghafla mambo yanaanza kubadilika pale katika ofisi. Kwa hivyo, suala hili litizamwe kwa uangalifu sana.

Mhe. Spika, mwisho kabisa naomba niunge mkono hoja lakini kwa ombi langu lile nililosema kwamba baada ya miaka miwili wizara hii kwa sababu ilikiri kwamba mswada umekuja ghafla, haukutimiza masharti yake lakini wanasheria wakautetea kwa hivyo baada ya miaka miwili tukijaaliwa uletwe tena katika Baraza. Wakati huo na sisi tunaufanyia kazi kwa kupitia wanasheria mbali mbali kuangalia ni kitu gani kilichopungua na kitu gani kilichoongezeka. Kwa sababu tunaitaka Zanzibar huu utumishi serikalini ndio roho ya serikali, huwezi kuwa na utaratibu mzuri serikalini bila ya kuwa na roho na serikali.

Mhe. Spika, lakini Mhe. Waziri ana wajibu wa kutayarisha *code of conduct* ya kazi baada ya sheria hii ili ajulikane kila mmoja na kazi yake. Mhe. Spika, baada ya hayo naomba niunge mkono hoja na niitakie kila kazi njema wizara hii mpya ambayo ingeweza kutuoneshea dalili ya mafanikio katika nchi yetu.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi kueleza chochote kuhusu mswada huu uliopo mbele yetu. Mhe. Spika, kwanza

napenda niipongeze serikali kwa kuweza kuleta mswada huu ambao unahusiana na utumishi wa umma jambo ambalo kwa kipindi cha miaka mingi sana limekosekana katika nchi yetu.

Mhe. Spika, huu ni mswada mzuri na kwa kiasi kikubwa kwa sababu asilimia zaidi ya 40 ya Wazanzibari ni wadau wa utumishi serikalini naamini utaondoa manung'uniko na kwa kiasi fulani hawa wenzetu wa *executive* itakuwa rahisi kuwatawala. Mhe. Spika, pamoja na uzuri wa mswada huu lakini kuna mapungufu madogo madogo yaliyojitokeza.

Mhe. Spika, kwanza ni vyema sheria zetu zikaendana na hali ya ulimwengu ilivyo sasa, sasa hivi ulimwengu mzima tunazungumzia suala la demokrasia na utawala bora. Mhe. Spika, unapoleta kizuri kama hiki bila ya kuwashirikisha wadau kwa maana ya waajiri pamoja na watumishi kwa kweli kwa kiasi fulani umekiuka ile dhana ya demokrasia na utawala bora, umeikiuka katika misingi miwili.

Kwanza kisiasa, kisiasa linapokaa jopo la wataalamu wakatayarisha kitu kama hiki bila ya kuwashirikisha wadau ni kwamba huku-*decentralize* demokrasi. Kwa hivyo, zile *inputs* za wale wadau zimekosekana. Kwa hivyo, Mhe. Spika, ni matarajio yangu kwanza serikali itakapoleta kitu kama hiki kwa mara nyengine itakwenda kwa watu ili mawazo ya watu yawemo, hii itatusaidia sana kuweza kupata mawazo ya wenyewe kuliko wataalamu kuwateremshea tu watu.

Mhe. Spika, jengine kuhusu huu mswada kwa hali hiyo ni kwamba umekosa *democratic,* kwa sababu mawazo ya watu wa chini hayakuchukuliwa. Kwa hivyo, hii rasimu iliyoletwa ya huu mswada hapa kinachotafutwa sasa hivi ni uhalali wa kisheria tu, lakini wakati inakuja hapa imekosa uhalali wa kisiasa kwa sababu haikuwagusa wenyewe. Kwa msingi huo basi, ni kwamba zile kero za watumishi humu hazimo.

Kwa mfano, mswada huu haukueleza mambo ya msingi yanayowahusu watumishi kama vile mambo yanayohusu maslahi yao. Mambo yanayohusu maslahi ya watumishi kwa kiasi kikubwa mswada huu umeyapa mgongo. Kwa sababu tunazungumzia suala la utawala bora na demokrasia nilidhani mswada huu ungeweka pahala pa watumishi wa serikali kutolea pumzi, wasiwe hawana pahala pa kutolea pumzi, wangeruhusu kuwemo kwa mambo ya migomo kama migomo halali pale wanapokosa maslahi yao, wangekaa na vyombo vinavyohusika na utumishi kujadili maslahi yao.

Lakini haya hayakuzungumzwa Mhe. Spika. Kwa hivyo, ni matarajio yangu kwamba Mhe. Waziri haya atayaona, kwamba pamoja na mapungufu mengine

mswada huu umezipa mgongo zile kero zinazowagusa watumishi. Kwa mfano haki ya kufanya majadiliano kuhusu maslahi yao pengine na hizi bodi za utumishi hakuna vipengele vinavyoruhusu hawa watumishi kufanya majadiliano na viongozi wao kuhusiana na mambo yanayohusu maslahi.

Aidha, pale linapotokea tatizo la migongano na viongozi wao vile vile hatukuona kwamba wanaweza kuandaa migomo halali ili kuonesha hisia zao katika kero wanazozipata. Kwa hivyo, hilo ni moja Mhe. Spika.

Mhe. Spika, katika mswada huu kuna utitiri wa vyombo vinavyohusiana na watumishi. Kwa msingi huo ni kwamba ufanisi wa kazi unaweza ukakosekana na uajibikaji vile vile unawezekana usiwe na ufanisi. Kwa sababu vyombo ni vingi hivi vinavyosimamia. Kwa hivyo, nadhani vyombo hivi vingepungua ikawa kuna chombo madhubuti kinachosimamia ufanisi katika suala hilo.

Kwa mfano, katika wizara husika, bodi za utumishi, kamisheni ya utumishi, na kadhalika, tunaona vyombo ni vingi sana Mhe. Spika, hivyo ufanisi unaweza ukakosekana. Haya ni mapungufu mengine.

Sasa Mhe. Spika, nadhani niende moja kwa moja katika kifungu nambari 14 kuhusiana na uteuzi na majukumu ya Katibu Mkuu Kiongozi. Kwa kweli Mhe. Spika, Katibu Mkuu Kiongozi amepewa uwezo mkubwa, uwezo huu nadhani ungepwa taasisi kuliko mtu mmoja. Unapotoa uwezo mkubwa kama huu mara nyingi Mhe. Spika, huandamana na ukandamizaji, unapompa mtu binafsi. Lakini ingekuwa wamepewa taasisi basi nadhani tungelikuwa na kubadilishana mawazo ndani ya taasisi yakapatikana maamuzi yaliyokuwa hayana ukandamizaji. Kwa hivyo, naomba Mhe. Spika, katika hili liangaliwe sana.

Vile vile tukiangalia katika kifungu cha 14(5) huyu bwana uwezo aliopewa unaweza ukasababisha matatizo katika nchi ikiwa hatukuangalia. Kwa mfano, katibu huyo kapewa uwezo wa kuwasimamisha pamoja na kuwafukuza kazi watendaji wakuu. Napata wasi wasi kwamba kuna siku akiwa yeye hayupo anaweza kaja akamfukuza kazi Kamanda wa Vikosi vya KMKMK au JKU yakaja yakawa mashaka hapa. Nadhani mambo haya ayafanye rais mwenyewe na kwa sababu mswada huu ukipita kama ulivyo sasa Mhe. Spika, ina maana na sisi wanasiasa tunaingia katika kundi la watumishi. Napata wasi wasi siku moja huyu bwana Katibu akija kwenda katika Jimbo la Makunduchi akamfukuza Mwakilishi jambo ambalo watu wa Makunduchi hawatokubali.

Napata wasi wasi vile vile kuna siku anaweza akaja akatufukuzia Spika wetu humu hatutokubali vile vile. Kwa hivyo, haya mamlaka ni makubwa kupewa mtu ni vyema ingepewa taasisi.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, kama yatafanywa mabadiliko hayo niliyoyataja nitaunga mkono hoja ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa na mimi nichangie maneno mawili matatu katika mswada huu. Mhe. Spika, mimi kwanza namshukuru sana Mhe. Waziri kutuletea mswada huu kwa ajili ya kuwawekea mazingira mazuri watumishi. Lakini bado mimi naendelea kutoa wasi wasi wangu kuhusu Katibu Mkuu Kiongozi kama nilivyozungumza kwenye semina na leo bado naendelea kutoa mchango au maoni yangu.

Mhe. Spika, kwa kweli mimi sipingani na viongozi wetu wa ngazi za juu kulindiwa heshima na kujaliwa kwa maslahi yao pale ambapo wamestaafu. Lakini nililozungumza mimi ni hili ninaloendelea kulizungumza tena. Mhe. Spika, Katibu Mkuu Kiongozi au kiongozi yoyote yle wa ngazi ya juu anapostaafu ni wajibu kuangaliwa kimaslahi, lakini ninalosema mimi ni kwamba, mtu anapokuwa tayari keshastaafu kazi basi asilipwe mshahara ule ule aliokuwa akilipwa. Sasa kama yeye alikuwa akilipwa mfano shilingi laki sita lakini sasa keshastaafu kazi alipwe tena zile zile laki sita itakuwa kastaafu nini. Mimi huwa najiuliza sana atakuwa kastaafu nini na bado itakuwa mshahara wake ni ule ule kapumzika kufanya hiyo kazi tu, lakini mshahara uko pale pale.

Mhe. Spika, ninavyozungumza sisi tunaweza tukawa na makatibu viongozi ambao tayari wameshastaafu kama wanne au watano kwa mfano, lakini mshahara wao bado uko pale pale, basi na mimi bora niwe katibu mkuu kiongozi mstaafu nipumzike nyumbani halafu nipewe pesa hizo hizo. Kwa hivyo, Mhe. Spika, bado nasema mtu anapostaafu angalau apewe nusu ya mshahara sio apewe pesa zile zile. Kwa sababu kama atapewa pesa zile zile kastaafu nini? Mhe. Spika, nasema bado maoni yangu mimi apunguziwe, ni kweli tuwaenzi, tuwaheshimu, lakini apunguziwe mshahara wake asipewe ule ule.

Suala jengine ni kwamba naomba na mimi niungane na wenzangu kwamba mswada huu kidogo uwape nafasi wafanyakazi, endapo maslahi yao wataona kidogo yamebanwa basi waweze kufanya mgomo kwa ajili ya kudai maslahi yao. Lakini ikiwa hawana nafasi haya ya kugoma basi serikali itafanya hivyo hivyo inavyotaka, lakini kidogo ikiwa na wao wana nafasi basi serikali yenyewe itajua kwamba hapa tukienda hivi kidogo wafanyakazi wanaweza wakagoma na ikawa hatari.

Kwa hivyo, wapewe nafasi serikali isiwabane, wapewe nafasi wajitanue kidogo ili na wao wakiona maslahi yao yamebanwa waweze kugoma kidogo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri hili aliangalie na awape nafasi.

Mhe. Spika, mimi naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja lakini. *Concern* yangu ilikuwa ni hiyo. Ahsante sana.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Spika, nami nichukue nafasi jioni hii kutoa maoni yangu juu ya mswada huu ulioko mbele yetu. Mswada huu pindi ukipita kuwa sheria itakuwa tumesogea mbele kidogo. Kwa sababu hivi sasa hakuna sheria maalum ya utumishi serikalini. Wafanyakazi wanakwenda kazini kwa mujibu wanavyojua wenyewe, wanaingia wakati wanaotaka na kutoka wakati wanaotaka, wanakwenda harusini bila ya ruhusa na mambo mengineyo. Kwa sababu labda hakuna sheria maalum ya kazi iliyowekwa.

Kwa hivyo, hapa itakuwa ile nidhamu ya kazi imepotea na kazi bila nidhamu kwa kweli hapana kazi. Sasa hapa pametajwa nidhamu ya watumishi wa umma na pia wamepangiwa adhabu mbali mbali pale ambapo wamechelewa au hawakwenda kabisa kazini. Lakini unapompangia mtumishi adhabu na umemuwekea wakati maalum kuwa wakati huu uwe umefika kazini. Je, umemuwezesha kufika hapo kazini kwa wakati?

Tujaalie mtu mwalimu nichukulie kule ninakokujua mimi anakaa Kengeja anafanya kazi Skuli ya Mizingani, anatakiwa saa moja na nusu awe ameshafika kazini. Je, umemuwezesha kufika kazini kwa wakati huo hata ifike pahala umuadhibu kwa sababu kachelewa? Kwa hivyo, ili wafanyakazi wafike mapema kazini lazima wawezeshwe namna ya kufika mapema, tusiwapangie adhabu wakati ambapo hatujawawekea utaratibu wa kufika kazini mapema. Kwa sababu kufika kazini na kufanya kazi ni wajibu lakini na muajiri awawezeshe kufika kazini hapo.

Sasa nije kwenye sehemu ya sita kunakozungumzia viwango vya kazi na mahusiano ya kazini. Hapa naomba kidogo ninukuu hii sentensi inasema kwamba, “Kaibu Mkuu Kiongozi, Katibu Mkuu, Waku wa Idara au taasisi watachukua hatua ambazo ni muhimu kuhakikisha kwamba mazingira ya kazi yako salama, yanafaa na hayahatarishi usalama wa afya wa waajiriwa na kwa mujibu wa sheria ya afya na usalama kazini”.

Mhe. Spika, wafanyakazi wetu wengi wanafanya kazi katika mazingira magumu ambapo hata usalama wao wa kiafya haupo. Nichukulie mwalimu ambapo skuli zetu nyingi bado zinakwenda kwenye *chalk and talk*, anaandika akifuta, vumbi puani, vumbi mdomoni. Je, afya yake huyu tumeiweka wapi? Hakuna siku anayoangaliwa afya yake, akienda kazini na chaki yake mkobani aliyonunua basi, tunaifikiria vipi afya ya mfanyakazi huyo.

Kwa hivyo, ni lazima tuweke mazingira ya kila wakati kuangalia afya za wafanyakazi wetu, vyenginevyo tutakuwa na wafanyakazi ambao afya zao haziridhishi.

Daktari anapofanya operesheni anajifunga kitambaa mdomoni na puani nadhani kuzuia viambukizi fulani, sina taaluma ya udaktari. Lakini je, *orderly* ambaye anafagia vyoo na mwenginemo ana kinga gani kazini pake pale? Kwa hivyo, kila sehemu lazima tuitafutie usakama wa afya za wafanyakazi wetu.

Kwenye utengenezaji wa barabara siku hizi barabara zetu zinatengenezwa kwa fusi, gari inapopita mwenye rangi kama yangu anakuwa kama nywele zangu au ndevu zangu zinavyoonekana. Vumbi lile halimalizii mwilini tu, lakini linamalizia na puani, mdomoni, ambapo wakivuta pumzi linakwenda ndani. Hapa kwa kweli usalama wa wafanyakazi na raia wetu bado haujazingatiwa katika masuala yetu mbali mbali. Ni vyema basi, tumeleta mswada huu pindi ikiwa sheria naomba yote yale yaliyoingizwa humu yaweze kuchukuliwa hatua kikamilifu.

Wafanyakazi walio wengi maslahi yao yako duni sana, mapato yao hayalingani na kazi wanazozifanya. Tulipofika sio ule wakati wa kuwa fanya kazi baadae muda uliobaki ukafanye kazi nyengine. Mhe. Spika, mfanyakazi anatakiwa kazi anayofanya imuendeshe. Mwalimu aendeshwe na ualimu wake, daktari aendeshwe na udaktari wake isiwe lazima kuwa akitoka kazini akatafute kazi nyengine ndio maslahi yake yakamilike. Lakini afanye hivyo kwa hiari yake lakini isiwe kwa kutimiza sehemu ya maisha yake, kufanya hivyo ndio maana wafanyakazi wetu wanakuwa katika harakati kama nyuki katika mzinga wao, hawapumziki saa zote wako kazini, ufanisi wa kazi katika maafisi na maidara unakosekana.

Kwa hivyo, tuwawezeshe wafanyakazi waweze kufanya kazi za serikali au katika ajira zao ili ufanisi serikalini upatikane. Hali tunayokwendanayo sasa ya mtumishi mmoja kufanya kazi zaidi ya mbili kwa kweli ni tatizo, haidhuru anapata mapato lakini ni tatizo. Kwa sababu hana wakati wa kupumzika, nikitoa mifano zaidi nitatoa kwa walimu kwa sababu ni miongoni mwa watu ninaowajua kuwa wana kazi ngumu.

Mwalimu ana kazi nyingi, awahudumie wanafunzi wengi hata kama wakitoka anatakiwa kazi ya leo aimalize, lakini maisha kama hukumuwezesha anakwenda kwenye kazi nyengine, usiku alale asubuhi anakwenda kazini. Kwa kweli hali hii si nzuri. Mhe. Waziri ningeomba maslahi ya wafanyakazi yapewe kipaumbele na aliyetangulia na watu wenye sifa moja za elimu kwa kweli viwango vyao vya pesa vilingane, wa leo na wa kesho watafautiane.

Kuna wafanyakazi wa sekta mbali mbali wao maisha wanaanguka katika kima cha chini cha mshahara. Hii inatokana kwa sababu hakuna ile nyongeza ya kila mwaka ya mshahara. Tunangojea ile pengine ongezeko la Mhe. Rais la kuongeza mishahara tunakwenda pamoja. Sasa hii haileti tofauti baina ya mtu aliyeingia mwanzo na aliyekuja baadae. Sheria hii naomba izingatie hilo ili wale waliofanya kazi zamani wasivunjike moyo na kufanya kazi. Kuna watu wanashindwa kwa mapato na wajukuu wao kikazi sio watoto wao ni wajukuu wao.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo machache naomba niunge mkono mswada huu. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii nami niweze kutoa mchango wangu katika mswada huu wa sheria.

Mhe. Spika, napenda pia nimpongeze sana Mhe. Rais kwa kuanzisha Wizara hii ya Utumishi na Utawala Bora, kwa sababu ilikuwa kilio kikubwa cha Wazanzibari. Aidha, nimpongeze sana Mhe. Waziri na watendaji wake kwa kazi nzuri ambayo imemsaidia sana waziri kuweza kuwasilisha mswada huu mzuri kwa ajili ya maslahi ya wafanyakazi wetu.

Mhe. Spika, nilikuwa nikiwasikiliza kwa makini Waheshimiwa Wajumbe kwa namna walivyokuwa na imani kubwa juu ya wafanyakazi wetu. Nia yao ni kuhakikisha kwamba wafanyakazi wetu wanapata maslahi yaliyobora zaidi na wanatetewa haki zao ili waweze kumudu kufanya kazi zao vizuri zaidi. Hiyo ndio nia ya serikali kuhakikisha kwamba maslahi ya wafanyakazi yanalindwa. Kwa hivyo, niseme kwamba, Waheshimiwa Wajumbe na serikali inazungumzia neno moja au lugha moja katika kutetea maslahi ya wafanyakazi wetu.

Yamekuwepo malalamiko kuhusu mfumo wa mishahara, ushirikishwaji wa wafanyakazi na waajiri, kuwa na kanuni zilizo bora, ukosefu wa vitendea kazi, wataalamu kupangiwa kazi nje ya taaluma zao na masuala mengine mengi.

Mhe. Spika, nia ya serikali katika kuanzisha wizara hii ni katika kushughulikia matatizo hayo. Mwanzo umekuwa mzuri wa serikali kwamba ili uweze kushughulikia vizuri lazima tuwe na sheria. Kwa sababu sheria hii Mhe. Spika, naweza kusema ni mtoto aliyezaliwa kutokana na sera ya utumishi na mageuzi ya watumishi wa umma. Kwa kweli sera ile na mageuzi ya watumishi wa umma yalishirikisha sana wadau na mengi yaliyomo katika sheria hii yanatokana na maoni na ushauri uliotokana na wadau.

Kwa hivyo, serikali ilivyokuja na sheria hii ilidhani yale maoni yaliyotokana na sera na mageuzi ya watumishi wa umma yanakidhi haja ya kuanzisha sheria, lakini leo tumeyaona malalamiko mengi kidogo yakihusiana na kwamba ushirikishwaji wa watumishi kama wadau muhimu wa sheria hii haukuwa wa kutosheleza.

Mhe. Spika, nia ya serikali ni kusikiliza maoni ya wawakilishi wetu, kusikiliza maoni ya wafanyakazi wetu. Mhe. Waziri kwa kiasi kikubwa sana katika hotuba yake ya leo alipokuwa akiwasilisha hivi asubuhi, yale mengi ambayo yalikuwa ni malalamiko ya wafanyakazi na waheshimiwa wawakilishi waliyozungumzia hapa yamechukuliwa katika sheria hii.

Kitu cha msingi hapa Mhe. Spika, ni kuanza utekelezaji wa sheria hii. Katika ku-*practice* sheria yako mambo yatakayojitokeza ya mapungufu na siku zote sheria si msahafu. Kwa hivyo, hatua kwa hatua zinazojitokeza tutafanya mabadiliko ili iendane na hali halisi. Lakini kwa sasa ni jambo zuri sana Waheshimiwa Wawakilishi kuipitisha sheria hii na kuanza shughuli zake ili ziweze kuwasaidia wafanyakazi na kujenga mazingira yaliyo bora zaidi kwa watumishi wetu wa umma. Na mimi nichukue fursa hii kuwapongeza sana watumishi wetu wa umma kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kutumikia taifa lao.

Mhe. Spika, nimemsikia hapa rafikiri yangu Mhe. Subeit Khamis Faki akilalamikia sana kuhusu maslahi ya kustaafu ya Katibu Mkuu Kiongozi. Kwanza lazima tukubali ukubwa wa majukumu ya Katibu Mkuu Kiongozi. Mhe. Spika, katiba yetu kifungu cha 49(2) kinamtambua Katibu Mkuu Kiongozi kama ndiye kiongozi mkuu wa utumishi wa umma. Ikiwa Mhe. Spika, kupata mshahara wake anavyopata leo baada ya kustaafu sioni kama ni jambo baya. Kwa sababu ikumbukwe kwamba ni mshahara sio marupurupu mengine na mishahara yetu sote tunaijua kiasi chenyewe. Mtu kama yeye anapotoka katika uongozi huku akisema kweli kazi za aina ile zina lawama nyingi inamshinda hata kwenda dukani kwa mtu kukopa katika kumaliza muda wake.

Kwa hivyo mimi naamini kwamba hiki kiwango alichotengewa ni kiwango ambacho kingemsaidia sana na kuweza kumhamasisha kuweza kutenda wajibu wake vizuri zaidi, kwa hivyo hii tungeomba Waheshimiwa Wawakilishi waone kwamba mwenzetu huyu, au wenzetu hawa wanaopata fursa ya kulitumikia tafia katika nafasi hiyo ni kubwa basi na sisi ni vyema tukawatizama kwa maslahi ya namna hii.

Mhe. Spika, nia ya serikali yetu ni kuangalia maslahi ya wafanya kazi wote tatizo letu kubwa ni hali yetu ya uchumi, ndio mtihani ulio mbele yetu lakini naamini Mhe. Spika, ka hatua ambayo Zanzibar imefikia hivi sasa niseme

kweli tulikuwa na matatizo makubwa ya kisiasa, lakini baada ya maridhiano tukawa na umoja wa kitaifa. Sasa naamini matatizo ya kisiasa yameondoka na mazingira haya yatavutia sana kujenga uchumi wan chi yetu, kwa hivyo naamini uchumi wetu utaimarika na kuwa katika hali nzuri zaidi kadri ya uchumi utakavyoimarika ndivyo tutakavyoweza kuwahudumia watumishi wetu vizuri zaidi.

Mhe. Spika, serikali nia yake kubwa ni kuwahudumia wafanyakazi wetu hakuna nia ya kukandamiza wafanyakazi wetu lakini hali halisi ya uchumi ndio iliyotufikisha hapa, sasa kwa mazingira haya naamini hali itakuwa nzuri na wafanyakazi wetu wote watakuwa katika hali nzuri zaidi.

Mhe. Spika, baada ya hayo niwaombe sana sana wawakilishi wenzangu tuipitishe sheria hii ili itusaidie katika kujenga mazingira mazuri ya kuufanyia kazi uchumi wetu. Mhe. Spika, baada ya hayo naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia mswada uliopo mbele yetu. Kwa kawaida Mhe. Spika, tungetosheka na maelezo yaliyotolewa na Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, lakini kutokana na hoja za wajumbe nyingi zilizochangiwa hapa nimeona na mimi kuna haja ya kuchangia ili kuzidi kusaidiana kuelewa hata yale ambayo yalipita katika kamati katika kuujadili mswada huu.

Mhe. Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dk. Ali Moh'd Shein kwa hatua ya kuanzisha wizara katika ofisi yake inayosimamia Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Hii ni hatua muhimu na kwa muda mrefu sana ilikuwa imekosekana wizara ambayo ingeweza kusimamia moja kwa moja masuala haya.

Lakini pili matokeo ya kuanzishwa kwa wizara katika ofisi hiyo ni leo hii kwamba tunajadili mswada huu wa Sheria ya Kuweka Miundo, Uendeshaji na Usimamizi wa Utumishi wa Umma Zanzibar. Kwa hivyo, naipongeza sana wizara kwa hatua hii iliyotufikisha hapa leo katika historia ya Zanzibar.

Mhe. Spika, pia nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Waziri na wasaidizi wake wote ambao katika kamati alionesha utayari wa kukubali hoja mbadala ili kuufanya mswada uwe mzuri kama unavyoonekana baada ya kuwasilishwa hapo mbele.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, niseme kwamba sote tumepata nafasi ya kusikiliza malalamiko ya washiriki wengine katika masuala haya hasa Vyama vya Wafanyakazi. Binafsi nilibahatika kupata nakala ya maoni ya Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Zanzibar na kamati yetu ililetewa.

Mhe. Spika, naomba kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba mapendekezo haya yaliyotolewa na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi yalizingatiwa katika kamati na ndio maana utaona mapendekezo ya kamati yamekuja yakiwa katika karatasi nyingi kama hivi yalivyo. Kwa sababu yamezingatia maoni ya Vyama vya Wafanyakazi lakini pia *concerns* nyingi ambazo zimeelezwa hapa za wajumbe mbali mbali.

Kwa hiyo Mhe. Spika, nataka niwatoe wasi wasi wajumbe kwamba haya mengi tunayoyajadili tukiutazama vizuri mswada katika *version* mpya tuliyoletewa baada ya kupita katika kamati tutaona mengi haya yamefanyiwa marekebisho.

Mhe. Spika, kwa mfano Vyama vya Wafanyakazi katika maoni yao waliyoyatoa wamelalamika kwamba kutokutambuliwa kwa majadiliano ya pamoja. Lakini tukiuangalia mswada huu Mhe. Spika, hasa baada ya marekebisho kifungu cha 80 (2) kinataja kuwepo kwa majadiliano ya pamoja. Vile vile kifungu cha 94 (3) kinatambua suala hili.

Lakini kinatambua pia uwezekano wa kuwepo makubaliano ya pamoja yanayotokana na majadiliano ya pamoja, tukijua kwamba haya yanafanywa kupitia vyama vya wafanyakazi. Mswada huu umelizingatia hilo lakini mbali ya hayo Mhe. Spika, kifungu cha 80 (2) katika kanuni ambazo zitawekwa na Waziri ambazo kwa Kiingereza zimetafsiriwa kwamba ni *public service, labour relation*, sio zile kanuni za kawaida tu hizi. Pia inazungumzia pale muajiriwa au vyama vya wafanyakazi watawasilisha malalamiko yao katika sehemu zao za kazi. Kwa hivyo, nasema suala hili limezingatiwa.

Lakini hata hilo jengine ambalo limetajwa la migomo sisi kamati yetu imepitia kwa kina mswada huu, hakuna pahala popote ambapo mswada umezuia mgomo na migomo inaongozwa na sheria nyengine za kazi zinazolinda haki hiyo. Sasa mswada huu haukupini matatizo na ingekuwa una matatizo ungekuwa umezuia haki yetu, lakini hapana pahala popote na tumeupitia kwa kina kabisa katika kamati yetu. Hilo pia nilitaka Baraza lako nilieleze.

Lakini pia suala jengine lililozungumzwa hapa ni uhusiano mwema sehemu za kazi. Mhe. Spika, sehemu nzima ya sita mswada huu unazungumzia viwango vya kazi na mahusiano kazini, *labour relation* zimezingatiwa. Kwa hivyo, nasema haya mengi ambayo yametajwa katika mswada huu tumeyazingatia

katika kamati na ndio maana mswada umekuja katika hali hii ambayo tumeuona hapa leo.

Lakini kwa upande mwengine Mhe. Spika, hata haya madaraka ambayo yanalalamikiwa kwamba kulikuwa na madaraka mengi, ni kweli ukitazama mswada ulivyokuwa mwanzo ulikuwa ugawike madaraka mengi sana kwa Katibu Mkuu Kiongozi. Lakini kupitia katika kamati imefanya kazi kubwa sana ya kuweka uwiano mzuri baina ya Waziri, baina ya Wizara, baina ya Kamisheni ya Utumishi wa Umma na baina ya Katibu Mkuu Kiongozi. Kwa hivyo, hilo limezingatiwa sana nawaomba Waheshimiwa Wajumbe waliangalie vizuri kwenye huu waraka wa kamati ambao umefanya marekebisho makubwa.

Lakini jengine vile vile hata kwa hili lililokuwa likitiliwa wasi wasi kwa mgawanyo wa madaraka baina ya mamlaka tatu kubwa katika nchi, mamlaka ya utendaji kwa maana ya serikali, mamlaka ya kutunga sheria na mamlka ya utoaji haki yamezingatiwa. Ndio maana katika kifungu cha nne kuna misingi mikuu ya utumishi wa umma ikaondolewa ile dhana nzima ya kuwepo wajibu wa kutumikia serikali, tukasema mamlaka ya kuitumikia nchi kwa maana ya kwamba kila mmoja aliyekuwemo katika utumishi atatumikia mamlaka yake anayofanyia kazi. Mbali ya kuzingatia kwamba hata katika kuundwa ile Kamisheni ya Utumishi wa Umma, pamezingatiwa kwamba wajumbe watatokana na mapendekezo yatakayotoka kwa Spika kwa upande wa watumishi wa Baraza la Wawakilishi kwa sababu wamo mle. Itatoka kwa Jaji Mkuu kwa sababu wamo kutoka Mahakamani na wajumbe wawili kutoka serikalini kwa upande wa utumishi wa serikalini.

Kwa hivyo, nasema kumefanyika uwiano mzuri sasa baada ya kazi ambayo ilifanywa kupitia kwenye Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

Mhe. Spika, jengine ambalo limelalamikiwa ni vyama vya wafanyakazi na kwenye kikao hiki tukalisema ili wakajua kwamba wawakilishi wa wananchi wao ikiwa ni sehemu yao wamezingatia. Lile la kusema kwamba mswada unaonekana unawapendelea baadhi ya watu na tukatolewa mfano kifungu cha 14 (4) kutaka kwamba Katibu Mkuu Kiongozi lazima awe miongoni mwa Makatibu Wakuu au mtu mwengine mwenye nafasi za juu.

Mhe. Spika, huu ndio utaratibu katika ulimwengu kwamba huyu Katibu Mkuu Kiongozi hawezi kuwa mtu yeyote tu ni mtu ambaye amegonga wadhifa fulani baada ya kuwa Katibu Mkuu, au afisa wa ngazi za juu katika serikali. Kwa hivyo, nasema mambo mengine haya yanatupa shida.

Lakini nataka kusema kitu kimoja Mhe. Spika, nadhani tunapata shida na itakuwa sio sisi peke yetu. Katika nchi nyingi ambazo zinafuata mfumo kama

wetu ambao ni *mix system* na *presidential system* na *parliamentary system*, kwa kuwa katika mifumo ya *parliamentary system* ambayo ndio mifumo inayofuatwa na nchi nyingi za jumuiya ya madola hakuna Wizara ya Utumishi wa Umma. Mara nyingi inafanywa moja kwa moja na Waziri Mkuu na Waziri Mkuu anakuwa ndio Mkuu wa Serikali. Sasa kwa kuwa Katibu Mkuu Kiongozi anakuwa katika Afisi ya Waziri Mkuu inakuwa afisi ile ndio isimamie. Hakuna mgongano baina ya Katibu Mkuu Kiongozi kwa sababu ni sehemu yake Afisi ya Waziri Mkuu katika mfumo wa Jumuiya ya Madola.

Lakini nchi zetu hizi zinafuata mfumo ambao ni *mix system* kwa hivyo lazima utafute utaratibu wa kuweka sehemu ya madaraka ya sehemu moja wapo ya Katibu Mkuu Kiongozi, lakini bila ya kuathiri kwamba tunapata mfumo ulio rahisi wa madaraka kwa hivyo yale yatekelezwe na Waziri wake ambaye ni Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Anayeshughulikia Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Kwa hivyo, nataka niwatoe wasi wasi wajimbe kwamba hayo yamezingatiwa na kamati iliyopitia kwa kina na ikarekebisha. Baada ya kuwatoa wasi wasi sasa nataka kuwaambia mswada huu kwa maoni ya kamati baada ya marekebisho yaliyofanywa, kwamba ni mswada mzuri na sisi kama kamati tunaliomba Baraza hili kwamba waupitishe kwa nguvu moja, na iwe sasa ni chachu ya kuleta mabadiliko tunayoyahitaji katika nchi yetu katika dhana nzima ya utumishi wa umma.

Lakini pamoja na kuupitisha huko nilikuwa naneno machache ambayo ningependa kuyasema sio mapendekezo kwa sababu mapendekezo tumeyapitisha kwenye kamati na kiutaratibu umeshapita huu, lakini nataka kusema hasa kwa waziri ayazingatie haya na wale watakaopewa dhamana yote.

Mhe. Spika, kifungu cha 5(2)(c) cha sheria hii ukikitizama kimeweka dhana moja inawezekana tumeitizama juu juu, nayo ni kwamba inasema zaidi ya maadili hayo mtumishi atapaswa kufuata maadili ya umma yafuatayo, (c) inasema muundo wa utumishi wa umma wa Zanzibar utazingatia kwa kadiri itakavyowezekana mchanganyiko wa watu wa Zanzibar. Mhe. Spika, hili nilikuwa nataka kulizungumzia nawaomba wahusika walitizame kwa makini sana.

Mhe. Spika, kuna utaratibu umezoeleka katika nchi yetu kwamba kuna sehemu ya Wazanzibari wenye asili ya jamii fulani wamekuwa hawakubaliki baadhi ya kazi kwasababu tu ya kuonekana kwamba utiifu wao na uaminifu wao ni wa kutiliwa mashaka, labda niwe muwazi hasa katika vikosi vya ulinzi na usalama na kwa sababu nazungumzia serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar nitazungumzia idara maalum, haimo katika sheria lakini imekuwa ni *practice* na *practice* hii

imeingia hata katika taasisi za kusimia haki za binaadam katika nchi yetu. Katika ripoti ya kituo cha huruma za sheria Zanziabr ripoti ya mwaka 2006 imezungumzia suala tunaloliita kuwa ni ubaguzi katika utaratibu wa uendeshaji wa serikali yetu, inawezekana yalitoke matatizo fulani ya kihistoria huko nyuma na zaidi katika misuko suko ya kisiasa katika nchi yetu ikapelekea kuwa hivyo.

Lakini hili linaleta unyonge katika nchi hata kama ni mwanasheria katika ule utendaji *practice* inajenga dhana kwamba tunawagawia matabaka mawili, kuna ambao utiifu wao hautiliwi mashaka na kuna raia fulani wa jamii fulani hawa hawaaminiki kufanya kazi, kwa sababu ya sheria za utumishi wa umma na tukisema utumishi wa umma inakava maeneo yote, kuanzia utumishi serikalini, utumishi katika Baraza la Wawakilishi, Utumishi katika Mahakama na utumishi katika sehemu maalum, kwa sababu wametambua katika madai yao yanazingatiwa *by visite* ya *population* ya Zanzibar. Basi naomba pia katika utendaji na utekelezaji wa sheria hii hilo lizingatiwe, sawa sawa ili hii dhana ya umoja wa kitaifa ipenye mpaka ndani kabisa na kila mwananchi wa Zanzibar ajione kwamba ni sehemu ya nchi hii na anafaidi haki na fursa zote kama ambavyo wananchi wenzake wanazifaidi.

Jengine la jumla Mhe. Spika, nilitaka kuzungumzia vile vile suala zima ambalo liko nje kidogo lakini linawahusu watumishi, watu wakifikia umri wa kustaafu basi kuna haja ya kustaafu ili kutoa nafasi kwa wengine nao kupata nafasi ya kuajiriwa. Mhe. Spika, binaadam tuna sifa ya kuwa *dynamic* na kwa hivyo kila shughulil inayofanywa na binaadamu inakuwa na sifa ile ile ya *dynamic*. Tumeona katika muda mfupi tuliotembelea serikali katika taasisi ambazo zimo kwenye kamati yetu, katika baadhi ya Afisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambazo zimeajiri vijana wapya waliosoma na mawazo ya kileo wanaokwenda na wakati, tumeona mabadiliko makubwa ya utendaji.

Naomba nichukue nafasi hiyo hapa kuzitaja ambazo zimenifurahisha sana na naomba kuchukua nafasi hii kuzipongeza sana, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Afisi ya Mwendesha Mashataka *DPP*. Ukienda pale unaona tofauti huwezi kuamini ukiangalia afisi hizi na afisi nyengine zilizokuwemo kwenye serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kimoja nilichokiona ni vijana wengi walioajiriwa ambao wana mawazo ya kisasa kwa hivyo wanaleta yale mawazo yao ya mafunzo yao yanaingizwa serikalini na yanaleta mabadiliko.

Kwa hivyo nasema kweli tunaheshimu wazee wetu na hali ngumu ya maisha ipo kila mmoja anataka kubakia kazini, lakini na vijana wetu waliosoma wanataka kuajiriwa katika nchi hii hii, juzi tu Mhe. Waziri wa Fedha Uchumi na Maendeleo alitwambia hapa kwamba Zanzibar *private sector* haijakua. Kwa

hivyo bado watumishi wengi bado wanaendelea kutegemea ajira katika serikali, sasa hili lionekane pia na Kamisheni, Waziri na Katibu Mkuu Kiongozi na wote watakaosimamia kwamba mtu akishamaliza muda tumpe ruhusa apewe haki zake na wengine waingie katika utumishi wa umma na watuletee mabadiliko ambayo yanahitajika sana Zanzibar.

Lakini pamoja na hilo Mhe. Spika, hatuwezi kuwa- *intrest* kuja hawa ikiwa mafao yao bado yako katika hali ya chini, kwa hivyo nilikuwa naomba pia katika kusimamia haya kuwe na sehemu nzuri ya kuzungumzia *paplic service* basi pia litizamwe hili kwa jicho la rehema vile vile, tunaposema uchumi wetu unakua na pato la taifa linaongezeka, basi pia lionekane kwa wafanyakazi wetu kuwa tunawajali na kwamba kidogo kidogo tunachopata na wao maslahi yao yanaongezeka.

Mhe. Spika, huwezi kumleta daktari bingwa kama hujamlipa laki tatu katika nchi, kama akipata maslahi zaidi ataondoka tu ndio maumbile ya binaadam kwa hivyo vitu kama hivi tuvizingatie sana. Waingereza wana msemo wanasema ukijidai unanilipa na mimi nitajidai nafanya kazi, sasa mazungumzo mengi ndio ufanisi wa kazi unapungua kwa sababu hawafanyi kazi kwa upeo wa uwezo wao kwa sababu ule motisha unaondoka. Wanatambua hali ya nchi yetu kama walivyosema mawaziri hapa lakini nasema hilo ni vizuri tukalitazama kwa huruma.

Mhe. Spika, sasa nimalizie la mwisho mswada huu pia una sehemu nyingi sana haja ya kuanzishwa serikali ambayo inaendeshwa kwa kutumia mifumo ya *electronic government* na kitengo kizima ambacho wanakiita *record information management*, napongeza sana hatua hiyo inayokuja na ikaifanya na serikali ya Mapinduzi nayo iende na wakati katika mabadiliko yaliyotokezea katika ulimwengu, na sisi tufike pahala tupate taarifa kwa kubonyesha kitufe tu katika kompyuta ukapata taarifa unazozihitaji.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo niseme sheria hii ni muhimu sana kama walivyosema wajumbe wengi hapa kwamba ni mwanzo mzuri, tumetoka pale tulipokuwa tukifanya kazi kwa mazoea au kila mtu anafanya kazi katika sehemu yake kwa kuzingatia tu maelekezo fulani lakini hakuna sheria hata moja inayoelekeza, hii imeweka vizuri inaonyesha misingi mikuu ya utumishi wa umma, inaweka kanuni za maadili. Inaweka taratibu nzuri za mtu kujua kwamba nimefanya makosa, umeweka utaratibu mzuri wa maslahi yao kulingwa nasema mambo mengi yamezingatiwa. Kutakuwa na mapungufu kwa sababu jambo lolote likianza linakuwa na mapungufu yake, lakini mapungufu hayo nafikiri yatakuwa pembeni wakati sheria hiyo inatekelezwa na baadae katika siku za mbele kama walivyopendekeza Waheshimiwa wajumbe hayo yatapatiwa ufumbuzi.

Kama nilivyosema Mhe. Spika, sheria hii ni muhimu kwa hivyo tuipitishe na nawaomba sana Wajumbe wa Baraza la wawakilishi wote kwa umoja wetu tuunge mkono hoja hii, tuupitishe mswada huu ili tufungue ukurasa mpya Zanzibar katika dhama nzima ya utumishi wa umma, ambayo naamini itakuwa chachu ya kuleta mabadiliko ya kiuchumi na kijamii katika nchi yetu.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo kwa niaba yangu na wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla sijawaita waheshimiwa wengine wanaofuata naomba nitoe taarifa ndogo kwamba ile semina ya *Zantel* ambayo ilipangwa siku ya Jumamosi, ndugu wetu wa *Zantel* wamekubali semina hiyo ifanyike siku ya Jumapili tarehe 30. Semina hiyo itafanyika Kiwengwa katika Hoteli ya *Ocean Paradise Resort.*

Sasa wahudumu watazungusha waraka fulani kwa sababu *Zantel* walikuwa wametayarisha usafiri, lakini bila shaka kuna Waheshimiwa Wajumbe wengine wana usafiri wao na wengine watakuwa hawana usafiri. Kwa hiyo, wale ambao hawatakuwa na usafiri na kwa maana hiyo watapenda kutumia usafiri unaotayarishwa *Zantel* wajiorodheshe humo.

Naomba tutumie nafasi hii ndogo iliyobaki ili wahudumu wazungushe kwa wajumbe wote wale ambao watapenda kutumia usafiri wa *Zantel* na waweke majina yao ili wajue ni mabasi mangapi ya kutupeleka huko. Naelewa kwamba wako baadhi ya wajumbe hawana usafiri, mimi ninao. Wahudumu karibuni.

Mhe. Haji Faki Shaali (Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii na napenda niunge mkono hoja kabla ya kuchangia lolote.

Mhe. Spika, mimi katika sheria ambazo zimeletwa katika Baraza hili nikaziona nzuri basi moja ni sheria hii. Nitaeleza sababu chache sana ambazo zinanifanya nione sheria hii kwamba ni nzuri sana. Kwanza nimekwenda katika kifungu cha 28 (3). Mhe. Spika, kifungu hichi kinatoa fursa kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kupokea Ripoti ya Utumishi Serikalini kila mwaka jambo ambalo Baraza lako tukufu lilikuwa hawapati fursa hiyo.

Kwa hiyo Mhe. Spika, lazima tujipongeze wawakilishi baada ya kuipitisha sheria hii kwamba itakuwa tumeweka mazingira mazuri ya kila mwaka kupokea na kuijadili taarifa itakayoletwa na waziri kuhusu utumishi wa umma Zanzibar. Hilo ni jambo moja zuri ambalo linatanua demokrasia katika nchi yetu.

Mhe. Spika, fursa kama hii tunaipata kwa Mkaguzi wa Mahesabu tu kwa kupitia Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali. Lakini ripoti nyengine kama hizi kwa kawaida inakuwa haziletwi katika Baraza.

Mhe. Spika, hata ukiangalia katika hotuba za bajeti za mawaziri zinaelezea kwa jumla tu juu ya mafanikio na changamoto za wizara zao, lakini bado hazielezi juu ya hali ya utumishi serikalini. Kwa hiyo, nasema hilo ni jambo moja la kujivunia sana kwa Baraza lako tukufu kwamba likiridhia sheria hii kupitishwa basi watakuwa wamejiwekea mazingira mazuri na wao ya kuweza kupokea taarifa ya utumishi serikalini kila mwaka.

Hayo yamefafanuliwa katika kifungu cha 31 vile vile kinazungumzia juu ya suala hilo hilo, lakini uzuri wa pili wa sheria hii ninaona mimi katika kifungu cha 37 cha mswada huu, ambacho kinaelezea juu ya majukumu ya Mawaziri, kabla ya hapo hakukuwa na sheria inayofafanua majukumu na uwezo wa mawaziri kisheria yalielezwa kijuu juu tu katika katiba na katika miongozi mingine ya serikali lakini hayakuwa na nguvu za kisheria. Kwa hivyo mswada huu utakapopita itakuwa uwezo wa waziri upo kisheria.

Hivyo hivyi kamati ya Makatibu wakuu ambayo ni Kamati ya watalam wetu wanaolisaidia Baraza la Mapinduzi nayo ilikuwa inafanya kazi nzuri kwa mazoea lakini haikupata uhalali wa kisheria, ka hivyo chombo kikuba kama hichi kinachofanya kazi kwa niaba ya Baraza la Mapinduzi kuwepo bila ya misingi ya kisheria si jambo zuri sana, kwa hivyo mimi nataka nimpongeze mwenzangu Mhe. Waziri kwa kuleta mswada huu mzuri ambao unaondoa matatizo yaliyokuwepo katika nchi.

Lakini haukuishia hapo tu hapa wameeleza vile vile majukumu ya Katibu Mkuu nayo yalikuwa yameelezwa katika vitabu maalum vinavyoeleza majukumu mbali mbali ya serikali, lakini yalikuwa hayana nguvu za kisheria lakini sasa hivi majukumu yao yamelezwa kisheria katika kifungu cha 40 cha mswada huu, ndio nikasema huu mswada kama ingekuwa ni chakula sijui nilinganishe na chakula gani kwa uzuri wake. Maana umeondoa matatizo mengi yaliyokuwepo ni mzuri mno.

Halafu umeeleza majukumu wakati Makatibu Wakuu na wao sasa watakuwa wanafanya kazi kwa kujiamini kabisa, kwa sababu wamepewa nondo ya kufanyia kazi walikuwa wanafanya kazi lakini walikuwa hawana nondo ya chuma ilikuwa nondo ya mti. Lakini sasa hivi makatibu Wakuu tumewakabidhi nondo ya chuma kwa hivyo tunategemea baada ya mswada huu kupita watakuwa na nguvu kubwa ya kusimamia nidhamu na uwajibikaji kama inavyoelekezwa katika kifungu cha 45 cha sheria hii.

Mhe. Spika, ukiacha hayo mazuri machache ambayo nimeamua kutaja kuna kifungu cha 59(1) hichi nadhani ndicho kitakachofanya wajumbe wote waunge mkono mswada huu. Masharti ya kuingia katika utumishi wa umma labda Mhe. Spika, kwa ruhusa yako nisome kidogo. Kifungu hiki kinasema hivi naomba kunukuu,

Kifungu cha 59(1)	Ajira katika utumishi wa umma kwa mashari ya malipo uzoeeni utakuwa kwa Wazanzibari tu.

Mhe. Spika, haya ni mambo ambayo muda mrefu Waheshimiwa Wajumbe walikuwa wanalilia na kilio chao serikali kwa kupitia wizara hii kimeyasikia. Kwa hivyo, sasa fursa ya utumishi wa umma kwa masharti ya malipo uzeeni, hii itakuwa ni haki yetu sisi Wazanzibari tu, wasiokuwa Wazanzibari wataajiriwa lakini kwa mikataba maalum, sio kwa masharti haya kama tunavyopata sisi.

Mhe. Spika, nasema hili ni jambo moja ambalo mimi binafsi yangu nalifurahia na kila mwananchi atakayesikia mswada huu kwamba unalinda haki za Wazanzibari, basi najua atalifurahika suala hili.

Mhe. Spika, mimi kwa kumalizia, nataka niwashauri Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu wote, kwamba hapa Barazani kwa bahati nzuri sheria zote karibu ukizitaka unazipata katika Afisi ya Katibu, ukionana na Bi Moza ukimwambia nahitaji sheria Fulani, basi atakupatia kitabu utafanya *reference* na itakusaidia. Sasa naomba hilo kwanza tufanye.

Mhe. Spika, hapo hapo nataka niunganeshe kitu, kwamba huu mswada wa sheria Mhe. Spika, ambao unahusu utumishi wa umma hauzungumzi kila kitu kuhusu wafanyakazi, lakini umejikita zaidi katika miundo ya utumishi wa umma. Sasa kuhusu masuala ya maslahi ya wafanyakazi na mambo mengine yanayohusiana na hayo, yanaonekana katika sheria nyengine.

Nakumbuka Mhe. Spika, chini ya uongozi wako, kama sikosei itakuwa ni mwaka 2004 au mwaka 2005, wajumbe wako tulipata fursa katika hoteli ya Nungwi ya Baobao ile, tulifanya semina ya siku mbili chini ya Mhe. Samia nadhani wakati ule ndio alikuwa waziri anayehusika na masuala ya kazi. Tulifanya semina ya miswada miliwi ambayo ilikuwa inahusiana na kazi.

Mswada mmoja nakumbuka Mhe. Spika, ulikuwa ni mswada wa sheria ya usalama kazini na tukaupitisha kwa sheria. Kwa hivyo, ipo sheria ya usalama kazini. Sina uhakika na hiyo miaka kama nilivyosema, itakwa ni mwaka 2004

au 2005. Mhe. Spika, AG ananiweka sawa kuwa ni mwaka 2005, ni siku nyingi zimepita. Nakumbuka tulikaa Nungwi siku mbili.

Halafu kuna mswada mwengine wa sheria unaohusiana na mambo haya haya ya kazi, lakini kidogo jina la ile sheria nimelisahau. Kwa ufupi nataka niseme tu kwamba sheria zinazohusiana na mambo ya kazi zipo na huu mswada umejikita zaidi kama unavyojiele hapa, zaidi ni miundo ile ya utumishi na haifafanui maslahi ya wafanyakazi. Mambo mengine zaidi nadhani ufafanuzi wake yatapatikana katika *scheme of service*. Sasa mambo kama hayo tusiyatarajie *scheme of service* kuyakuta katika mswada kama huu wa sheria.

Mhe. Spika, kwa wale wenzetu ambao ndio kwanza wanaingia kilingeni, labda tusaidiane kidogo kitu kimoja. Kwa kawaida miswada ya sheria ikishapitishwa kuwa sheria, waziri anayehusika huwa anatayarisha kanuni. Kwa hivyo, mambo mengine hayawezi yakaonekana yote katika sheria, mengine yatakuja katika kanuni. Kwa hivyo, mambo mengine nadhani yaliyokuwa tunazungumziwa humu hayawezi yakaingizwa katika sheria, maana tena hiyo sheria itakuwa ni mzigo mkubwa sana, kwa hivyo mengine tutayakuta katika kanuni.

Mhe. Spika, imani yangu ni kwamba baada ya kuridhia mswada huu kupitishwa, bila shaka hata kanuni za utumishi serikalini yaani *General Order (GO)*, litabadilika na zitakuja kanuni mpya. Kwa hivyo, humo katika *General Order* ndio mambo mengi haya yatajitokeza.

Mhe. Spika, baada ya kueleza machache hayo, kwa sababu mimi nimepata fursa katika Baraza la Mawaziri kuchangia mswada huu na leo kwa mara ya pili nimepata fursa ya kushirikiana na wenzangu katika kuuchangia mswada huu, naona niishie hapo na kwa mara ya pili tena nirudie *tradition* yetu ya nyuma kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia, ahsante sana *(Makofi).*

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, na mimi niungane na wenzangu kukushukuru kunipa nafasi kwa mara nyengine tena, ya kushiriki katika mjadala huu kusaidia kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya mambo kama vile walivyofanya wenzangu.

Naomba pia kushukuru kwamba serikali ya Mhe. Dk. Shein imeunda hii wizara ambayo inasimamia masuala ya utumishi. Ni kweli tulikuwa tunaendesha serikali na shughuli zikienda, lakini zilikuwa zinaishia kwenye Kurugenzi ya Utumishi Serikalini. Sasa kuja kwa wizara kamili na kuzingatia masuala ya sera ya utumishi na kuleta waraka huu, unatusaidia kuanza upya au kujisahihisha.

Mhe. Spika, juzi tulikuwa kwenye semina kule kujadili hii kama mtaalamu alivyokuwa akituambia. Baada ya kutoka wengi wa wale waliokuwa pale waliokuwa nje ya wawakilishi, aidha walikuwa ni wanafunzi wangu au ni mtu tuliyefanya naye kazi. Mhe. Spika, bahati mbaya au nzuri mimi ni mtu wa masihara sana. Mmoja akaniambia, Babu Juni sisi tulitegemea baada ya nyie wataalamu muliobobea na mumeingia kwenye serikali mnatuletea waraka wa aina hii, aah! Babu Juni nakutizama kwa njia ya ajabu. Sasa mimi nikamwambia kwani kabla ya hapo ukiongozwa na waraka upi. Akaanza kunitizama. Nikamrudia kabla haijaja hii sheria, ulikuwa na sheria gani iliyokuongoza. Basi akacheka, akasema ilikuwa hakuna. Nikamwambia sasa bora ipi, bora kuwa na hii ambayo wewe una matatizo nayo, au kuwa haipo. Akasema bora hii. Nikamwambia basi twende, tutarekebisha kila tunavyokwenda.

Mhe. Spika, mimi bahati nzuri nilikuwemo katika serikali kama mwajiriwa na nilishawahi kuwemo kama mtendaji mkuu, sio vizuri kusema nilikuwa na vyeo gani, lakini niliwahi kuwa Katibu Mkuu, nikawa tunakumbuka kulikuwa na ile *plan commissioner*. Kwa hivyo, nilikuwa katikati ya mambo yanayohusu mambo haya.

Kwa hivyo, tunaomba tufahamu kwamba moja katika utaratibu wa kuajiriwa serikalini, unaweza ukapanda cheo au ukashushwa, ndio kawaida. Mara nyinengine kunakuwa na sababu nyengine. Mimi sipendi kujitolea mfano lakini panapo lazima katika kutoa maelezo hujitolea mfano. Mimi nilikuwa Katibu Mkuu Afisi ya Waziri Kiongozi, nikawa mwalimu wa kawaida Mikunguni, sikukatiwa mshahara wangu, nilikatiwa maslahi ya kuwa Katibu Mkuu, nilikosa haki ya kuwa na madaraka ya kuamrisha. Lakini nilikuwa mwalimu wa kawaida mshahara wangu ule ule niliotoka nao Afisi ya Waziri Kiongozi nilikuwa nao na nikilipwa huo. Kwa utaratibu wa utumishi mshahara huo unaitwa *personal to your self*, unakuwa hauongezeki lakini haupunguwi. Ni kulinda heshima ya utu, kwamba huyu mtu alikuwa anapata Shs. 10, hebu muachieni hizo Shs. 10 nyinyi mtakosa nini.

Kwa hivyo, hoja hii ya kuonekana kuwa Katibu Mkuu atapata mshahara ule ule, kwamba anakuwa kastaafu, hana madaraka ya kuamrisha kama aliyonayo yule aliyeko kwenye kiti. Kwa hivyo, tusiseme hakustaafu kwa sababu tu anapata mshahara ule. Nakumbuka kwenye semina nilieleza kwa urefu kuwa hiki ni kitu cha kawaida ma-*brigadier* wa jeshi wakishastaafu pesa zao zinakuwa ni nyingi hata kuliko huo mshahara na marupurupu pia wanapata. *Gavana* wa Benki Kuu akistaafu, nilitoa mfano vile vile viongozi wa kitaifa hawa ni hivyo hivyo, tena sio kwa Zanzibar tu, hata Marekani na nchi nyengine zozote. Kuna heshima fulani ukishafikia kwenye utendaji wa serikali inabidi ulindwe kwa sababu ni heshima ya kiserikali.

Mhe. Spika, kuna taasisi inaitwa (*TRA),* yaani *Tanzania Revenue Authority,* ni moja katika watu wanaolipwa mishahara mikubwa sana katika nchi hii. Watu walikuwa wanasema kwa nini hawa wanalipwa mishahara mikubwa. Wanalipwa mishahara mikubwa kwa sababu ni watu wanaokabili vishawishi. Binadamu ana tabia yake, lakini angalau basi mpe maslahi na mshahara na marupurupu ili asione ile sababu ya kusema basi nigaiye ipunguwe, yaani rushwa.

Hivi karibuni nilikwenda kutoa gari pale Dar es Salaam *baggage room,* nilikuwa huku Zanzibar nimeshalipa, lakini niliambiwa lazima uende tena Dar es Salaam. Basi kuna kijana pale ukimuone pale kwenye alipokaa na mavazi yake vile alivyovaa na mbwembwe, basi unaona huyu jamaa anashiba. Sio mchezo bwana, ukiitizama shati yake na zile mbwembwe na ubani anavyotafuna huku anazunguka kwenye kiti. Basi aliniambia aah! Mheshimiwa, hii nimeitia hapa, nadhani inabidi ulipe milioni 2.00 zaidi. Lakini anakuambia ulipe milioni 2.00 zaidi wala hana wasi wasi, wala hakuambii basi zungumza, kwa sababu hana tamaa. Ni kwa sababu amepewa malipo yanayostahiki kwa ile kazi. Kwa hivyo, Mhe. Spika, kuna mambo mengine haya ni lazima vitu hivi vizingatiwe.

Nakumbuka Mhe. Spika, siku ya semina ndugu Masoud pale, alisema haipendezi na sio vizuri kwa kiongozi wa serikali. Mimi nilijua anamtolea mfano nani. Kwamba kawa Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi, halafu anakwenda kuwa karani wa Baraza la Mji, yaani *town clerk,* ati tu anaitwa Mkurugenzi. Lakini juzi ndiye alikuwa anajua siri za serikali na alikuwa ndio mtu wa kwanza anayemuona baada ya Rais, hata Waziri Kiongozi huwa hajafika, basi anafika yeye kwanza kwa Rais. Halafu kesho kutwa unamkuta anatembea na malapa, kisha anakuita pembeni, Babu Duni hee, basi maana yake leo mambo hayajakaa vizuri kule nyumbani. Haipendezi kwa viongozi wa serikali.

Kwa hivyo, tunaposema kwamba kiongozi mstaafu alipwe marupurupu au mshahara wake, hatuna maana ya chochote isipokuwa kulinda heshima ya serikali. Hilo la kwanza.

Lakini la pili, kuna kidogo mazowea Mhe. Spika, nisamehe kutizama cheo ukamtizama mtu ni hatari. Cheo hiki anaweza kuwa Babu Juni leo kesho akawa Makame na keshokutwa akawa Haji Kheir au Hamadi Masoud. Ni cheo tunalinda wadhifa wa serikali, hatumlindi mtu, tunalinda heshima ya serikali.

Mhe. Spika, kuna kitu, nadhani Mhe. Abubakar Khamis anajua wanaita *security of tenure,* yaani usalama wa kazi. Majaji ni watu wenye vishawishi.

Mhe. Mwanasheria Mkuu ananitizama pale. Hawa huwa nao wanapewa kila linalostahiki katika kazi ili kuhakikisha kwamba wanalindwa kazi yao. Kulindwa kazi yao ni kama unakaa pale na kusema Babu Juma muachie huru, hufanyi kwa sababu tu amekushawishi kitu fulani na hufanyi kwamba labda kesho utafukuzwa. Ndio maana Majaji Rais anawateuwa lakini kuwafukuza ndio tabu. Nadhani ni kweli Mhe. Spika. Jaji Mkuu akishamuweka pale basi sio rahisi kumwambia kesho nakuondoa, kwa sababu kuna kitu kinaitwa *security of tenure*.

Kwa hivyo, hizi ni tabia za kuendesha serikali, hatuwezi kuziepuka. Nashukuru sana Mhe. Spika, kwamba angalau leo unapotaka kuja kudai haki yako kama mfanyakazi, unaweza kusema kwamba nadai haki hizi kwa sababu kuna sheria ya utumishi serikalini.

Namshukuru Mhe. Haji Faki Shaali ambaye ni Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum, alieleza habari ya *scheme of service*, yaani muundo wa utumishi. Kuna mjumbe mmoja hapa alisema hata hizi diploma zinatofautiana. Ni kweli, diploma uliyokwenda miaka mitatu ya afya, sio diploma uliyokwenda miaka mitatu ya Mzumbe. Kwa hivyo, diploma uliyokwenda miaka mitatu ya afya, utalipwa kwa kulingana na kazi inayohusu afya na diploma ya miaka mitatu ya Mzumbe utalipwa kulingana na kazi inayohusu shughuli za utawala au uchumi. Hizo diploma vile vile zina *grade*, mnaweza kuwa nyote mko kwenye diploma lakini zina *grade*.

Mhe. Spika, hata ile *increment*, kwamba kuna *automatic increment*, mwaka ukiisha anaweza kuwa mmoja nyongeza yake ni Shs.20,000/- na mwengine akawa nyongeza yake ni Shs.50,000/- kulinganana kiwango kile. Sasa msingi huu ndio unaosababisha iwepo hiyo *scheme of service* na hiyo *scheme of service* ndio inayotuwezesha kujua kazi zako nini na mimi kama msimamizi nitaweza kusema kwamba kazi ni yako lakini hukuifanya. Hivi sasa nasikitika kusema kuna mambo mengi tunafanya kwa mazowea na kufanya kwa mazowea, kuna hatari yake kwamba unaweza ukampa mmoja zaidi na mwengine usimpe zaidi, ambapo mmoja akalalamika mbona mimi sikupewa ukawa huna kinga.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, nawaomba waheshimiwa wenzangu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba tuupitishe mswada huu, angalau sasa tunapoanza kuendesha mambo yetu iwe serikali nzima inajua kwamba tunaendesha kwa misingi ya sheria badala ya vile matakwa ya mtu yanavyotaka.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nampongeza Mhe. Waziri Haji Omar Kheir, Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora,

kwamba pamoja na upya wake katika wizara na pamoja na muda mchache aliyokaa pale, basi wameweza kuja na kitu tukapata kusema sasa tunaanza kuendesha serikali kwa utaratibu unaostahiki. *(Makofi).*

Mhe. Spika, kuna mambo yanaweza kuwa yana upungufu, lakini sheria zote ndivyo zinavyokuja na ndio hivyo hivyo. Tunakuja hapa tunafanya marekebisho ya sheria, tunakwenda tena baada ya miaka mitatu yanafanywa marekebisho tena. Kwa hivyo, hakuna kitu kilichokamilika, kwa hivyo hayo yatakuja kila siku zinavyoendelea. Kwa kweli tuipongezeni serikali kwamba imeweza kuleta hili.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia juu ya mia, nakushukuru sana *(Makofi).*

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Spika, kwa kupata fursa hii ya kuchangia mswada huu. Kwanza nikupongeze wewe kwa saa hizi kunipa fursa hii. Vile vile nimshukuru na Mhe. Waziri kwa kuleta mswada wake huu.

Kwa kweli mimi nizungumzie kuhusu sehemu ya 11 ya masharti mengineyo, katika ukurasa nambari 53 kifungu nambari 99(1), naomba ninukuu.

> "Kwa mujibu misingi ya utumishi wa umma, taratibu za uongozi na uendeshaji wa utumishi wa umma utazingatia jinsia na kuweka uwiano wa kijinsia kwa kadiri itakavyoonekana".

Mhe. Spika, hapa sijui kama ni kwa ufahamu wangu mdogo au vipi, kama masharti haya yatawekwa, aidha kama tunafuata jinsia. Tunapokwenda kuomba kazi, sijui kama kutakuwepo na zingatio gani, yaani unapokwenda kuomba kazi afisini, utaambiwa kwamba kwa mujibu wa kazi hii labda ni ya mwanamke au ni ya mwanamme, sifahamu hapa. Je, Mhe. Waziri au hiyo tume ya utumishi wa umma itazingatia haya kwamba hapa tunataka mwanamke au hapa tunataka mwanamme, kazi hii ni ya mwanamme au kazi hii ni ya mwanamke. Kwa hivyo, hapa sijafahamu, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja baadae kutoa majumuisho, naomba anifafanulie hapa, kwa sababu sisi ni wanawake na tumesema kazi zote tunaziweza.

Kwa mfano Mhe. Spika, kuna ma-*engineer* wanawake wazuri tu. Sasa kama kutakuwa na masharti haya, nahisi kuwa tutafika pahala labda tutakosa wafanyakazi kwa kutizama jinsia. Hasa nina wasi wasi na mimi nikiwa ni mwanamke na ikiwa sikuingia pahala ambapo panaonekana labda hapa mwanamke atakoroga au atafanya suala jengine lolote. Kwa hivyo, Mhe. Spika, akija Mhe. Waziri hapa kidogo anisaidie.

Suala la pili Mhe. Spika, ni kifungu nambari 100 chenye kifungu kidogo (1), kinasema,

> "Hakuna mamlaka yoyote ya uajiri katika utumishi wa umma itakayoagiza mtu yeyote katika utumishi wa umma, kupima kama ana maambukizi ya Ukimwi kwa ajili ya kufahamu hali ya mtu huyo, kwa madhumuni ya kumuajiri".

Mhe. Spika, niseme kwamba kwanza hii tusiiweke sasa hivi kuwa Ukimwi ni *issue,* sijui kama itaingia nikisema *burning issue* au vipi, isiwe *issue* hiyo, kwa sababu ni maradhi sasa hivi ya kawaida na watu wameshayazowea na wanasema kuwa watu wanaishi kwa matumaini, hata wao wenyewe watu wanakuwa hawajifichi, wanasema kwamba mimi nimeathirika na kwa sababu *privilege* nyingi tu ambazo anazipata mgonjwa wa Ukimwi. Kuna maradhi hatari zaidi ya Ukimwi. Uzoefu ni kwamba ukiomba ajira unakwenda *medical examination.* Kwa hivyo, huu tusiutenge tukauweka pahala tukaita ni *issue*. Mimi nafikiria kwamba iwepo pamoja na matatizo mengine ambayo ni hatari zaidi.

Mhe. Spika, tukisema kwamba mgonjwa wa kifua kikuu labda umekwenda kumpima na ukamuona labda ataambukiza. Lakini ugonjwa wa Ukimwi tumeshapata mafunzo mengi tu kutoka kwa washauri nasaha na hasa tukizingatia kila mtu anaambiwa kuwa mkiingia viwanjani labda mvae viatu na kadhalika. Kwa hivyo hii ni jambo la kawaida, lisionekane kila siku tunalitenga mpaka watajihisi hawa wenye matatizo haya kwamba labda bado tunawatenga mpaka kwenye sheria zetu. Kwa hivyo, iwepo katika sehemu moja tu ya kwamba mwajiriwa unapotaka kuajiriwa, basi unakwenda *medical check,* hivyo iwe ni pamoja na matatizo mengine ya kiafya. Kwa kweli ni muhimu kupima afya zetu.

Mhe. Spika, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Amani ambao wameniteua, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia, ahsante sana Mhe. Spika (*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, nakushukuru sana. Hata hivyo nilikuwa nimeshaingia unyonge kidogo, naona nimesimama muda mrefu nilikuwa sipati nafasi. Lakini nikafikiri labda umefikiri mimi ni miongoni mwa wafanyakazi wako, kutokana na hizi nguo nilizovaa mimi na hawa wafanyakazi wa humu ndani. Kwa hivyo, kila niliposimama sipati nafasi nikaseme Mhe. Spika, anafikiri labda na mimi ni mfanyakazi wa humu ndani, lakini nashukuru hatimaye umenipatia. Kwa sababu hata mishono inalingana.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na nitangulie kwanza kusema kwamba kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Makunduchi naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja, na ninawaomba wajumbe wote tuunge mkono.

Aidha, naomba nichukuwe nafasi hii Mhe. Spika, kumpongeza Mhe. Rais kwa kuunda wizara hii ya utumishi wa umma na utawala bora. Kwa kweli ni wizara ambayo ni muhimu wana. Pia nimpongeze Mhe. Rais kwa kumteua Mhe. Haji Omar Kheir kuiongoza wizara hii na mimi nina hakika kwamba *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akitujaalia basi mambo yatakwenda vizuri.

Mhe. Spika, katika mswada huu kila kifungu unachokiangalia ni kizuri na kina maana kubwa. Kwa hivyo, mswada huu umekusanya kila kitu.

Mhe. Spika, naomba nitowe hadithi moja. Kule Makunduchi kulikuwa na mzee wetu mmoja alikwenda dukani, akauliza sijui kama vijana wa siku hizi wanajua kuna kitu kinaitwa buluu, akauliza buluu ipo, akaambiwa ipo, akauliza majani ya chai yapo, akaambiwa yapo, akauliza sukari ipo, akaambiwa ipo. Basi akasema duka hili kila kitu kinapatikana. Kwa hivyo, ikawa ni duka ambalo limekusanya kila kitu. Kama mswada huu umekusanya kila kitu kizuri. Lakini alipouliza tangawizi ipo, akaambiwa hapana. Basi akasema duka hili hapana kitu chochote, kwa kuuliza kile kitu kimoja hapana ndio ile sifa ikaanza kuondoka. Lakini Mswada huu ni tofauti na hivyo.

Niunganishe na hapo hapo Mhe. Spika, kwamba mswada huu umekusanya mambo mengi, hata yale mambo ambayo baadhi ya waheshimiwa wameyazungumza, sikusudii kuwa najibu hoja, lakini nitamsaidia waziri mwenzangu katika baadhi ya mambo ambayo yamo humu ndani.

Kwanza nikupongeze sana Mhe. Waziri kwa kupitia kwako Mhe. Spika, kwa ile semina ambayo iliandaliwa juzi. Nilifurahi sana kuona vyama vya wafanyakazi au shirikisho lile la wafanyakazi wamealikwa na wamefurahi kweli. Nashukuru sana hata Mhe. Ismail Jussa naye katika kuchangia naye alichangia jinsi ya walivyoshirikishwa na umuhimu wao.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri ajitahidi sana, hasa kwenye ile Tume ya Utumishi Serikalini, kama kuna utaratibu na sifa zinazohitajika pengine kwenye vyama hivi au shirikisho la wafanyakazi wanazo sifa kama hizo, basi sio vibaya mmoja au wawili wakaingizwa kwenye nafasi kama hizo ili nao wajisikie zaidi.

Mhe. Spika, kwenye mswada huu bahati nzuri kuna suala limeelezwa humu na mjumbe nadhani kama sikosei, Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Konde,

alizungumza kuhusu suala la usalama wa afya kazini. Ni kweli, hata katika muundo wa wizara yangu nimependekeza. Natarajia *Inshaallah* Mhe. Spika, kama litakubalika kwamba tunaanzisha Idara ya Afya na Usalama Kazini.

Mhe. Spika, nilipokuwa nausoma mswada huu, katika kifungu cha 79(3)(p), kinasema hivi;

> "wajibu wa kutoa usalama na kuwapatia vifaa vya kinga waajiriwa katika ngazi zinazohitaji kinga hiyo".

Hii ina maana kwamba mswada huu umekusanya kila kitu ambacho kimehitajika kiwemo, ni muhimu sana. Alipozungumza suala la walimu, chaki na mavumbi yale. Lakini ile ndio kazi ya walimu sote na mimi natokea huko huko, lakini hatima yake ndio nimefika hapa, pengine unga ule wa chaki una baraka kidogo.

Mhe. Spika, mimi sikumbuki katika maisha yangu tokea nilipokuwa mwanafunzi, mpaka nimemaliza kwamba kumkuta mwalimu kajifunga kitambaa kama kile cha watu wanaofanya upasuaji, sijawahi kumuona. Kwa sababu Mwenyezi Mungu naye ana hifadhi zake. Kuna maeneo ambayo ni ya hatari ya wafanyakazi. Mfano kwenye mambo ya vyombo vile vya ufundi, pengine kwenye karakana na maeneo yale ambayo mhandisi Mhe. Hamad Masoud atakuwa anaelewa zaidi kule na kuna maeneo mengine kama hayo. Kwa hivyo, sisi kwa upande wetu kiwizara, tumeliona na tunaliangalia vizuri.

Vile vile alizungumzia kuhusu suala la nyongeza pamoja na mambo mengine ya mishahara. Mhe. Spika, wakati nilipokuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tulifanya utaratibu wa kuwaangalia, kwa sababu alilalamika kwamba nyongeza zimesimama.

Kwa kweli kuna kipindi nyongeza zilisimama, lakini baadaye zilirejeshwa zile nyongeza kwa utaratibu ambao uliwekwa, kiasi ambacho wale walimu ambao walikuwa ni *senior teacher* waliangaliwa kwa vizuri zaidi. Lakini ninahakika baada ya mswada huu kuna maeneo mengine pamoja na sekta nyengine nazo zitaangaliwa.

Mhe. Spika, mswada huu umekuja wakati ambao unafaa kabisa katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa, tunahitaji kuwa na masuala kama haya. Kwa hivyo, ni vyema Waheshimiwa Wajumbe sote tuwe kitu kimoja na kuunga mkono mswada huu.

Kwa hayo machache nadhani sina haja ya kuchukua muda wako mwingi zaidi Mhe. Spika, isipokuwa nikushukuru sana na nimpongeze sana Mhe. Waziri na

ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Vile vile niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wote tuunge mkono mswada huu. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza na mimi nataka nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri jirani yangu kwa kazi nzuri aliyoifanya kwa kushirikiana na watendaji wake wakuu ndugu Joseph Meza na ndugu Yakuti Hassan Yakuti pamoja na watendaji wao wengine wote. *(Makofi)*

Kwa kweli wamefanyakazi nzuri licha ya upya wa Mhe. Waziri, lakini kazi hii ambayo wametuletea hapa napenda kusema kwamba nzuri sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwanza nataka niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kuunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja, kwa faida yetu sote, kwa watumishi wetu pamoja na nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nimejaribu kuwasikiliza kwa makini sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Kwa hiyo, nataka nichangie maeneo mawili matatu, ili kusaidia pale ambapo Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho.

Kwanza nataka niwaambie Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuhusu madhumuni ya mswada huu kama yalivyoelezwa ndani ya waraka na Mhe. Waziri ni kuweka Miundo, Uendeshaji na Usimamizi wa Utumishi wa Umma unaolingana na viwango na utekelezaji wa kimataifa. Mhe. Spika, hapa ndipo pa kuanzia unao lingana na viwango na utekelezaji wa kimataifa.

Hivi sasa dunia *is global village* na wala hatuwezi kwenda na utumishi wa aina yetu au peke yetu na ukitaka kulinganisha huwezi unasema mtumishi wangu yuko hivi mbona wa Kenya yuko vile unalinganisha na nini, wakati sheria yako haizungumzii uwiano na sheria za wenzetu. Kwa hiyo, hapa nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri, kwa sababu anatuwekea viwango vya kimataifa. *(Makofi)*

Vile vile nataka niseme Mhe. Spika, panapo mtumishi kuna muajiri na muajiriwa. Sasa muajiri na muajiriwa wanapofanyakazi kila mmoja anataka kufikia ile *stage* ya *win win situation*, ukisema mmoja anataka kushindwa na mwengine ashindwe basi hapa ajira haipo.

Sasa katika mswada huu Mhe. Waziri kuna vipengele vingi sana ambavyo amevieleza kwa bayana tena kwa uwazi kabisa, kwamba tutaongeza nidhamu makazini. Mhe. Spika, nimewasikiliza Waheshimiwa Wajumbe walipokuwa wakizungumza na kusema kwamba Wazanzibari hatujitumi, basi mswada huu utatufanya Wazanzibari tujitume. Vile vile Wajumbe walisema kwamba hali yetu ya uchumi iko chini, kweli huwezi kuinua uchumi bila ya kujituma.

Kutokana na hali hiyo, utakapoongeza nidhamu katika kazi, naamini uchumi nao utakua, pia ninaamini ile *win win situation* itapatikana baina ya muajiri na muajiriwa, sasa muajiri ni serikalini na watumishi wetu. Kwa hivyo, mswada huu umeeleza kwa wazi kabisa na wala hauna utata Mhe. Spika.

Hata hivyo, mswada huu Mhe. Spika, umetilia maanani walemavu. Kwa mfano, leo Mhe. Spika alikuja mlemavu kuniona pale wizarani kwangu, basi ameshindwa kunifuata juu ghorofa ya pili na nimelazimika nimfuate yeye chini na kuzungumza naye pamoja na kumalizana.

Mswada huu unasema kutakuwa na acssebility kwa ajili ya walemavu kutufika sisi. Nadhani hapa ndipo tutakapoanza kurejebisha majengo yetu kwa kupitia mswada huu. Mhe. Spika, leo sisi wazima tunaona ni kazi, lakini wenzetu walemavu wanaumia, lakini kuwepo kwa mswada huu utawasaidia sana ndugu zetu walemavu. *(Makofi)*

Pamoja na hayo, mswada huu umechangamkia suala la zima la kutomnyanyapaa mtu mwenye maradhi ya UKIMWI, yaani mswada wetu unasema hapana kupima kwa UKIMWI kwa sababu ya ajira jambo hili lisiwepo, kwa sababu hatutaki kuwanyanyapaa wewe una UKIMWI huwezi kufanyakazi hii mswada huu umeweka bayana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nataka niseme mswada huu kwa kweli sasa unakwenda na viwango vya kimataifa.

Pia jambo jengine Mhe. Spika, mswada huu umetuwezesha kutambua mwenendo mzima wa mtumishi wa ki-*carrier*, yaani kwamba mimi nimeajiriwa naanza wapi na Mwenyezi Mungu akinijaalia nitakapofika miaka 60 kama sijapata cheo nitakwenda vipi na hapo awali ilikuwa haiwezekani. Kwa kweli mtu anasubiri rehema za Rais usikie kwenye redio ndio umekua, lakini mswada huu unakwambia wewe baada ya kipindi fulani unaondoka nasafi hii unakwenda nafasi nyengine.

Mhe. Spika, mimi kama waziri mwenye dhamana ya fedha mswada huu umenisaidia. Hivi sasa ile *wage bill* itakuwa ya uhakika Mhe. Spika na huko nyuma ilikuwa tunakwenda, yaani unasikia tuweke au tuongeze kiasi gani kwa ajili ya mishahara.

Kwa hivyo, mimi sasa nitakuwa nikifanyakazi na Waziri wa Nchi (AR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ajili ya kunipa *statistics* zote na kuniambia ninaowapandisha madaraja, ninaowapandisha mishahara na

nitakaowaajiri mwaka huu ni wangapi. Kwa hivyo, itanipa ile *wage bill* in *real sense* na sio huko nyuma Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mswada huu kwa kweli sasa unakwenda na vile viwango vya kimataifa.

Pamoja na hayo, mswada huu sasa imefika wakati kuwalinda wataalamu wetu. Mhe. Spika, huko nyuma mtaalamu anaajiriwa na wala hajui anakwenda vipi. Sasa hapa mtaalamu anaingia anakuwa na *package* inayomuonesha ile *working carrier* yake itaanza utaratibu wa kuwalinda.

Mhe. Spika, kama nilivyosema katika ajira yoyote ni *win win situation*, yaani Utumishi na Hazina wote wapo, sasa tutakuwa tunakaa pamoja. Kwa maana hiyo, sasa Waziri wa Utumishi na Waziri wa Hazina tunakaa pamoja kwa ajili ya kuangalia tunakwenda vipi katika maslahi ya wafanyakazi kwa kutumia pamoja na sheria nyengine. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nimewasilia Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wengine wanasema baada ya miaka miwili sheria tuirudishe, wengine wanasema bado vipengele hivi na vile.

Nadhani huwezi kwenda kabla ya kuanza kutambaa, yaani wazungu wanasema *something is better than nothing*. Sheria hii ni bora kuwepo na halafu tuje tui-*practice* na tuone kama kuna vifungu vyenye matatizo na wala hatujajifunga kuifanyia marebisho Mhe. Spika. Kwa hivyo, wale waliosema baada ya miaka miwili, mimi nasema hatujifungi hata baada ya miezi 6 kuifanyia marekebisho. *(Makofi)*

Kwa mfano, Mhe. Spika kuna sheria ilifanyiwa marekebisho juzi tu na Baraza lako tukufu na mimi naileta sasa kuifanyia marekebisho. Kwa kweli marebisho sio kwamba mmekosea ndani ya sheria, yaani marekebisho mnakwenda na *momentum* ya mabadiliko ya kiulimwengu.

Kwa hivyo, kama ulimwengu unabadilika kwa nini na nyinyi mbakie na sheria zenu zile zile, lazima mzibadilishe. Kwa maana hiyo, marekebisho kwa mujibu wa Mwanasheria Mkuu yanaruhusiwa ndani ya sheria zetu na wala tusiogope marekebisho. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sheria hii ndugu yangu Mhe. Ismail Jussa Ladhu amesema kuwa imeweka *E Government*, yaani itaturahisishia sisi kuweza kuona ni ajira ya kiasi gani tunayohitajia ndani ya serikali.

Lakini sheria hii uzuri wake Mhe. Spika, hapo zamani ilikuwa Tume yako ya Baraza la Wawakilishi inakutana kwake, ili ya Serikali Kuu inakutana kwake na ile ya Mahakama inakutana kwake hata kama mnamatatizo hamuwezi mka-*exchange notices* na leo tunakutana, yaani kuna chombo ambacho kinatukutanisha Mhe. Spika kwa uwiano na kuweza ku-*exchange notices*. Kwa mfano, Mahakama, Baraza lako tukufu na Serikalini tukajua matatizo ya kiutumishi ni yepi, baadaye kwa umoja wetu tunaelewa kumbe matatizo yetu ya kiutumishi ni haya yanayotusumbua. Kwa hiyo, sheria hii imetukutanisha.

Mhe. Spika, nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu tuunge mkono mswada huu kwa asilimia mia moja na mimi na naunga mkono mswada huu nasisitiza tusiogope mabadiliko yatakayokuja baadaye tutairekebisha sheria hii almuradi tunaweka viwango kulingana na wenzetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nataka nimalize kwa kusema kwamba Mhe. Waziri amefanyakazi kubwa tena nzuri, kwa sababu huwezi kusema unataka kufanya masahihisho kama kile unachokifanyia masahihisho huko nacho, *you need a plate in hand*, yaani kabla hujaanza hayo matayarisho yako. Kwa hivyo, *this is a plate* ambayo Mhe. Waziri ametupatia. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, nampongeza sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji na mimi naunga mkono mswada huu na ninawaomba tena Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu Mhe. Spika, kwamba tuunge mkono mswada huu.

Mhe. Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nishauriana na Mhe. Waziri kwamba kuna wajumbe wawili waje wachangie kesho nadhani wanataka ku-*exchange notices*.

Sasa nichukue nafasi hii kumpa *backbencher* wangu mmoja ambaye amechelewa kidogo kuomba, ili baada ya yeye tuahirishe hadi kesho kwa ajili ya kufanya majumuisho. Kwa hivyo, kesho watakaochangia kabla ya Mhe. Waziri ni pamoja na Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Mwanasheria Mkuu na hatimaye Mhe. Waziri.

Nafasi ya mwisho tumpe Mhe. Mussa Ali Hassan.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia mswada huu ambao ulikuwa mzigo tena mgumu kwa upande wa Wawakilishi. Mimi naunga mkono katika kuchangia mswada huu, kwa sababu

ni miongoni mwa wanakati ambao tuliujadili mswada huu. Kwa mfano, kwanza niliunga mkono vizuri mswada huu upitishwe kwa kuwa tayari nimeshaupitia pamoja na kuuchunguza na kuona unafaa kutumika hasa kwa vile ni mpya.

Kwa hivyo, naomba niwatoe wasiwasi Waheshimiwa Wajumbe wenzangu kwamba mswada huu ni mpya kwetu na kitu kipya chochote huwa kina ugeni, basi nadhani ni vyema kuunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja bila ya kuzuia kifungu hata kimoja tena sote kwa pamoja.

Kwa kweli tukisema tupunguze kifungu chochote basi ni sawa kupunguza mnyororo kijino kimoja na mnyororo huo hautokuwa mzuri. Mhe. Spika, mswada huu ni mzuri na utaongoza wafanyakazi wetu kuweza kujua majukumu yao wakati wote wa kazi.

Kwa mfano, hivi sasa wanafunzi wa kidato cha nne wamepata matokeo yao na wengi wao walikuwa na wasi wasi wa kupasi, lakini wengi wamepasi na mategemeo yao ni kupata kufanyakazi. Sasa watakapokuwa wakifanyakazi watakuwa na tamaa kuwa watashika nafasi za wazee ambao wameshapitisha mswada huu.

Kwa maana hiyo, mswada huu ni mzuri na utawapa tamaa kwamba waziri kusoma na wengi wao hivi sasa wamepasi kwa kiwango kikubwa na hata mimi mwanangu amepasi kwa kiwango kikubwa. Mhe. Spika, alinituma mwenyewe kwenda kwenye *internet*, basi baada ya kumpa jibu kuwa amepasi kwa kiwango kikubwa alilia machi kwa furaha na kusema kwamba baba umefanya jambo zuri la kunisomesha na ninatamaa nitashika nafasi yako baada ya miaka kidogo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mwanzo nilipoanza kuja katika Baraza lako tukufu, nilikuwa na wasiwasi kwamba nitaingia vipi katika Baraza la Wawakilishi mwaka huu, lakini baada ya kufika siku mbili, tatu basi nimeanza kujua hata mwendo wa kutembea wakati wa kuingia kwenye hili Baraza. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe ninakuombeni vifungu vyote vya mswada huu vilivyopitishwa na kamati basi vifungu hivyo ni halali tena vizuri na wala tusiwe na wasiwasi, isipokuwa tuhakikishi kuwa tunaviunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa hayo machache na kwa niaba ya Jimbo langu la Koani ninaunga mkono mswada huu upitishwe bila ya matatizo yoyote ili uwe sheria na kuweza kuendeleza kazi zake kwa faida ya wananchi yote wa Zanzibar.

Nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie kuhusu kifungu 31 ambacho kimenipa tamaa nzuri zaidi ya kumpa nafasi Mhe. Waziri kila baada ya mwaka

mmoja kuweza kurudia tena masuala haya Mhe. Spika naomba kunukuu kidogo.

Kifungu cha 31 kinasema hivi:-

> "Waziri kila mwisho wa mwaka wa fedha atawasilisha ripoti inayohusu utendaji wa utumishi wa umma iliyotayarishwa na Kamisheni chini ya Sheria hii pamoja na maoni yake na utekelezaji wa mambo yaliyoguswa katika ripoti katika Baraza la Mapinduzi na katika Baraza la Wawakilishi".

Kwa maana hiyo, utumishi huu tusiwe na wasiwasi kila baada ya muda utapitiwa na kutizamwa uhalali wake.

Kwa hivyo, naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, ninahoja baada ya mwaka mmoja nitengeneze *desks* zangu. Nadhani ni vyema tupige kwa utaratibu mzuri kwa ajili ya kupongeza itakuwa ni vizuri zaidi. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, ninakushukuruni sana kwa michango na mashirikiano makubwa. Kwa hiyo, kama nilivyoeleza mwanzo kwamba tunasitisha majadiliano kwa leo. Lakini kesho tutaendelea na majadiliano haya kwa kumsikiliza Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, baadaye Mhe. Mwanasheria Mkuu na hatimaye tumalizie Mhe. Waziri anayehusika na mswada huu na kazi hiyo itafanyika mara baada ya kipindi cha maswali na majibu.

(Saa 1:30 Baraza liliakhirishwa mpaka
tarehe 27/01/2011 saa 3:00 asubuhi)